SUPA JACKPOT
TZS. 1,033,283,276
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## MIFUGO yafa kwa ukosefu wa malisho


ama
ALHAMISI SEPTEMBA 22, 2022
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 14

VITA MIMBA ZA UTOTONI NCHINI
UNFPA yataja mafanikio ikiwa na angalizo, Norway yakiri imevutiwa

Ushuhuda wa vita kuikabili saratani kupitia mikakati afya, mkoa Manyara

Ukurasa 15

DARASA LA NYWELE ZAKO...

Hivi ndivyo zilivyo, namna ya kuzitunza kwa ufasaha kiafya

• Namna kinamama kuziosha, steaming...

Na Dk. Mussa Zaganzi

MTU anaweza kujiuliza, nywele ni nini? Kitaalamu, Inatajwa ni nyuzi za protini zinazokuwa kwenye ngozi na ni moja ya wasifu unaomuelezea mwanadamu ni nani.

Kwa binadamu, nywele nyingi hupatikana kichwani, kwapani na maeneo ya faragha mwilini.

Namna ya kutunza nywele inatajwa kujumuisha kuziosha kwa maji ya vuguvugu na matumizi ya shampoo.

Hatua ya kwanza kuzisafisha nywele, inatajwa zinasafishwa kuondoa mafuta na uchafu unaoshikana na nywele, hasa kwa vile kwa baadhi ya watu huwa zinamaliza wastani wa wiki mbili, pasipo kuosha nywele.

Wenye nywele za asili huogopa kuziosha kila mara wakihofu zitasinyaa kuwa fupi. Njia bora inashauriwa, kwamba nywele zinapaswa kusafishwa walau kila wiki.

Pili, inaelezwa kwamba nywele inaweza kufanyiwa 'steaming' ambayo ni kitendo cha kuipa uhai nywele na hapo ipo katika namna nyingi.

Njia mojwapo inayoshauriwa kitaalamu na hufanyika kwa namna nyingi, zifuatazo zinatajwa kufaa: Kuchukua mayai matatu na yakatolewa viini vyake na inashauriwa vyema, ikatumika viini pekee; pia kuna kuongezewa vijiko sita vya asali.

Lingine, analitaja kuwa ni kuongeza mafuta ya parachichi kwenye nywele; hali kadhalika nywele kuwekewa mafuta ya kulainisha nywele, mfano habat sauda.

Baada ya hapo, la tatu analieleza ni kwa kuvuruga nywele, yenye mchanganyiko tajwa, kama mhusika hana muda wa kuandaa hiyo 'steaming' asilia, nunua kwa muuzaji unayemuamini.

Baada ya hatua hiyo, mwanamama anashauriwa kwamba, baada ya yote mtu apakae na mchanganyiko huo na kuvaa kofia ya kufunika.

*Mwandishi ni mtaalamu bingwa wa nywele na ngozi, anapatikana katika taasisi ya Natural Skin Solution na kazi hizo zinapatikana bure kupitia njia ya mtandao 'Online Skin Solution'. Simu yake ni + 255 713 039876.*

Hali halisi ya nywele zilizohudumiwa na zinazohudumiwa katika namna tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

UKURASA 13

Nipashe
Alhamisi Septemba 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581076
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Bunge laagiza benki, simu zibanwe tozo



**WIZARA** yafafanua kuhusu msamaha miamala ya 30,000/ - ...*Endelea ukurasa 2*



## Tanzania, Msumbiji kupambana na ugaidi

UKURASA 3

Rais Samia Suluhu Hassan, akisindikizwa na mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Filipe Jacinto Nyusi, alipokagua gwaride la heshima baada ya kuwasili Ikulu ya Maputo, nchini humo jana. **PICHA: IKULU**

## Wafugaji kuku walia udumavu wa vifaranga

UKURASA 2

**MICHEZO** MGUNDA SASA AMULIKA MAMBO MAWILI SIMBA UK.24

**KABWELA** UK. 7

## Wafugaji kuku walia vifaranga dumavu

**Na Halfani Chusi**

JANGA jipya limewakumba wafugaji wa kuku nchini baada ya kubainika kuwapo kwa mbegu dumavu ya vifaranga.

Wakizungumza na Nipashe jana kuhusu uwapo wa vifaranga dumavu, wafugaji hao walisema wamekuwa wakipata hasara na kuwakatisha tamaa ya kuendelea na biashara hiyo.

Pia waliieleza Nipashe kwamba muda wa kuuza kuku unapowadia baada ya wiki tatu hadi nne, wanakuwa wadogo hali inayosababisha wanunuzi kuwakataa.

Mmoja wa wajasiriamali wa kuku wa nyama eneo la Tandale mkoani Dar es Salaam, Alfred Amidu, alisema ni vigumu kukibaini kifaranga kama ni dumavu au la hadi muda wa kuuza unapowadia.

Alisema serikali kupitia wizara husika inapaswa kuingilia kati suala hilo ili kurejesha matumaini kwa wafugaji na kuongeza upatikanaji wa kuku.

"Ndiyo maana kuna uhaba wa kuku hata kama serikali ilizuia vifaranga kutoka nje ya nchi, lakini kuna baadhi ya mbegu ambazo hazikui, mwezi mzima bado yupo rika la kifaranga unalazimika kumuhudumia hivyohivyo kwa sababu ili umpeleke sokoni lazima awe amekomaa na kafikia kuliwa," alisema. "Kwa hiyo serikali tunaomba ilitazame hili kwa macho matatu kwa sababu mbegu hiyo ikisambaa itafikia hatua tutakosa kuku kabisa na wafugaji watashindwa kuendelea na biashara hiyo," aliongeza. Mfugaji mwingine kutoka Goba, Bezaleri Mazengo, alisema wafugaji wa kuku kwa sasa wanapitia wakati mgumu kwa sababu wanapokwenda kununua vifaranga inakuwa siyo rahisi kubaini kama ni mbegu dumavu.

"Sisi wafugaji siyo rahisi kukijua kama hiki kifaranga ni mbegu dumavu au laa, kwa hiyo utakuja kubaini hilo baadaye wakati unahudumia unaona siku zinazidi kwenda hakikui.

"Kwa sasa kupata mbegu nzuri imekuwa kama kamali na ulaji wa kuku siku zote ni uleule kwa hiyo unajikuta unatumia gharama nyingi hata sokoni unalazimika kupandisha bei," alisema.

**SERIKALI YAKIRI**

Ofisa Mifugo wa Mkoa wa Dar es Salaam, Odetha Mchunguzi, alipotafutwa na Nipashe, alikiri kuwapo kwa vifaranga dumavu pamoja na kupokea malalamiko kutoka kwa wafugaji, huku akitaja hatua ambazo zinachukuliwa.

"Ni kweli kuna mbegu dumavu ya vifaranga ambayo hawakui kwa wakati lakini wakati mwingine ni matunzo na chakula cha mfugaji mwenyewe vinaweza kusababisha kuku wasikue kwa wakati," alisema. "Kwa hiyo huwa tukipokea malalamiko tunakwenda kwa mfugaji moja kwa moja kuangalia kama mbegu ilikuwa nzuri tunaangalia matunzo yake yalikuwaje. Kwa hiyo kuna mambo mengi ambayo yanafanya kuku adumae," aliongeza.

Mchunguzi alisema baada ya hapo wanatoa elimu kwa kushirikiana na maofisa mifugo wa wilaya ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Alisema huwa wanafanya uchunguzi kwanza hadi wanapata ukweli wa tatizo kama ni mbegu ya kuku au vyakula anacholisha mfugaji.

"Kwa mfano mfugaji akienda kuchukua vifaranga kutoka kiwanda fulani, tukaona malalamiko mengi kutoka kwa wafugaji tunaenda mpaka kwenye hicho kiwanda kuona shida ni nini? Tukibaini tatizo, tunamfungia mpaka pale atakapojirekebisha," alisema.

Aidha, Mchunguzi alisema kwa wale kuku ambao wamedumaa kulikosababishwa na chakula hulazimika kwenda katika kiwanda kilichozalisha chakula hicho, wanachukua sampuli na kupeleka maabara kwa ajili ya uchunguzi.

Aliwaonya wafanyabiashara wanaouza chakula cha kuku ambacho hakijakidhi vigezo na wale wanaojihusisha na uuzaji wa mbegu dumavu za vifaranga huku akisema kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.



Makamu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Prof. Yohana Mashalla (kushoto), akikabidhi zawadi kwa Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Western Kentucky cha Marekani, Prof. William Mkanta, alipotembelea na ujumbe wake chuoni hapo, Dar es Salaam jana. Kulia ni Prof. John Sunnygard kutoka chuo hicho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Bunge laagiza benki, kampuni simu zibanwe miamala ya tozo

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI machungu ya tozo yakiwa hayajapoa, Bunge limeagiza serikali kuangalia ni namna gani 'itazibana' benki na kampuni za simu za mkononi ili kushusha gharama za tozo za huduma ya miamala yao ambazo ziko juu kuliko tozo inayopata serikali.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku mbili, baada ya serikali kutangaza kupunguza na kufuta baadhi ya tozo za miamala mbalimbali ya kielektroniki, kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza jana Bungeni jijini Dodoma baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali na majibu, Naibu Spika, Mussa Hassan Zungu alisema:

"Jana (juzi) serikali imetangaza kupunguza gharama hizi za miamala lakini wananchi wengi wanalalamikia kodi ya serikali. Hawatizami mapato yanayokatwa na mabenki, hawatizami makato yanayokatwa na kampuni za simu. Lazima hii ifanyiwe marekebisho.

"Benki unatuma pesa, inachukua pesa nyingi zaidi ya serikali, kwa asilimia kubwa sana. Lakini serikali imejenga madarasa na vituo vya afya, lakini ndiyo inayolaumiwa," alisema.

Akionyesha kutokubaliana na makato hayo, Naibu Spika, alisema kwa sasa kuna mtandao wa watu ambao umetengenezwa kuikosoa serikali, wakati pesa wanaochukua ni watu wengine.

"Kwa hiyo kuna ki-sindycate ambacho kinatengenezwa kuipiga dongo serikali, wakati pesa wanachukua watu wengine. Kwa hiyo hili nalo mlitizame ni namna gani mta-regulate (mtarekebisha) mapato ya mabenki ili kupunguza gharama za service charge zao (gharama za huduma) pamoja na gharama za simu.

"Mimi niwaombe wananchi pamoja na sisi Wabunge, unapotuma pesa, tizama break down ya pesa iliyoandikwa (mchanganuo), utaona levy ya serikali (tozo ya huduma) iko chini sana, na mapato wanachukua kampuni za simu na taasisi za fedha. Makato yako juu zaidi ya mapato inayopata serikali," alisema.

Katika hatua nyingine, Bunge limeitaka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kuja na mkakati maalum wa kuhakikisha umiliki wa mfumo wa huduma za mtandao wa intaneti, unabaki nchini na mapato yake yanabaki nchini.

"Umiliki wa mfumo wa huduma za mtandao ibaki nchini na mapato haya yabaki nchini, tusilipe nje ya nchi. Intaneti inaweza ika-decentralize maeneo mengi nchini (ikasambazwa), hata vijana hawa wakawa watoa huduma za intaneti,"alisema Naibu Spika.

Zungu alisisitiza kwamba mtandao wa mawasiliano ya intaneti kwa Tanzania, hauna mchango kwenye pato la taifa linalotokana na intaneti.

"Tanzania hatuna GDP internet (hatuna mchango kwenye pato la taifa unaotokana na intaneti) sovereignity kwenye internet (hatuna uamuzi kwenye intaneti), gateway iko nje ya nchi (umiliki/uamuzi). Kwa maana hiyo, pesa zinakwenda nje ya nchi tunapowasiliana kwa intaneti. "Sisi tunao service providers (watoa huduma) lakini na wao vilevile wanalipwa hizi pesa nje ya nchi. Nikuombe Mheshimiwa Nape (Waziri), wewe ni mtaalam, na wewe ndio mwokozi wa nchi hii. Tunakutegemea wewe ufanye haya mabadiliko nchini mwetu.

"Tupate pesa nyingi kwenye intaneti, sasa hivi mapato mengi ya simu sio kwenye voice call (kupiga) ni kwenye data (matumizi ya vifurushi) na huko ndiko ambako pesa ziko.

"Sasa nikuombe wewe na Wizara yako, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, muweke mkakati maalum wa kuhakikisha gateway ya internet, ibaki nchini na mapato haya yabaki nchini, tusilipe nje ya nchi. Intaneti inaweza ika-decentralize maeneo mengi nchini, hata vijana hawa wakawa service providers," alisisitiza.

**UFAFANUZI 30,000/-**

Wizara ya Fedha na Mipango imesema kuondoa tozo ya miamala kwa njia ya kielektroniki kwa kiwango kisichozidi Sh. 30,000, kumezingatia malipo ya wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kiwango hicho mara nyingi ndicho kinatumiwa kulipa wanufaika wa TASAF Tanzania Bara na Zanzibar Sh. 20,000 na ndio sababu ya kuondoa tozo.

Kamishna Msaidizi wa Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha na Mipango, Wiliam Mhoja, alitoa ufafanuzi huo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ufafanuzi wa tozo za miamala ya kielektroniki.

"Wanufaika wa TASAF sasa hivi wanalipwa kupitia benki au simu za mkononi ndiyo maana tukapunguza. Kwa wafanyakazi hoja zao zimezigatiwa pamoja na watoa huduma wote kwa sababu wapo wafanyabiashara wadogo na wakubwa wanaotumia hizi huduma hivyo tumemzingatia kila mmoja," alisema.

Alisema hatua zilizochukuliwa ni mwendelezo wa usikivu wa serikali katika kufanyia kazi matatizo yanayowakabili wananchi.

Alisisitiza kuwa mbali na hatua hiyo, serikali itahakikisha inaendelea kusikiliza maoni ya wadau, ili kufanyia kazi kero nyingine zinazowakabili wananchi katika tozo.

Mhoja alisema tozo zote zilizokuwa zikilalamikiwa zimeguswa na hatua zimechukuliwa ili kupunguza mzigo kwa wananchi. Alisema, mafanikio hayo si ya serikali pekee bali kwa ushirikiano wa wadau na watoa huduma wa sekta husika katika kuhakikisha jamii inanufaika na mabadiliko hayo.

Mhoja alieleza kuwa baada ya kanuni kutoka viwango vyote vya miamala ambavyo vimeshuka na kufanyiwa marekebisho vitatolewa taarifa ili kupanua wigo wa uelewa kwa jamii.

"Pia tumeona tutolee ufafanuzi ili jamii ielewe kuwa serikali imesamehe tozo ya miamala katika utoaji fedha taslimu kupitia wakala wa benki na Mashine ya kutolea Fedha (ATM) kwa miamala yenye thamani isiyozidi sh. 30,000 na kupunguza gharama ya miamala kwa asilimia 10 hadi asilimia 50 kufuatana na kundi la miamala.

Alisema, tozo hizo ambazo viwango vya tozo vilishushwa kwa asilimia 30 kutoka kiwango cha juu cha Sh. 10,000 hadi kiwango cha juu cha Sh. 7,000, vilianza kutumika Septemba saba mwaka jana. Aliongeza kuwa kutokana na agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kupunguzwa zaidi tozo, Wizara ya Fedha ilipunguza tozo zaidi kwa kushusha tena kiwango cha juu kutoka Sh. 7,000 hadi Sh. 4,000 marekebisho ambayo yataanza kutumika Oktoba Mosi, mwaka huu.

**■Imeandaliwa na Godfyey Mushi, DODOMA na Mary Geofrey, DAR.**

## HABARI KITAIFA

# Tanzania, Msumbiji kupambana na ugaidi

**Na Elizabeth Zaya**



TANZANIA na Msumbiji zimekubaliana kuendelea kushirikiana katika maeneo mbalimbali ikiwamo ulinzi na usalama hususani katika kupambana na tishio la ugaidi katika maeneo ya mpakani.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya makubaliano hayo, marais wa nchi hizo, Samia Suluhu Hassan (pichani) na mwenyeji wake, Filipe Nyusi, walisema uko mpaka mkubwa unaozunganisha nchi hizo, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kushirikiana katika kuimarisha ulinzi.

Maeneo mengine ambayo walikubaliana na marais hao ni Tanzania kufundisha lugha ya Kiswahili nchini Msumbiji, kubadilishana wanafunzi vyuo vikuu, uwekezaji na sekta za gesi na madini.

Akizungumza katika mkutano huo, Rais Samia alisema ziara hiyo itafungua ukurasa mpya baina ya pande hizo katika kuleta ustawi wa ushirikiano wake.

"Tanzania tunashirikiana mpaka ambao ni mrefu sana na kwa msingi huo ni lazima tuwe na ushirikiano mkubwa zaidi kuendelea kuilinda mipaka yetu na hii inatokana na kwamba kumekuwa na uhalifu mipakani na ugaidi, kwa mazingira hayo kuna haja ya kushirikiana katika usalama," alisema Rais Samia.

Samia alisema miongoni mwa maeneo mengine ambayo wanahitaji kuongeza nguvu ya ushirikiano ni katika biashara na uwekezaji, akisema hivi karibuni limeonekana kushuka.

"Hili ni eneo muhimu ambalo tunatakiwa kulifanyia kazi kwa sababu hivi karibuni limeshuka sana, tumekubaliana kuona namna ya kutumia fursa za kibiashara hasa eneo la kilimo na uchimbaji madini," alisema.

Rais wa Msumbiji Nyusi, alisema hakuna mgogoro wowote wa mipaka kati ya nchi hizo, hivyo aliishukuru Tanzania akisema ni miongoni mwa nchi ambazo zimechangia nchi hiyo kufanikisha kupambana na suala la ugaidi.

"Tunaishukuru Tanzania kwa ushirikiano wake iliotoa katika kupambana dhidi ya magaidi, imetusaidia sana hadi magaidi wengi kujisalimisha na maisha kurudi katika hali ya kawaida.

Tukizungumzia mpaka ambao umeendelea kuwa imara na ambao unatuunganisha kupitia Mto Ruvuma, kila nchi inafahamu inapoishia na hatuna mgogoro wa mipaka," alisema Nyusi.

# Mifugo yafa kwa kukosa malisho

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NG'OMBE 320, mbuzi na kondoo 250 wamekufa kati ya mwezi Julai na Septemba 15, mwaka huu mali ya wafugaji wa Kijiji cha Mawala Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro kutokana na ukosefu wa malisho.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kijiji hicho, David Laiser, alisema kwa sasa katika kijiji hicho, wafugaji wanakabiliwa na matatizo ya malisho kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kijiji changu kina wakulima na wafugaji, kwa upande wa wafugaji hali yao sio nzuri kutokana na mifugo zaidi ya 570 kufa kwa kipindi cha Julai mpaka Septemba 15, mwaka huu, wakiwamo ng'ombe 320, mbuzi na kondoo 250, hii ni hali ya hatari sana, tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwatafutia maeneo ya vichaka kwenye hifadhi za taifa kulisha mifugo hiyo ili kuiokoa kwa sasa kila ukitembea unakutana na mizoga ambayo ni hatari kwa afya za binadamu," alisema.

Alisema licha ya kufahamu makatazo ya serikali katika kusimamia matumizi bora ya ardhi, ipo haja ya kuwasaidia wafugaji hao kwa kuzungumza na mashirika yasiyo ya kiserikali yenye maeneo ambayo yanamalisho.

"Kwa hapa karibu yetu kuna kiwanda cha sukari cha TPC, kuna maeneo yenye malisho, ni vizuri serikali ikazungumza nao ili wafugaji hao waweze kulisha mifugo hiyo kwa miezi hii michache wakati wakisubiri mvua za vuli," alisema.

Kwa upande wake, Mhifadhi Mkuu wa Misitu ya Kahe na Rau, Godson Ulomi, alisema msitu huo uliopo karibu na eneo hilo, ulitengwa kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji.

Alisema Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002 inaelekeza ni marufuku kwa mifugo kuingizwa ndani ya hifadhi na ni marufuku kufanya shughuli zozote za kibinadamu ndani ya hifadhi.

"Lakini, tunawashauri wakafuata mpango wa matumizi bora wa ardhi na kupunguza mifugo ikiwa ni pamoja na kufuga kisasa ili kukabiliana na matatizo ya mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kwa sasa," alisema Ulomi.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, alisema wamepokea maombi ya wafugaji hao na watahakikisha wanafanya mazungumzo na wadau mbalimbali kuhakikisha wanawasaidia.

"Kama walivyopendekeza, tutaona namna ya kuzungumza na wenzetu wa TPC kupata eneo lao ambao hawalitumii kwa sasa ili wafugaji kuingiza hiyo mifugo, kwa kweli hali ni mbaya kwa wafugaji wetu, mifugo inakufa kwa wingi na sababu kubwa ni ukosefu wa malisho hasa ukizingatia eneo nila tambarare," alisema.


SOS CHILDREN'S VILLAGES

SOS Children's Villages Tanzania
P.O.Box 13196 Arusha
www.sos-childrensvillages.org
A loving home for every child

## INVITATION FOR TENDER FOR WATER BOREHOLE DRILLING

**22st September 2022**

**Introduction**

SOS Children's Villages Tanzania is a local Non-Government Organization affiliated to SOS Children's Villages International, a worldwide child care and protection organization that provides orphaned and destitute children with a permanent home and educational opportunities. Established 70 years ago, SOS Children's Villages International the umbrella organization currently has Children's Villages and other projects in 135 countries around the world. Globally, it runs the SOS Children's Village Programme which has two main arms, i.e. Family Based Care based at SOS Children's Villages and Family Strengthening Programmes supporting families in local communities. SOS has been working in the United Republic of Tanzania since 1991 and implements its programs in the following locations Zanzibar, Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, and Iringa.

SOS Children's Villages Tanzania invites qualified Contractors to bid for the water Borehole Drilling at Ngaramtoni Urban within Arusha District Council as per the below specifications:

a) Direct mud rotary or percussion method of drilling is recommended right from the start to avoid caving in of the unconsolidated sediments during the drilling operation;

b) The recommended depth and well assembly for the borehole to be drilled are 150metres, and 15.24 cm respectively. The borehole diameter is recommended to be 20.32 cm.
However, the final drilling depth can be altered by the site supervisor depending on the rock strata penetrated, and the quality and quantity of water struck during the drilling operation;

c) A pilot hole should be drilled to the recommended depth and reaming to be done after the of the water;

d) Drilling of the borehole, design, and installation of well assembly, pumping test should be carried out under the supervision of a Hydrogeologist/Senior Technician;

e) Large, well-rounded quartz pea-size gravels (2 — 4mm diameter) should be used in packing the borehole.

f) Water from different strikes/aquifers should be chemically analyzed for quality at the Water Quality Laboratory

g) A concrete slab should be built around the top of the good assembly for sanitary Protection. The top five (0 — 10) meters should be cement grouted to avoid Pollution. After construction, the borehole should be fully developed by compressed air until the water becomes absolutely silt free before a production testing of at least 4 hours.

h) An interest Constructor should possess a valid class 1 Operation License

**Table No. 1: Detailed Specifications of the required Drilling**

| SIN | AB/2(M) | NN/2(m) | K | R^ | KxR (Am) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1.5 | 0.5 | 6.28 | 30.0 | 188.4 |
| 2 | 2.0 | ‘’ | 11.78 | 15.0 | 176,7 |
| 3 | 2.5 | | 18.84 | 8.0 | 150.72 |
| 4 | 3.0 | ‘’ | 27.48 | 2.5 | 68.7 |
| 5 | 4.0 | ‘’ | 49.46 | 1.05 | 51.93 |
| 6 | 5.0 | ‘’ | 77.77 | 0.5 | 38.88 |
| 7 | 6.0 | ‘’ | 112.26 | 0.3 | 33.67 |
| 8 | 8.0 | ‘’ | 200.18 | 0.15 | 30.02 |
| 9 | 10.0 | ‘’ | 313.22 | 0.089 | 27.87 |
| 10 | 10.0 | 2.5 | 58,88 | 0.27 | 15.89 |
| 11 | 12.0 | ‘’ | 86.51 | 0.20 | 17.30 |
| 12 | 15.0 | ‘’ | 137.38 | 0.11 | 15.11 |
| 13 | 20.0 | ‘’ | 247.28 | 0,075 | 18.54 |
| | 25.0 | ‘’’ | 388.58 | 0.059 | 22.92 |
| 15 | 25.0 | 5.0 | 1884 | 0.43 | 81.01 |
| 16 | 30.0 | ‘‘‘ | 274.75 | 0.63 | 170,9 |
| 17 | 40.0 | ‘’ | 494.55 | 0,369 | 182.48 |
| 18 | 50.0 | ‘’ | 777.15 | 0.25 | 194.28 |
| 19 | 50.0 | 10.0 | 376.8 | 0.495 | 186.51 |
| 20 | 60.0 | ‘’ | 549.5 | 0.34 | 186.83 |
| 21 | 75.0 | ‘’ | 867.43 | 0.25 | 216.85 |
| 22 | 100.0 | ‘’ | 1554.3 | 0.15 | 233,14 |
| 23 | 100.0 | 25.0 | 388.75 | | |
| 24 | 125.0 | ‘’ | 942 | 0.375 | 353.25 |
| 25 | 150.0 | ‘’ | 1373.75 | | |
| 26 | 180.0 | ‘’ | | | |

***Note:*** *Interested Contractors Should apply for Drilling Permits from Pangani Water Basin Office-Moshi in accordance with Water Resources Management Act No. 11 of 2009.*

**Requirements:**

- A duly completed and signed price offer in Tanzania shillings VAT inclusive;
- Bidder should submit a **certified** copy of the valid Business license, Contractor's Registration Certificate, Certificate of Incorporation, VAT/TIN registration, Water Drilling Permit, and current Tax Clearance Certificate;
- Bidder must submit/indicate experience in carrying out similar Works;
- Bidder must indicate Defect Liability Period of the Borehole;
- Bidder should indicate completion time upon submission of their priced bids; and
- Bidder should state his terms of payment.

**Opening of Bids**

At the indicated time and place, the opening of Bids shall be carried out by SOS Children's Villages Tanzania, Arusha. It reserves the right to conduct the opening of Bids in Public or not.

**Submission of Bids:**

Bids must be submitted in a sealed envelope physically to SOS Children's Village of P.O.Box 13196 Arusha

***Bids shall be submitted by hand delivery to the above address on or before Wed, 5th October 2022at 14:00 EAT***

***Late Bids, bids not received and opened shall not be accepted irrespective of circumstances.***

***Note: No tender document will be issued, all enquiries should be addressed to National.Office@sos-tanzania.org***

217057202

# Wahukumiwa kunyongwa mauaji ya ofisa wa JWTZ

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Morogoro, imewahukumu watu watatu kati ya tisa waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya mauaji ya ofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Leonard Yamakwa.

Msajili wa Mahakama ya Rufani, Selvester Kahinda, akisoma hukumu hiyo juzi, alisema mahakama imejiridhisha pasipo na shaka kuwa watu hao, Charles Expedito, Hassan Athuman na Alfred Dotto, walimuua marehemu kwa makusudi, hivyo adhabu yao ni kunyongwa hadi kufa.

Alisema mahakama imejiridhisha kuwa watu hao walitenda kosa la mauaji kwa makusudi kinyume cha kifungu namba 196 na 197 kwa Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 ya marejeo ya mwaka 2002, hivyo adhabu yao ni kufa kwa kunyongwa.

Kahinda alisema katika kesi hiyo Na. 6 ya mwaka 2020, kosa hilo likifanyika Mei 25, 2019 majira ya saa 12:00 jioni eneo la mashamba ya mkonge Tungi, Manispaa ya Morogoro. Alisema kesi hiyo inawahusisha washtakiwa tisa na kati yao sita wameachiwa huru kwa sababu upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha kama kulikuwa na nia ya pamoja kutenda kosa la mauaji. Walioachiwa huru kwa kukosekana kwa uthibitisho wa uhusika ni Juma Saidi, Yusuph Saidi, Mbaya Edward, Mnambo Michael, Rehema Kibwana na Daudi Chilogo.

Alisema washtakiwa baada ya kuumua mwanajeshi huyo, walimbaka mpenzi wake akiwa juu ya mwili wa marehemu na kisha kutokoweka na pikipiki na simu ya ofisa huyo wa jeshi.

Kesi hiyo iliyokuwa ikiendeshwa na mawakili wawili wa serikali na sita wa upande wa utetezi, Wakili wa Serikali Happiness Makungu, aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa washtakiwa na mahakama ikakubaliana na hoja hiyo kwa kutoa hukumu ya waliotiwa hatiani kunyongwa hadi kufa. Kwa upande wa utetezi, Wakili Aziz Mahenge, alidai kuwa hawakubaliani na hukumu hiyo, hivyo watakata rufani.

# Leo ni leo uchaguzi wabunge Afrika Mashariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE leo linafanya uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) huku wagombea 20 wakiingia katika kinyang'anyiro cha kupata wawakilishi tisa kutoka Tanzania.

Katika uchaguzi huo, Tanzania inapaswa kutoa wajumbe tisa ambapo kulingana na uwiano wa idadi ya wabunge, Chama cha Mapinduzi (CCM) kina nafasi nane huku upinzani (walio wachache bungeni) nafasi moja.

Upinzani mkali utakuwa kwenye kundi la wagombea wa vyama vya walio wachache bungeni ambapo wagombea wake ni Ado Shaibu (ACT-Wazalendo), Jafari Mneke na Mashaka Ngole kutoka Chama cha Wananchi (CUF).

Akizungumza juzi na waandishi wa habari, Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alisema alipokea majina ya wagombea 21 kutoka vyama vyenye uwakilishi bungeni ambavyo ni ACT-Wazalendo mgombea mmoja, CCM wagombea wanane na CUF wagombea 12.

Hata hivyo, alisema mgombea mmoja kutoka CUF, Zainab Mndolwa, alijiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

"Baada ya kupitia masharti ya uchaguzi, nimejiridhisha wagombea wote wametimiza masharti ya kugombea nafasi hizo. Ilipofika saa 10:15 jioni nilipokea barua kwa mgombea mmoja wa CUF akiomba kujiondoa kugombea nafasi hizo," alisema.

Aliwataja waliopitishwa kuwania nafasi hizo kuwa ni Angella Kizigha, Nadra Juma Mohamed, Shogo Mlozi, Sonia Magogo, Queen Lugembe, Zainab Ham Abdul.

Wengine ni Dk. Abdulla Hasnuu Makame, Machano Ali Machano, Anderson Ndambo, Husna Mohamed Abdalla, Mohamed Habib Mnyaa, Ado Shaibu, Jafar Mneke na Mashaka Ngole.

Katibu huyo pia aliwataja wagombea wengine ni Ansar Kachwamba, James Millya, Dk. Ng'waru Maghembe, Adui Kondo, Mohamed Ngulangwa, Thomas Malima.

Alisema Bunge lina wabunge 392 ambapo CCM ina wabunge 365, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wabunge 20, ACT-Wazalendo wabunge wanne huku CUF wabunge watatu.




Mhazini wa Benki ya NMB, Aziz Chacha (kushoto), akipokea tuzo ya Hati Fungani Bora ya Mwaka 2022 kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jukwaa la Ufadhili wa Ujasiriamali, Mathew Gamser, katika hafla iliyoandaliwa na IFC jijini Phnom Penh, Cambodia juzi. Benki ya NMB kupitia hatifungani yake ya NMB Jasiri imeshinda tuzo ya Platinum upande wa Kundi la Dhamana Endelevu ya Mwaka Kwenye Tuzo za Ufadhili wa Ujasiriamali za Mwaka 2022. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# USAID, Vodafone Foundation kutoa bil. 34/- kusaidia usafiri wa dharura kwa wajawazito

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Kimarekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Vodafone Foundation na Serikali ya Tanzania wameahidi kupanua mfumo wa usafiri wa dharura kwa maelfu ya wajawazito utakaosaidia kuwafikisha haraka katika hospitali na vituo vya afya.

Hayo yalielezwa jana katika Mkutano wa "Demokrasia Huleta Matokeo Chanya" kujibu ombi la Rais Samia Suluhu Hassan la kupanuliwa kwa programu hiyo ili iweze kutekelezwa nchi nzima.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani jana ilisema, USAID na Vodafone Foundation zimeahidi kutoa Dola za Kimarekani milioni 15, kati ya hizo, Dola milioni 10 zikitolewa na Vodafone Foundation na Dola milioni tano zikitolewa na USAID.

Serikali ya Tanzania, ambayo katika hafla hiyo iliwakilishwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, imeahidi kugharimia gharama zote za usafiri na kutoa wahudumu wote wa afya watakaohitajika toka siku ya kwanza ya utekelezaji wa programu hiyo. Jitihada hizo mpya zitapanua wigo wa programu hiyo kutoka wilaya mbili, zenye wakazi milioni moja hadi Tanzania nzima yenye wakazi wanaokadiriwa kuwa milioni 60.

Vodafone Foundation imeahidi kutoa kiasi kingine cha Dola za Kimarekani milioni tano ili kuanzisha utaratibu huo katika nchi nyingine za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zenye kiwango kikubwa cha vifo vya wajawazito na kufanya jumla ya kiasi kitakachotoa kufikia Dola za Kimarekani milioni 15. USAID itaangalia uwezekano wa kuwa na programu nyingine za ubia na Vodafone Foundation ili kupeleka mafanikio yaliyopatikana Tanzania mahali pengine.

"Viwango vya vifo vya wanawake kutokana na matatizo ya uzazi bado ni vikubwa Tanzania. Katika jamii za vijijini, gari la kubebea wagonjwa linaweza kupatikana mara moja katika matukio 10 ya dharura yanayohitaji akinamama wajawazito kusafirishwa haraka," ilisema taarifa hiyo.

Kama sehemu ya programu ya mwaka 2013-2020 ya kusaidia afya ya wajawazito katika wilaya za Sengerema/Buchosa na Shinyanga, Vodafone Foundation na USAID walianzisha utaratibu wa wajawazito kuchangia usafiri wa bure. Chini ya programu hiyo, wanawake walio katika dharura itokanayo na hali yao ya ujauzito walipiga simu ya bure kuzungumza na mhudumu wa afya ambaye huchukua taarifa zao kisha mfumo wa kielektroniki hubaini hospitali iliyokaribu na dereva wa teksi aliye karibu na mama huyo.

Dereva hulipwa malipo yake baada ya kumfikisha mgonjwa hospitalini au katika kituo cha afya. Hivi sasa halmashauri katika wilaya hizi za majaribio zinagharimia zenyewe programu hizi ambazo gharama zake ni za chini kuliko bei ya kununulia gari moja la wagonjwa na hadi hivi sasa, programu hizi zimewasafirisha akinamama na watoto wachanga zaidi ya 15,000.

Ahadi ya Vodafone Foundation ilitangazwa na Afisa wa Biashara na Masuala ya Nje wa Vodafone na mjumbe wa Baraza la Wadhamini la Vodafone Foundation, Joakim Reiter, katika hafla iliyoongozwa na Ofisa Mkuu wa USAID Samantha Power - ambaye pia ndiye aliyetangaza ahadi ya USAID - akieleza jinsi biashara na taasisi za ufadhili zinaweza kushirikiana na nchi zenye demokrasia inayokua.

TOLEO MAALUM

# TANESCO yapiga hatua kubwa, Kigoma, Kagera kwa mara ya kwanza sasa kwenye Grid ya Taifa

**Na Valentine Oforo, Dodoma**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limefanikiwa kuziunganisha kwenye umeme wa mfumo wa Gridi ya Taifa wilaya nne za mikoa ya Kigoma na Kagera, hatua yamafanikio makubwa ambayo ni miongoni mwa juhudi zinazoendelea kutekelezwa na TANESCO ili kuboresha upatikanaji na usambazaji wa umeme wa uhakika katika maeneo yote hapa nchini.

Pamoja na mipango mingine, TANESCO kwa sasa inatekeleza mpango mkakati wa nchi nzima unaolenga kuhakikisha wilaya zote nchini zinapata umeme wa uhakika kwa kuunganishwa kwenye mfumo wa Gridi ya Taifa, mkakati ambayo umeanza kuzaa matokeo mazuri.

Septemba 17, 2022, TANESCO ilifanikiwa kuzima mitambo yake minne iliyokuwa ikitumia mafuta ya dizeli kwa ajili ya kuzalisha umeme na kuwasha umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa, ikiwa ni kwa mara ya kwanza tokea kupata uhuru mwaka 1961, ambapo wateja 10,000 tayari wameshaunganishwa kwenye mfumo wa umeme wa Gridi ya umeme ya Taifa.

Wilaya hizo zimeunganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa kutokea kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Nyakanazi ambapo awali zilikuwa zinatumia umeme wa kuzalishwa kwa jenereta (Disel) uliokuwa ukiigharimu Serikali takribani Shilingi bilioni 22.4 kwa mwaka ambazo TANESCO itaziokoa kwa kuzima jenereta Wilaya za Kibondo, Ngara na Biharamulo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alieleza kwamba serikali kupitia Wizara ya Nishati imetekeleza kwa vitendo kipaumbele chake cha kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Kigoma na Kagera.

Aidha ailongeza kuwa, kwa upande wa Wilaya ya Kibondo TANESCO inaokoa shilingi milioni 734 kwa mwaka ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya kulipia gharama za matengenezo ya mashine, na shilingi bilioni 8.7 kwa mwaka zikiwa ni gharama za kununua mafuta ya Disel.

"Akiwasilisha Bungeni hotuba ya Wizara ya Nishati mnamo tarehe 2 Juni 2022, Waziri wa nishati January Makamba alikitaja kipaumbele cha kwanza kuwa ni, "Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project"), ahadi ambayo sasa imetekelezwa kikamilifu.

Pamoja na hayo, akieleza zaidi juu ya utekelezaji mahiri wa wizara ya nishati, ikiwa ni pamoja na TANESCO, katika kuongeza wigo za upatikanaji wa nishati ya umeme kote nchini, Maharage aliongeza: "Na mnamo mwezi Julai 2022, akiwa kwenye ziara yake ya kikazi pale Nyakanazi, waziri Makamba aliwaahidi wananchi wa Nyakanazi kuwa ifikapo mwezi Oktoba 2022 watakuwa wanapata umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa. Ahadi hii imetimia kabla hata ya mwezi wa Oktoba 2022 kufika,"

Msemaji wa Shirika hilo, Martin Mwambene, akieleza juu ya mafanikio zaidi yaliyofikiwa na TANESCO hadi sasa, alisema TANESCO imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi, pamoja na kuzindua kituo cha kupokea na kupoza umeme chenye Kilovoti 220/33 cha Nyakanazi.

"Pamoja na hatua hii nzuri, pia TANESCO imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 33 kutoka Nyakanazi hadi Kakonko kwa lengo la kuunganisha Kakonko, Kibondo na Kasulu kwenye Gridi ya Taifa," alieleza.



Kituo Cha kupokea na kupoza umeme wa msongo 33/11 Cha kibondo

Aidha, aliongeza kuwa, TANESCO imekamilisha ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa msongo wa Kilovoti 33 na Kilovoti 400 katika mkoa wa Geita na Kigoma, na kusema juhudi zinaendelea za kukamilisha ujenzi wa njia ya kufikisha umeme wa msongo wa Kilovoti 33 wilayani Kasulu hadi Kigoma mjini kufikia mwanzoni mwa mwaka 2023.

Akieleza juu ya faida za maeneo hayo kuunganishwa kwenye mfumo wa Grid ya Taifa, alisema kukamilika kwa ujenzi wa njia hizo za kupeleka umeme wa msongo wa Kilovoti 33 wa Gridi ya Taifa kumewezesha kuimarisha huduma ya upatikanaji umeme kwenye maeneo yalikuwa yanategemea umeme wa kuzalishwa kwa mashine nne zilizokuwa zikitumia mafuta ya dizeli.

"Kwa sasa, tunaamini kwamba wananchi wanaoishi katika maeneo ya Nyakanazi na Biharamulo mkoani Kagera pamoja na Kakonko, Kibondo na Ngara mkoani Kigoma wamepata fursa kubwa ya kujikita ipasavyo katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kutokana na kuanza kupata huduma ya umeme wenye nguvu kubwa na wa uhakika," alieleza.

Alifafanua, kwa kukamilika kwa mradi huu, kwa eneo la Kibondo pele yake, TANESCO inaokoa jumla ya Sh. 734 milioni kwa mwaka ambazo ni gharama za matengenezo ya mashine pamoja na Tsh. 8.7 bilioni kwa mwaka zikiwa ni gharama za kununua mafuta ya dizeli.

"Na kwa eneo la Kasulu, TANESCO inaokoa Sh 1.1 bilioni kwa mwaka ambazo ni gharama za matengenezo ya mashine kwa mwaka pamoja na Sh.11.85 bilioni kwa mwaka zikiwa ni gharama za kununua mafuta ya dizeli," aliongeza.

Hatua ya kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo ni jitihada za kuhakikisha wilaya zote nchini zinaunganishwa na mfumo wa gridi ya Taifa ili ziwe na umeme wa uhakika, unaotabirika na utakao wasaidia wananchi katika shughuli zao za kiuchumi na kimaendeleo.

Mahitaji ya umeme Wilaya ya Kibondo ni megawati 2.7, huku mashine za kuzalisha umeme zilikuwa na uwezo wa megawati 2.5, hivyo uunganishwaj wa umeme wa gridi ya Taifa Kibondo unatarajia kusaidia wananchi wengi kufikiwa na umeme.

Takwimu zinaonyesha kwamba mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanatarajiwa kupanda kutoka Gigawatt (GWh) 10,176 hadi 28,663 ifikapo mwaka 2030, ikiwa ni asilimia 13.82 ya kiwango cha ukuaji wa kila mwaka (CAGR), TANESCO kwa upande wake tayari imeanza kuchukua hatua mbalimbali za kukidhi mahitaji ya umeme yanayotarajiwa kuongezeka, ikiwa ni pamoja ya mkakati unaoendelea unaolenga kuongeza uzalishaji wa megawati 9000 za umeme ifikapo mwaka 2030.

Hata hivyo, mahitaji ya umeme nchini Tanzania yanakadiriwa kukua kwa wastani wa kati ya asilimia 10 na 15 kwa mwaka, na kwa kuzingatia kwamba kwa sasa ni asilimia 24 tu ya watanzania ndiyo wanaopata umeme, TANECO imejipanga vyema kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme nchini, kutoka megawati 1,695 zinazozalishwa kwa sasa hadi kufikia megawati 5,000 ifikapo 2025.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande miradi mingine itakayotekelezwa kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na mradi wa kuboresha mfumo wa usambazaji umeme katika Jiji la Dodoma, mradi wa njia ya kusafirisha umeme Msongo wa KV 132 kutoka Tabora hadi Urambo na kutoka Urambo Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma.

"Miradi mingine inayoendelea ambayo katika siku za usoni inatarajiwa kutoa mchango mkubwa katika kuongeza upatikanaji wa umeme ni pamoja na mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga, pamoja na Mbeya-Tunduma" aliongeza.

TANESCO ni shirika linalohusika na ugawaji wa umeme nchini Tanzania. Shirika hili lilianzishwa mwaka 1964. Shirika la TANESCO linamilikiwa na serikali ya Tanzania. Wizara inayosimamia shughuli za TANESCO ni Wizara ya Nishati.



kituo Cha kupokea na kupoza umeme wa msongo wa kilovoti 220/33 Cha Nyakanazi

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upigaji fedha za miradi ya maendeleo ukomeshwe

**KATIKA** siku za hivi karibuni wakati viongozi mbalimbali wa kiserikali wakitembelea miradi ya maendeleo ya ujenzi, kumeibuka madai ya fedha kutumika ndivyo sivyo au kutoendana na gharama halisi za miradi yenyewe.

Viongozi hao wakiwamo wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na wa ngazi za juu, wanapotembelea miradi hiyo hubaini kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi hiyo.

Hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alishangazwa na ujenzi wa kibanda cha mlinzi kutumia gharama kubwa kuliko uhalisia.

Huo ni mfano mmoja kati ya mingi inayojitokeza wakati viongozi wanapotembelea miradi hiyo.

Waziri Joyce Ndalichako, hivi karibuni naye alibaini ujenzi wa chuo kimoja kutumia gharama kubwa kuliko mradi wenyewe na kukosa majibu ya uhakika.

Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru pia anapotembelea miradi ya maendeleo, wakati mwingine hugoma kuizindua kutokana na kutoridhishwa na utekelezaji wake.

Hali hiyo huiibua Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini kuchunguza ubadhirifu wa mabilioni yanayotolewa na serikali kutekeleza miradi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Fedha nyingi zinazolalamikiwa kutumika vibaya ni pamoja na za UVIKO-19 ambazo zinatolewa na serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali.

Ukichunguza fedha hizo zinavyotumika ni kinyume na masharti yaliyotolewa na wafadhili na serikali katika utekelezaji wake.

Kwa mfano imeelezwa kuwa TAKUKURU imeanza uchunguzi wa mradi wa ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu Sabasaba kilichopo mjini Singida.

Uchunguzi huo unatokana na agizo alilolitoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, kwa TAKUKURU baada ya kutembelea chuo hicho na kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha uliofanywa na watendaji wa serikali.

TAKUKURU, ilipata taarifa za ubadhirifu katika chuo hicho na uchunguzi umeshaanza kufanyika.

Taarifa hizi za upigaji wa fedha za miradi hazipendezi kwa sababu zinarudisha nyuma juhudi za serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi wake.

Vile vile, ni aibu hata kwa wafadhili wanaotoa fedha hizo wakisikia kuwa zinatumika ndivyo sivyo.

Na watu wachache wenye tamaa na ubinafsi wasiharibu sifa ya nchi, hivyo hakuna budi watu hao wakashughulikiwa na kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia hiyo.

Ubadhirifu huo ni katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambavyo huongezwa bei kubwa kuliko uhalisia, kuweka makadirio makubwa ya mahitaji ya vifaa vya ujenzi (BOQ) na kutopelekwa kwa baadhi ya vifaa sehemu husika.

Kwa mfano matofali yakitakiwa 7000, watendaji wanaandika 14,700 na pesa inatolewa na kupigwa.


Bei ya saruji inawekwa kubwa Sh.18,000 bila kodi ya VAT na mifuko inayohitajika 2,912 wakati inayotakiwa kwa ajili ya kazi hiyo ni mifuko 900 pekee kwa mujibu wa mkandarasi, lakini pesa ikatolewa ya mifuko 2,912.

Upigaji mkubwa huwekwa kwenye vifaa vya ujenzi kwa kuongeza idadi kubwa kuliko mahitaji na bei pia ya kununulia huongezwa ili hao watu wachache waweze kujinufaisha.

Hizo ni sehemu tu ambazo watu hutumia mwanya wa kujinufaisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi.

Ziara hizi za viongozi ziendelee kuibua wabadhirifu hawa ili tabia hii iweze kukomeshwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi tuwe mabalozi wazuri kutokomeza uhalifu nchini

Na Pilly Kigome

**IFIKIE** hatua wazazi wawe jeshi kubwa linalosaidiana na polisi nchini kukabiliana na tatizo la uhalifu unaofanywa na watoto wetu. Tuwe katika nafasi ya kuweza kukabiliana na hata kuondoa tatizo la uhalifu ilikosimamia.

Wazazi inatupasa tuchukue hatua stahiki kuanzia ngazi ya familia, ili kuweza kutokomeza kabisa tatizo la uhalifu nchini, unaofanywa na watoto chini ya miaka 18 kwa kila namna na hata zaidi ya hapo, bado ni tegemezi kwa wazazi wao.

Makundi hayo yanavamia nyumba za watu usiku na kupora vitu mbalimbali kwenye nyumba hizo, kisha wanaondoka navyo, ikiambatana na vitendo vya kuua raia wanaoonekana kuonyesha ukaidi kwao.

Hivyo nasema, ni wakati wetu wazazi kuongeza nguvu katika upande wa malezi kuhoji na kudadisi kujua ama kazi au shughuli wanazojishuhulisha nazo watoto wetu, ili kwa pamoja twaondoe tatizo hilo nchini, kwani kufanya hivyo kutarahisisha ama kujua au kugundua kiurahisi shughuli kama kazi anayofanya mwanao.

Inasemekana katika kuaminika, kuna baadhi ya wazazi wanapokea zawadi za thamani kutoka kwa watoto hao zikiwemo televisheni za kisasa na mzazi anapokea pasipo kuhoji, wakati akijua mtoto huyo hana kazi wala biashara na mbaya zaidi, wengine wanatakiwa kuwepo shule.

Sasa inakuwa wazi zaidi, yameibuka makundi ya uhalifu yanayojihusisha na wizi, yakiwemo maarufu wa jina 'panya road' yanayoendelea kutishia maisha ya usalama wa raia na mali zao, hali inayozua hofu kubwa kwa wakazi na hasa mkoani Dar es Salaam.

Ni makundi yanayojihusisha na kunyang'anya, kujeruhi, kupora, kuiba na hata kuua, jambo linaloleta taharuki hata kuwafanya watu kupunguza saa za kufanya kazi na shughuli nyinginezo za kujiongezea kipato cha kila siku, wakijihami dhidi ya taharuki hiyo.

Tukiwa wazazi muda sahihi umefika tuwe mabalozi namba moja wa kutokomeza tatizo hilo nchini kote. Naamini, tukishirikiana pamoja tunaweza.

Inaaminika awali na hata sasa, kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wakipokea zawadi kutoka kwa watoto wao na kupokea zawadi hizo bila kuhoji ama kudadisi imetokea wapi hali ya kuwa mtoto hana kazi au biashara yoyote.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ametoa wito kwa wazazi kuweza kufuatilia mienendo ya watoto wao na shughuli zao wanazozifanya za kila siku za kujiingizia kipato, ili kubaini na kujiridhisha kazi wanazofanya.

Makala anawataka wazazi kushirikiana waweze kuisaidia polisi kukabili tatizo kabla halijafika pabaya zaidi na kuna baadhi yetu wazazi tunaelewa mienendo ya watoto wetu.

Makala anasema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam, imejipanga na kujiwekea mikakati madhubuti na tayari wameshawakamata watuhumiwa wa uhalifu 135, vijana sita wametangulia mbele ya haki katika mchuano na polisi.

Mkuu wa Mkoa, anasema vijana hao wote kwa pamoja, ni wale wanaojihusisha na uhalifu kama wizi, unyang'anyi wa mali mfano; televisheni, redio, simu na hata pesa kutoka kwa raia wema na wanaenda kuviuza.

Mbali na hilo, anafafanua kwamba tayari wameshaweza kuwatia mbaroni wanunuzi watano wakubwa wanaonunua bidhaa za wizi, kutoka kwa wahalifu hao maarufu kama 'panya road.'

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, anatoa wito kwa wananchi kuweza kushirikiana pamoja kutoa taarifa kwa jeshi hilo na kuwatoa hofu kwamba, kutakuwa na usiri mkubwa kwa atakayetoa taarifa hizo.

"Jeshi la polisi halijawahi kushindwa na halitegemei kushindwa, wahalifu wakae chonjo na wale wote wanaojaribu kuchezea wasimamizi wa sheria," anasema Muliro.

Tayari tunaambiwa, jeshi la polisi limeshachukua hatua kwa mujibu wa mamlaka na wajibu wake, sita kati ya tisa wanaosadikiwa kuwa 'panya road' wamekufa, katika mapambano na polisi waliokuwa wanawakabili.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea mfano wa njiwa mweupe kama ishara ya kuhamasisha amani duniani, katika maadhimisho ya Siku ya Amani Duniani, yaliyofanyika kitaifa mjini Moshi, Kilimanjaro jana. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu na (kushoto kwake) ni Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Zlatan Milisic. **PICHA: OWM**

# PM: Amani italindwa kwa nguvu zote

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali itaendelea kulinda amani nchini kama silaha muhimu ya kujenga uchumi na maendeleo endelevu kwa mustakabali wa taifa.

Majaliwa alisema hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Amani Duniani kwa mwaka 2022 yenye kaulimbiu 'Amani Yetu, Maendeleo Yetu' yaliyofanyika kitaifa mjini Moshi.

Alisema athari za kukosekana amani ni vita vinavyoendelea nchini Ukraine na wanaoathirika zaidi ni wanawake, watoto na wazee jambo ambalo dunia inapaswa kulitazama upya.

Waziri Mkuu aliihakikishia jumuiya ya kimataifa kuwa Tanzania itaendelea kuunga mkono juhudi za kikanda na kimataifa kuhakikisha amani inaendelea kuwapo na kwamba serikali itaendelea kuifanya Tanzania kuwa nchi salama na kimbilio kwa mataifa mengine yanapopoteza amani.

Kuhusu kudumu kwa amani iliyopo nchini, Waziri Mkuu alisema kazi kubwa imefanywa na viongozi wa dini ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa serikali.

"Serikali itaendelea kuwathamini, kuwaheshimu na kuwajali viongozi wa dini. Hili tumelitunza, tangu awamu ya kwanza hadi sasa, tutaendelea kuchukua kauli zao katika kulisaidia taifa," alisema.

Aliwataka Watanzania kuendelea kulinda tunu ya amani na utulivu ambayo imepatikana kutokana na misingi imara ya viongozi wa dini. Pia aliwataka wananchi kuhakikisha wanaisimamia amani na utulivu uliopo akisisitiza kuwa kukosekana kwake ndani ya familia ni kiashiria kimojawapo kukosekana ndani ta taifa.

Majaliwa alisema pamoja na Amani iliyopo, yako baadhi ya mambo kama ugonjwa wa UVIKO- 19 ambao ulitikisa amani iliyopo na kila taifa lilijiwekea utaratibu wa kukabiliana nayo.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka Watanzania kwenda kupata chanjo kwa afya zao kwa kuwa kinyume cha hapo watakosa fursa za kibiashara na mataifa mengine duniani.

Alisema jambo lingine ni mabadiliko ya tabia nchi na kuathiri shughuli za maendeleo kutokana na ukame na mafuriko hivyo kussababisha kukosa amani kwa sabau ya ukosefu wa chakula.

Mapema, Mratibu Mkazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa mataifa (UNDP), Zlatan Milisic ambaye pia ni mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, alipongeza serikali kwa kulinda amani iliyoko nchini.

Alisema Tanzania ni moja ya nchi za kupigiwa mfano kutokana na kuongoza kwa amani miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Milisic alitaka Watanzania wasione kama suala la amani ni jambo kawaida sana bali ni tunda linalotokana na kulindwa kwa misingi imara ikiwamo haki, upendo na utawala wa sheria.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema mkoa huo una amani ya kutosha licha ya kuwa na matatizo machache ikiwamo biashara ya mirungi ambayo zao halali nchini Kenya.

Alisema pia mkoa unaendelea kukabili wimbi la wahamiaji haramu kutoka baadhi ya mataifa kwa kisingizio cha kupitia kwenda nchini Afrika kusini kutafuta maisha Bora zaidi.

## KABWELA




## Kairuki, Kentucky kushirikiana utafiti kitaaluma

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), kimeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Kentucky (WKU) cha Marekani kwa ajili ya kuendeleza ushirikiano katika taaluma.

Makamu Mkuu wa HKMU, Prof. Yohana Mashalla, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati ujumbe wa chuo hicho ulipotembelea HKMU, kwenye ofisi zake Mikocheni, Dar es Salaam.

Alisema kwenye ushirikiano huo, watajikita kwenye utafiti mbalimbali wa masuala ya afya na kuandika mapendekezo ya kuomba fedha kuwezesha kufanya utafiti unaohitajika nchini.

Prof. Mashalla alisema ushirikiano huo utaijengea uwezo mkubwa HKMu wa kuandia maandiko ambayo yanaweza kuwavutia wadau mbalimbali duniani kutoa fedha za kusaidia utafiti kwenye masuala mbalimbali.

Alisema katika ushirikiano huo, watachapisha matokeo ya utafiti mbalimbali ambayo yatasaidia kueleza ambacho HKMU inafanya kwenye utafiti, hivyo kusaidia chuo kuonekana duniani kwamba kinaweza kufanya utafiti.

"Sisi HKMU tuna malengo matatu ambayo ni kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri kwenye taasisi za serikali na mashirika ya nje kwa kutoa mawazo na uzoefu wetu kwenye nyanja mbalimbali, hivyo ushirikiano huu utatujengea uwezo kutoa ushauri mzuri kwa serikali na wadau wengine," alisema.

Alisema kwenye mazungumzo yao wamebadilishana uzoefu wa namna ya kufundisha na teknolojia za aina mbalimbali zinazotumika kufundisha wanafunzi wa udaktari, uuguzi na fani zinginezo.

Prof. Mashalla alisema mmoja wa wafanyakazi wa WKU ni Mtanzania ambaye alisoma Tanzania na kumalizia masomo yake nchini Marekani na ndiye aliyekuwa nguzo ya kuanza kwa ushirikiano na HKMU.

"Uhusiano huu unamanufaa kwetu na kwao kwasababu kwa dunia ya sasa ni ngumu sana taasisi kuishi kama iko kwenye kisiwa hivyo lazima taasisi zishirikiane. Hapa tunasikilizana wao wana kozi gani nasisi tunakozi gani tushirikiane kuanzisha programu ambazo wao wanazo sisi hatuna," alisema.

Alisema kupitia ushirikiano huo watakuwa na utaratibu wa kubadilishana wanafunzi na wahadhiri wa chuo hicho kwa wao kuja kufundisha kwa muda kwenye fani ambazo hazina wataalamu wengi nchini.

Profesa William Mkanta, ambaye ni Mtanzania anayefanya kazi kwenye chuo hicho cha WKU, alisema aliamua kuwaunganisha ili waweze kushirikiana kwenye tafiti zenye manufaa kwa jamii.

"Mimi ni mzaliwa wa Tanzania ila nafanyakazi Marekani kama Profesa nimeona umuhimu wa vyuo vikuu kusaidia jamii kwasababu vyuo vikuu ndiyo kitovu cha utafiti, huduma na kitovu cha kujifunza.

"Ndiyo maana tumeona tuwe na uhusiano wa vyuo hivi ili tuweze kuhamisha vipaji vilivyopo kwenye vyuo hivi. Dunia ni kama kijiji siyo lazima watu majirani ndiyo mshirikiane bali hata walio mbali wanaweza kushirikiana ndiyo maana tumeona umbali uliopo baina ya HKMU na WKU si kikwazo cha ushirikiano," alisema.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

**CHUO CHA KODI**

**MAHAFALI YA 15 NA KONGAMANO LA WAHITIMU**

Mkuu wa Chuo cha Kodi (ITA) anapenda kuwajulisha wahitimu wote wa mwaka wa masomo 2021/2022 na umma kwa ujumla kwamba, **Mahafali ya 15 ya Chuo cha Kodi** yatafanyika katika Ukumbi wa Chuo, Multipurpose siku ya **Ijumaa tarehe 25 Novemba 2022** kuanzia saa tatu asubuhi.

**Wahitimu wote watakaoshiriki sherehe za mahafali wanashauriwa kuzingatia yafuatayo:-**

1. Kuthibitisha ushiriki wao kwa maandishi kwa Naibu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala kupitia **ita@tra.go.tz** kabla ya tarehe **10 Novemba, 2022.**

2. Kulipa Tsh. 50,000 kwa ajili ya kukodi joho na kuwasilisha stakabadhi ya malipo kwa mhasibu wa chuo kabla au ifikapo tarehe **23 Novemba, 2022.** (Malipo yafanyike kwa mtandao kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG).

3. Kuhudhuria mazoezi na kuchukua majoho tarehe **23 Novemba, 2022** kuanzia saa 3:00 asubuhi.

4. Wahitimu watakaoshiriki mahafali wanapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.

Sherehe za mahafali zitatanguliwa na Kongamano la Wahitimu wote (Convocation) waliosoma katika Chuo cha Kodi litakalofanyika chuoni tarehe **23 Novemba, 2022** kuanzia saa tatu asubuhi.

Wahitimu wote wa ITA wanaalikwa kuhudhuria kusanyiko hili.

**WOTE MNAKARIBISHWA!**

**Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:-**

**Mkuu wa Chuo**
**Chuo cha Kodi**
**S.L.P 9321, Dar es Salaam**
**Simu: 022 2216800/1 au 0783081348**
**Barua pepe: ita@tra.go.tz**

217056202

# Tanzania yashinda nafasi ya pili usalama mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA, imeshinda nafasi ya pili ya washindi bora katika Kielelezo cha Usalama wa Mtandao (GCI) kwa mwaka 2020 kati ya nchi 52 za Bara la Afrika.

Orodha ya Usalama mtandaoni ambayo hutolewa na Shirika la Mawasiliano la Kimataifa (ITU), lenye makao yake makuu mjini Geneva, Uswidi, imeonesha kuwa Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi za juu katika kukabiliana na matukio ya dharura za usalama katika anga la mtandao.

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), iliyotolewa jana ilisema ITU imeiweka Tanzania katika nafasi ya pili kwa mshindi bora barani Afrika ikiwa mbele katika kukabili mashambulizi ya mtandaoni kwa kiwango stahiki.

"Mashambulizi ya anga limekuwa tatizo sugu kwa baadhi ya nchi duniani yakisababisha athari katika mifumo ya mawasiliano na TEHAMA na kukwaza jitihada za kukuza uchumi.

Ripoti ya ITU iliyowasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa TCRA Dk. Jabiri Bakari (pichani) inaonesha katika Kanda ya Afrika nafasi za Global Cyber Index (GCI) Tanzania imepata maksi 90.58 ikiwa ya pili kwa ubora katika kukabili dharura za mtandaoni baada ya mshindi wa kwanza, Mauritius aliyepata alama za jumla 96.89. Ghana ilibuka mshindi wa tatu kwa jumla ya alama 86.69.

"Vita vya kimtandao ni tishio la wakati halisi kwa maendeleo ya uchumi wa kijamii wa watu na serikali sio tu ndani ya nchi bali pia katika ngazi ya kimataifa," alisema Dk. Bakari.

Dk. Bakari alisisitiza kuwa, mashambulizi ya mtandaoni ni hatari kuliko silaha za kisasa. "Kwa sababu hayahitaji kuwapo kwa wahalifu kwa sababu hayana kikomo cha umbali na yanalenga miundombinu muhimu ya nchi na taasisi na



kusababisha uharibifu mkubwa ambao haujawahi kutokea."

Ushindi wa Tanzania katika nafasi hiyo ulihusisha vigezo mbalimbali muhimu vya usalama wa mtandao vikiwamo Sheria na Kanuni za uhalifu mtandaoni na usalama wa mtandao, kupima utekelezaji wa uwezo wa kiufundi kupitia wakala wa kitaifa na sekta mahusus, kupima mikakati ya kitaifa na mashirika yanayotekeleza usalama wa mtandao, ukuzaji wa uwezo unaohusisha kupima kampeni za uhamasishaji, mafunzo, elimu, na motisha kwa ajili ya kukuza uwezo wa usalama mtandao pamoja na kiwango cha ushirikiano na ushirikiano na nchi nyingine, mashirika na kampuni.

"Haja ya kuwa na anga la mtandao ambalo ni salama ni muhimu zaidi kuliko hapo awali, hasa tunapozidi kutegemea "njia za maisha za kidijitali" katika mazingira dunia inapokabiliana na maradhi ya mlipuko ikiwamo UVIKO-19," alisisitiza Mkurugenzi, Ofisi ya Maendeleo ya Mawasiliano ya ITU, Doreen Bogdan-Martin.

Global Cybersecurity Index (GCI) ni mpango wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU), ambalo ni wakala maalumu wa Umoja wa Mataifa wa kusimamia masuala ya TEHAMA duniani.

# Mbaroni tuhuma mauaji ya bibi na shangazi zake

**Na Hamisi Nasri,** NACHINGWEA

MKAZI wa Kijiji cha Mchangani, Nachingwea mkoani Lindi, Raymond Milandi (33), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuwaua ndugu zake watatu ambao ni bibi yake na shangazi zake wawili kutokana na mgogoro wa kugombea shamba la urithi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Pilly Mande, aliwaambia waandishi wa habari jana mkoani Lindi kuwa tukio lilitokea juzi katika kijiji cha Mchangani, Nachingwea.

Mande alisema waliouawa na kijana huyo ni Angela Kambanga (76), Esther Jota (68) Lydia Jota (58) wote wakazi wa kijiji cha Mchangani.

Alisema siku ya tukio ndugu hao walikusanyika na kwenda kufanya usafi katika kaburi la baba yao katika makaburi yaliyoko kijijini hapo na wakati wakiendelea kufanya usafi, ndipo alipotokea Milanzi akiwa ameshika panga na kuwataka waondoke akiwaeleza kuwa hawaruhusiwi kuingia shambani.

Kamanda Mande alisema ndugu hao wakiwa wanaondoka kwenye shamba hilo, mtuhumiwa huyo naye alichukua baiskeli yake na kuondoka.

Mande alisema baada ya mtuhumiwa kuondoka, ndugu hao walirudi na mtuhumiwa Milanzi ambaye alikutana nao njiani, aliwaambia warudi katika kaburi hilo ili waendelee kufanya usafi.

Alisema walipofika kwa mara ya pili, ndipo alianza kuwashambulia kwa kuwachoma na kitu chenye ncha kali na Angela alijeruhiwa chini ya kwapa na kisu kikaenda mpaka kwenye mapafu wakati Lydia alijeruhiwa titi la kushoto na katikati ya kifua huku Esther akijeruhiwa katikati ya titi la kushoto na kulia .

Milanzi kwa mujibu wa Kamanda Mande, anashikiliwa na polisi na taratibu zote za kumfikisha mahakamani zinaendelea na mara zitakapokamilika atafikishwa ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

# Mahakama EAC yaongezewa meno

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limeiongezea mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, uwezo wa kuondoa utata wa mashauri yanayotokana na utekelezaji wa itifaki ya Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja wa Sarafu.

Kabla ya azimio la bunge la kuridhia itifaki hiyo, utaratibu wa sasa, endapo kunajitokeza mgogoro katika kutekeleza itifaki hizo, shauri huamuliwa na mahakama ya nchi mwanachama ambako mgogoro umetokea, ambako huweza kusababisha tafsiri tofauti za itifaki miongoni mwa nchi wanachama.

Akitoa maelezo jana kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya kuongeza mamlaka Mahakama ya Afrika ya Mashariki, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema ili kuondokana na dosari za namna hiyo, kuna haja ya kuipa mahakama husika, mamlaka ya kushughulikia mashauri yanayotokana na itifaki hizo.

Kwa kufanya hivyo, alisema kutatoa tafsiri za kisheria zitakazotumika katika nchi zote wanachama inapotokea utata kuhusu tafsiri ya vipengele mbalimbali vya itifaki hizo.

"Lengo la kuridhia itifaki hii ni pamoja na kuiongezea mamlaka Mahakama ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili kutekeleza majukumu ya kutatua migogoro ya biashara na uwekezaji ya Itifaki ya Umoja wa Forodha, Itifaki ya Soko la Pamoja na Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

"Vilevile kuridhiwa kwa itifaki hii, kutaongeza fursa za ajira kwa Watanzania wa kada mbalimbali wakiwamo majaji," alisema.

Waziri Dk. Ndumbaro pia alisema hatua hiyo ni muhimu hasa kunapotokea migogoro inayohusisha raia wa nchi zaidi ya moja, wanachama au mali zisizohamishika zilizo nje ya nchi kukitokea mgogoro.

Tanzania ikiwa ni moja ya nchi wanachama wa EAC, iliridhia uanzishwaji wa Umoja wa Forodha (2004), Soko la Pamoja (2010) na Umoja wa Sarafu (2013).

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Khajida Taya maarufu Keisha, alisema kamati inaitaka serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi, kuhusu mamlaka ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki.

Mahakama hiyo, kwa mujibu wa Waziri Dk. Ndumbaro, inashughulikia migogoro mbalimbali, ambayo inaweza kuibuka katika kutekeleza masharti ya itifaki mbalimbali zinazotumika katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

## Serikali yaokoa bil. 22/- umeme wa gridi ya taifa Kasulu, Kibondo

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeokoa Sh. bilioni 22.4 kwa mwaka, zilizokuwa zikitumika kununulia mafuta na matengenezo ya majenereta katika wilaya za Kibondo na Kasulu mkoani Kigoma, baada ya kuunganisha na umeme wa gridi ya taifa.

Juzi, mitambo ya umeme iliyokuwa ikitumia mafuta ya dizeli ilizimwa na wateja 10,000 katika mkoa huo tayari wameshaunganishwa kwenye umeme wa gridi ya taifa.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema gharama hizo zinatumika katika wilaya hizo mbili peke yake bila kuhusisha wilaya ya Kigoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na Kigoma pia maeneo ya Nyakanazi, Biharamulo na Ngara mkoani Kagera nayo yameunganishwa katika umeme huo.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa TANESCO imekamilisha ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za msongo wa kilovoti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi, kilovoti 33 na kilovoti 400 katika mkoa wa Geita na Kigoma pamoja na kilovoti 33 kutoka Nyakanazi hadi Kakonko kwa lengo la kuunganisha Kakonko, Kibondo na Kasulu.

Ilieleza kuwa tayari imezindua kituo cha kupokea na kupoza umeme chenye kilovoti 220/33 cha Nyakanazi na inaendelea na mpango wa kukamilisha ujenzi wa njia ya kufikisha umeme wa msongo wa Kilovoti 33 wilayani Kasulu hadi Kigoma mjini kufikia mwanzoni mwa mwaka 2023.

"Kukamilika kwa ujenzi wa njia hizi za kupeleka umeme wa msongo wa kilovoti 33 wa gridi ya taifa kumewezesha kuimarisha huduma ya upatikanaji umeme kwenye maeneo yaliyokuwa yanategemea umeme wa kuzalishwa kwa mashine nne zilizokuwa zikitumia mafuta ya dizeli," inaeleza taarifa.




Mshauri wa Usalama, Afya, Mazingira na Mahusiano ya Jamii wa Kampuni ya Kioo Ltd, Richard Msumule (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa mashine ya kutoa nakala 'photocopy' yeye thamani ya Sh. milioni 2. 9 kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Vianzi Mkuranga, Veronica Temu, jijini Dar es Salaam jana, kwa lengo la kusaidia mahitaji ya shule hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Anayedaiwa kugongwa na gari la Magereza azikwa, ndugu wanena

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWILI wa Mkazi wa Miyuji jijini Dodoma, Richard Bukombe, aliyefariki dunia kwa kile kinachodaiwa na ndugu zake kugongwa na gari la Jeshi la Magereza, ulizikwa juzi kwenye makaburi ya Chang'ombe, jijini hapo.

Ndugu wa marehemu wameliomba Jeshi la Polisi na uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, kufanya uchunguzi ili kubaini mwili wa marehemu uliingiaje katika chumba cha kuhifadhia maiti.

"Tunataka kujua mwili wa ndugu yetu uliingiaje mochwari na nani aliuleta wakati ndugu yetu hakuwa mgonjwa ambaye amelazwa pale. Kamera za ulinzi ziangaliwe ili tujiridhishe ni nani aliupeleka mwili wa marehemu pale," alisema Bulole Bukombe, mdogo wa marehemu.

Pia alisema pamoja na kuomba kufanywa kwa uchuguzi huo, pia familia imekubaliana kwenda kumwona Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Yussuf Hamad Masauni, ili kupata haki ya kifo cha ndugu yao.

Akizungumza kuhusu uamuzi wa kuzika mwili huo, alisema familia ilifanya kikao na kukubaliana kuuzika huku hatua zingine za kupata haki ya kifo cha ndugu yao zikiendelea.

"Mwili wa marehemu ulikaa mochwari kwa zaidi ya siku tano lakini nyumbani wageni ambao walikuja kwa ajili ya shughuli za mazishi walikaa kwa muda mrefu, hivyo tukaona tuzike kwanza halafu mambo mengine yaendelee na kama familia tutaendelea kupambania haki ya kifo cha ndugu yetu hadi ipatikane," alisema Bukombe.

Alisema kabla ya kuuzika mwili huo, ulifanyiwa vipimo na daktari na kubainika kuwa ulikuwa umeharibika kwa ajali, hivyo kutokana na hali hyo, wanaiomba serikali kuwafikisha mahakamani wote waliofanya unyama huo.

"Hadi sasa tunaamini kuwa ndugu yetu hakufa kwa ajali pale pale. Inawezekana kuwa walimmalizia wakati wakiwa njiani ili kupoteza ushahidi. Kama hawahusiki kwa kifo chake kwa nini waliompeleka hospitali wanaficha utambulisho wao.

"Tunaomba sana haki itendeke kwani namba za gari lililomgonga tunazo, jina la dereva tunalo. Magereza wasijifiche, watoe ushirikiano. Tutatoa ushahidi wakati mwafaka ukifika ili jambo hili liishe. Tunachotaka ni haki ya ndugu yetu. Ni aibu kwa jeshi kufanya kosa na kujificha. Hii inafundisha nini kwa raia wengine?" Alihoji.

Bukombe aliwataka viongozi wakuu wa Jeshi hilo la Magereza kulifuatilia suala hilo ambalo limepoteza uhai wa mtu badala ya kuendelea kukanusha kila wanapoulizwa na vyombo vya habari.

"Ndugu yetu hakuwa amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, inakuwaje akutwe mochwari na hakuna taarifa yoyote ya mtu aliyemleta wala aliyekabidhi mwili wake? Inabidi viongozi wa Magereza wajiulize na kufuatilia jambo hili kwa karibu ili kujibu maswali mengi ya wanafamilia," alisema Bukombe.

Bukombe, maarufu kwa jina la Baba Paroko, anadaiwa kugongwa na gari la Magereza (Landcruiser Pick Up) Septemba 13, mwaka huu, jirani na eneo la hoteli ya Twiga, Msalato jijini hapa.

Kwa mujibu wa ndugu zake, aligongwa na gari hilo majira ya saa 12:30 jioni na baadhi ya askari wa jeshi hilo walimchukua na kuondoka naye.

Ofisa Magereza Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi (ACP) Kenneth Mwambije, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alikiri kuwa analifahamu kama ambavyo watu wengine wanavyolisikia lakini akasisitiza kuwa watu wa kulitolea ufafanuzi ni makao makuu ya jeshi hilo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Masauni, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema anaomba kwanza kukutana na wanafamilia hao ili kusikiliza malalamiko yao.

# Mikakati kukabiliana na kifua kikuu yatajwa

SERIKALI imetaja mikakati mbalimbali ya kukabiliana na kifua kikuu (TB) ikiwamo mwaka huu kuviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya 1,859 kupima ili wagonjwa waanzishiwe matibabu mapema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana bungeni jijini hapo alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji, ambaye alihoji mkakati wa serikali wa kudhibiti maambukizi ya TB.

Dk. Mollel alisema mkakati uliopo ni kufikisha huduma ngazi za chini na kwa bajeti ya mwaka huu, vituo 1,859 vitawezeshwa kupima na kutakuwa na mashine za kisasa za X-Ray ambazo zitapelekwa nchi nzima na kila mkoa utakuwa na yake ili kuzunguka kwa jamii kusaidia.

Pia alisema mkakati mwingine ni kufanya utafiti kwa kushirikiana na vyuo vikuu mbalimbali duniani ambao umefanyika katika Hospitali ya Kibong'oto wilayani Siha ambao ulilenga kuangalia vinasaba vya TB.

"Huko nyuma TB ilichelewa kugundulika mapema kuwa na ugonjwa huo sasa ni TB mfu, sasa imegundulika kupitia Hospitali ya Kibong'oto teknolojia ya RNA ambayo inatambua kwa haraka. Kwa sasa kuna vipimo ambavyo vimegunduliwa na madaktari wa wazawa kwa kushirikiana na Marekani vya kutambua mapema vimelea," alisema.

Kadhalika, alisema serikali imenunua magari maalum ambayo ni hospitali tembezi yenye vifaa vya kisasa vya X-Ray ambavyo vinatembea mikoani na kupima wananchi kwenye matamasha na makongamano mbalimbali.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji kwa nini ugonjwa wa TB hauwezi kuonekana kwa mara moja unapompata mwathirika.

Naibu Waziri Mollel akijibu swali hilo, alisema TB huchelewa kuonekana kutokana na tabia na mwenendo wa vimelea vyake kuzaliana taratibu mwilini na mara nyingi hudhibitiwa na kinga ya mwili wa aliyeambukizwa.

"Hivyo kila mgonjwa ataanza kuonyesha dalili za ugonjwa kutegemea hali ya kinga ya mwili wake," alisema.

Naibu Waziri alitoa wito kwa wananchi kuwahi mapema katika vituo vya kutolea huduma za afya kupimwa mara tu wanapojisikia dalili zifuatazo, homa za mara kwa mara, kikohozi cha wiki mbili au zaidi, kutoa makohozi yaliyochanganyika na damu, kupungua uzito kwa haraka bila sababu ya msingi na kutokwa jasho jingi hasa usiku.




Habari zote: Augusta Njoji DODOMA



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kanuni biashara hewa ukaa zaja

OFISI ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wizara za kisekta na wadau, inaandaa mwongozo na kanuni za usimamizi wa biashara ya hewa ukaa ambazo zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Oktoba, mwaka huu.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Khamis, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavejuru Felix.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mikakati gani kuelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi za misitu kuhusu biashara ya uuzaji au utunzaji wa hewa ukaa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema katika kuhakikisha Watanzania na serikali inanufaika na biashara ya hewa ukaa mwongozo na kanuni hizo zitaonyesha namna ya kuratibu na kusimamia biashara hiyo ikiwamo mgawanyo wa manufaa kwa wadau watakaohusika katika mnyororo wa biashara ya hewa hiyo nchini.

Pia alisema baada ya kukamilika kwa mwongozo na kanuni, serikali imejipanga kuendelea kutoa elimu kuhusu biashara ya hewa ukaa kwa wadau mbalimbali wakiwamo wananchi ambao sehemu kubwa ya biashara hiyo hufanyika katika maeneo yao.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji katika kuandaa mwongozo huo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ambao wamekuwa na migogoro na wananchi wanaozunguka misitu hiyo wameshirikishwaje.

"Je, serikali haioni haja ya kushuka kwa wananchi kutoa elimu kuhusu hewa ukaa ili kujenga ufahamu zaidi?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Khamis, alisema miongoni mwa wadau muhimu walioshirikishwa kwenye mwongozo huo ni TFS na taasisi nyingine za binafsi na serikali.

Pia alisema suala la elimu tayari kuna kwenye mpango kutakuwa na timu maalum itakayozunguka kutoa elimu kwa wananchi ili kujua fursa na faida za kimazingira zilizopo kwenye mradi huo.

# Vijana warasmishwa kupitia taaluma, ujuzi

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, vijana 18,445 wamejitokeza na kujaza fomu kwa ajili ya kurasmishwa ujuzi wao kupitia programu ya taifa ya kukuza ujuzi na taratibu zinakamilishwa ili kupatiwa fursa hiyo.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima.

Katika swali lake, Sima huyo alihoji mkakati wa kurasimisha vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi.

Akijibu swali hilo, alisema serikali ina mkakati kupitia mpango wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano wa kurasmisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kwa vijana 100,000 ifikapo mwaka 2025/26.

Pia alisema katika utekelezaji wake, hadi Juni, mwaka huu, kupitia programu ya taifa ya kukuza ujuzi, vijana 22,296 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara wamerasmishwa ujuzi wao.

"Tunazo fani 10 zinazohusika katika urasimishaji ambazo ni uashi, useremala, ufundi magari, upishi na uhudumu wa hoteli, baa na migahawa, ufundi bomba, unyooshaji bodi za magari, umeme wa majumbani, ushonaji nguo na uchomeleaji vyuma," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, alihoji serikali haioni umuhimu wa kuwapatia vyeti mafundi hao ili kuajiriwa maeneo mbalimbali.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema katika utoaji wa mafunzo hayo yanaenda sambamba na utoaji wa vyeti ili watambulike.

"Pia serikali imeenda mbali zaidi ya hao vijana kuwapa vyeti, wanakutanishwa na Halmashauri ili kupatiwa fedha kama mtaji wa kuanza shughuli zao," alisema.

Pia alisema wamekuwa wakipelekwa kwenye maeneo ya kufanya kazi na kuajiriwa ambapo vijana 1,800 wamepata kazi kupitia Sh.bilioni tisa zilizotolewa na serikali kwa mwaka wa fedha uliopita.



## HABARI ARUSHA

# H'shauri yaanza usimamizi mashauri ya watoto mitaani

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Meru iliyoko wilayani Arumeru mkoani Arusha, imeanza mpango wa utekelezaji wa mfumo jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi kwa kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa mashauri hayo kwa ngazi ya jamii.

Wasimamizi mashauri waliopatiwa mafunzo hayo ni pamoja na watendaji wa vijiji, maofisa ustawi wa jamii na maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata lengo likiwa kutoa huduma kwa kundi hilo.

Akifungua mafunzo hayo jana, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Charles Makama, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mazingira, aliwataka washiriki kuhakikisha wanatumia mafunzo hayo kikamilifu ili kuwatambua na kuwapa huduma watoto wote wanaoishi katika mazingira hatarishi.

"Ndugu washiriki wa mafunzo haya hakikisheni mnatumia nafasi hii kwenda kuwatambua na kuwahudumia watoto walioko kwenye mazingira magumu na hatarishi kwenye jamii yetu," alisema.

Makama alisema utekelezaji wa mfumo huo unaotekelezwa na serikali kwa kushirikiana mradi wa KIZAZI Hodari ulianza mwaka 2017 katika halmashauri 81 nchini zikiwamo Halmashauri za Jiji la Arusha na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Alisema mradi huo, umetekelezwa kwa miaka mitano na kwa sasa umetoa fursa kwa Halmashauri ya Meru kwa kuwa mfumo huo, umelenga kuwafikia watoto 7,000 kwa Mkoa wa Arusha wakiwamo watoto wa eneo hilo.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, alisema: "Napenda kutoa wito kwa wananchi na jamii kwa ujumla kuhakikisha wanawalinda na kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na hatarishi kwa kuwa nao ni sehemu ya watoto katika jamii inayowazunguka."

# Kiwanda chapewa siku 14 kujenga mitambo ya majitaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Hamad Chande, ametoa miezi miwili kwa Kiwanda cha A to Z kilichoko jijini Arusha, kukamilisha ujenzi wa mitambo ya kutibu majitaka, yanayotiririka kwenda kwenye makazi ya wananchi kutoka kiwanda hicho.

Aidha, ameuagiza uongozi wa kiwanda hicho kuongeza miradi ya ujirani mwema ikiwamo kujenga kituo cha afya ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha sekta ya afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa ziara yake ya siku moja kiwandani hapo, kutokana na malalamiko aliyopata kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani na kiwanda hicho juu ya majitaka yanayotirika kutoka ndani ya kiwanda kwenda kwenye makazi yao.

"Nilikuwa nimejipanga kuja kufunga hiki kiwanda, lakini narudi na funguo zangu kwa sababu nimekuta mmeanza kutekeleza maelekezo ya serikali, kwa kuanza ujenzi wa miundombinu ya kisasa, kwa ajili ya kutibu majitaka na ujenzi ukikamilika maji hayatatiririka tena kwenda kwa wananchi.

"Mmeniahidi hapa ujenzi utakamilika baada ya miezi miwili kuanzia sasa ikifika Januari mwakani, nitakuja kukagua kama kweli mradi umeshakamilika na nikikuta bado hatutaelewana," alisema.

Kwa mujibu wa Chande, alisema serikali imedhamiria kukuza uchumi kupitia sekta ya viwanda, lakini ujenzi wa viwanda hivyo lazima uzingatie usalama wa wananchi wanaoishi jirani na maeneo hayo.

Kuhusu miradi ya ujirani mwema iliyotekelezwa na kiwanda hicho, Naibu Waziri huyo, aliutaka uongozi wa kiwanda hicho, kuongeza miradi mingi zaidi kulingana na ukubwa wake, ikiwamo kujenga kituo cha afya ili wananchi waweze kupata huduma bora za afya.

"Mmenieleza kwamba mmejenga madarasa matano, mmetoa msaada wa tangi la maji na kutoa chakula cha mchana kwa shule za msingi za hapa jirani hii bado haitoshi jengeni kituo cha afya ikibidi kwa wananchi wa eneo hili,"aliongeza.

Aidha alitumia fursa hiyo, kuupongeza uongozi wa kiwanda hicho, kwa kutoa ajira kwa watu zaidi ya 8,500 ambao ni wazawa, pamoja na kulipa kodi stahiki za serikali kwa wakati.

"Nimeridhishwa sana kwa namna mlivyotoa ajira nyingi kwa wananchi wazawa, pia kutoa kipaumbele kwa wanawake kwa kuwa tumeshuhudia hapa wengine wakiwa wakuu wa vitengo kikiwamo cha maabara,"alisema.

Meneja Mazingira wa Kiwanda hicho, Harrison Rehumbiza, alisema ujenzi wa mitambo hiyo, unatarajiwa kumalizika Desemba mwaka huu.

"Mradi huu, unakaribia kukamilika matangi ya kuhifadhi maji yanayotoka kiwandani kwa ajili ya kusafishwa yapo tayari na tumeshaanza kuweka maji kwa ajili ya majaribio,"alisema.

Meneja Usafirishaji wa Kiwanda hicho, Sylvester Kazi, alisema kiwanda hicho, kinatengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo fulana, vyandarua na bidhaa za plastiki. Alisema; "Licha ya bidhaa hizo, tumeanza kutengeneza vifungashio vya nafaka, vyandarua vya kitalu nyumba na vifungashio wa saruji, kadhalika tumetekeleza miradi ya ujirani mwema kwa kujenga vyumba vitano vya madarasa, tangi la maji na kutoka chakula cha mchana kwa shule za msingi za jirani na kiwanda chetu."



Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis (katikati), akitoa maelekezo alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya serikali kuhusu kuondoa changamoto ya harufu na majitaka yanayotiririka kupita mtaro unaopita kwenye makazi ya watu, katika kiwanda cha nguo cha A to Z, jijini Arusha juzi. **PICHA: OMR**

# Moto wateketeza bweni Sekondari Engutoto

**Na Allan Isack,** MONDULI

WANAFUNZI zaidi ya 190 katika Shule ya Sekondari ya Engutoto, iliyoko wilayani Monduli mkoani Arusha, wamekosa sehemu ya kulala baada ya bweni lao kuteketea kwa moto.

Hadi sasa chanzo cha bweni hilo, kuteketea kwa moto hakijajulikana na wanafunzi hao wamelazimika kutumia baadhi ya madarasa kama sehemu ya kulala. Jana Mbunge wa Monduli, Fredy Lowasa, alitoa pole kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Engutoto, walimu wa shule hiyo, wazazi, wanafunzi pamoja na wananchi wa eneo hilo, kutokana na janga la moto lililotokea Septemba 17 mwaka huu.

"Septemba 17, mwaka huu, tukiwa kwenye mazishi huko Kata ya Lashaine, wakati tunatoka tukapigiwa simu kwamba kuna moto umetokea katika Shule ya Sekondari Engutoto.

"Tuliwahi tukamkuta mwalimu mkuu pamoja na viongozi wengine wa serikali kutoka wilayani walikuwa tayari wamefika katika eneo la tukio na walishirikiana kuzima moto, pia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walipigiwa simu walifika kwa wakati kutusaidia katika kuzima moto kwa kuwa ulikuwa mkubwa sana," alisema mbunge huyo.

Aidha, alilishukuru na kulipongeza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kufika kwa wakati kutoka Arusha Mjini kwenda kuwasaidia kuzima na kuokoa baadhi ya vitu.

Hata hivyo, aliiomba serikali kwa sasa kupeleka gari la kuzima moto katika Wilaya ya Monduli, kwa kuwa majanga kama hayo yakitokea nyakati za usiku itakuwa hatari sana hadi kusubiri gari kutoka Arusha Mjini.

Naye Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Magreth Muro, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa shule hiyo, Isaya Swai, aliwashukuru wadau waliojitokeza kuwasaidia kukabiliana na janga hilo.

Ofisa Elimu huyo, alisema wako watu waliojitokeza kutoa msaada akiwamo mbunge kwa kuwa ameshirikiana na Shirika la Msalaba Mwekundu kutoa magodoro 200, mashuka 200 pamoja na vyandarua 200.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kutatua matatizo zinazoikabili shule hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, aliziagiza taasisi zinazohusika kufanya uchunguzi haraka kubaini chanzo cha tukio hilo, ili hatua zichukuliwe.

Mkuu huyo wa Mkoa, aliwataka wakuu wa shule na kamati zake, kujipanga kuhakikisha wanachukua tahadhari zote za kudhibiti athari zozote zitakazotokea kwa wanafunzi na miundombinu wanayotumia kwa kuwa kila jambo linalotokea kutokana na chanzo hivyo ni lazima ijulikane na kidhibitiwa.



## Maofisa elimu watakiwa kusimamia uandikishaji shule wenye ulemavu

**Na Mary Mosha,** SIHA

MAOFISA elimu maalumu ngazi ya kata na wilaya katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wametakiwa kuhakikisha watoto wote wenye ulemavu katika eneo hilo, wanaandikishwa shule mwaka 2023.

Pia wametakiwa kupata takwimu sahihi za watoto wenye ulemavu wilaya humo, ili iwe rahisi kuwaandikisha shule jumuishi kutokana na aina ya ulemavu walionao.

Agizo hilo lilitolewa jana na Ofisa Elimu Shule ya Msingi katika eneo hilo, Rose Sandi, wakati akizindua zana jumuishi za kufundishia na kujifunzia kwenye madarasa jumuishi katika Shule ya Msingi Sanya Juu.

Alisema lengo la serikali ni kutoa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu na watoto hao, wakipatiwa elimu watakuwa na uwezo mkubwa wa kupata fursa za kufanya kazi mbalimbali zikiwamo za kuajiriwa na kujiajiri.

"Naagiza maofisa elimu maalumu ngazi ya kata na maofisa elimu wote idara ya msingi, tunaanza kazi ya uandikishaji wa wanafunzi mwaka 2023, hakikisheni hakuna mtoto mwenye ulemavu wowote haachwi nyuma, iwe wa akili, usonji au ulemavu wa viungo ili kuwasaidia watoto hao, kwa kuwa wataalamu tunao.

"Kwa kufanya hivyo, kutaondoa mzigo kwa jamii na wataweza kujitegemea wenyewe, serikali inamipango imara na endelevu, tulianza na darasa moja, lakini kwa sasa tunayo mengi, watoto wanafundishwa kutumia dhana," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu Tanzania, Graciana Lyimo, alisema serikali imeanza kufundisha walimu mbinu za kutengeneza zana za kufundishia watoto wenye mahitaji maalumu kutokana na uwapo wa upungufu wa zana hizo hapa nchini.

Baadhi ya walimu waliopata fursa ya kutengeneza zana jumuishi za kufundishia, akiwamo Mkuu wa Shule ya Msingi Sanya Juu, Beatrice Matela, alisema kupitia kitengo cha elimu maalumu kilichoanzishwa shuleni hapo, kimesaidia kupata elimu jumuishi.

Alisema: "Kwa sasa watoto wenye ulemavu wamechanganyikana na watoto wa kawaida na wanafundishwa pamoja na watoto wa kawaida, tunatumia mbinu mbalimbali ikiwamo ya utengenezaji wa dhana, elimu kwa vitendo, itasaidia kujenga kizazi cha baadaye kuwa na usawa na watu wenye ulemavu.

Aliongeza: "Pamoja na hayo yako matatizo tunayokabiliana nayo, kama watoto wanaletwa hawajui kutembea vizuri, inabidi kuanza kuwafundisha, pia bado walimu wengi hawajapata elimu hiyo".

# Mabadiliko ya tabianchi yaathiri miradi ya kilimo

**Na Asraji Mvungi,** MWANGA

MIRADI ya kilimo na ufugaji wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi yaliyochangia kuwapo kwa ongezeka la magonjwa ya mifugo na wadudu kwenye mazao ya chakula, mboga na matunda.

Wakizungumzia tatizo hilo, baadhi ya wananchi wilayani humo, akiwamo Yusuph Juma, alisema mazao yanayoshambuliwa na wadudu ni maharage, migomba, mpunga, nyanya, huku kwa upande wa mifugo ni kuku, mbuzi na sungura.

"Kwa kweli tunalima na tunafuga lakini tunapata hasara kwa kuwa magonjwa na wadudu yanatusumbua sana, licha ya kushauriwa na wataalamu kutumia dawa bado tatizo ni kubwa, pia gharama za kilimo na ufugaji zinaongezeka tunahitaji msaada,"alisema Juma.

Kutokana na tatizo hilo, wadau mbalimbali wameanza kujitokeza kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, kusaidia kukabiliana na tatizo hilo, likiwamo Kanisa Katoliki Jimbo la Same, wameanzisha mradi wa kuwasaidia wananchi hao kupunguza makali ya tatizo hilo.

Akizungumzia hatua hiyo, Msaidizi wa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Wilhad Philipo, alisema mradi huo, umefadhiliwa na Baraza la Maaskofu wa Katoliki Ujerumani na utatekelezwa katika kata tatu wilayani humo.

Mratibu wa Idara ya Maendeleo Kanisa Katoliki, Pamela Mainda, alizitaja kata zitakazotekeleza mradi huo, ni Kileo Kifula na Kiria kwa kuwa zina fursa ya kilimo cha umwagiliaji cha mazao mbalimbali yakiwamo ya mpunga, ndizi na mboga, pia ufugaji wa wa mifugo wa kuku, mbuzi na sungura kwa kuwa mradi umelenga kuwanufaisha wananchi 561 katika vitongoji 17 vya kata hiyo.

Mmoja wa wataalamu wa kilimo, wanaosaidia wananchi hao, Besodi Msita, alisema nguvu kubwa imeelekezwa kuelimisha wananchi kuhusu mbinu za kuhimili kasi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia rasilimali walizonazo kuzalisha kwa tija.

Mwakilishi wa wahisani hao, kutoka nchini Ujerumani, Dk.Regine Brandt, alisisitiza umuhimu wa ushirikishaji wananchi katika utekelezaji wa miradi hiyo, kwa kuwa ikikamilika itakuwa na tija kwao na Taifa.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdalah Mwaipaya, amelishukuru Kanisa Katoliki Jimbo la Same, wahisani hao, kwa kuona umuhimu wa kushirikiana na serikali kukabiliana na tatizo hilo linalowakabili wananchi.




Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, akizungumza katika mahafali maalum ya maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), katika Shule ya Polisi Tanzania (TPS) mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro mapema wiki hii. **PICHA: JAMES LANKA**

## 'Watumishi mahakama zingatieni matumizi TEHAMA'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JAJI Mkuu Prof. Ibrahim Juma, amesema endapo watumishi wa mahakama watazingatia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utakuwa msingi bora wa kuwahudumia watu hasa kupata haki zao kwa haraka.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua masijala ndogo ya Mahakama ya Rufani kwa Mkoa wa Kilimanjaro, iliyofanyika mkoani Moshi.

"Matumzi ya TEHAMA yamerahisha utendaji wa shughuli nyingi ikiwamo za mahakama kwa kuwa tayari teknolojia hiyo, imeanza kutumika na mpango ulioko kwa sasa ni kuhakikisha mahakama zote, zikiwamo zile za mwanzo zinafungwa mifumo hiyo, ili wananchi waweze kufuatilia mashauri yao kwa ukaribu," alisema.

Alisema kwa kilichofanyika ni hatua kubwa katika mpango wa utoaji wa haki kwa jamii kwa kuwa itakuwa fursa kwa wananchi wa mkoa huo, ambao baadhi yao walikuwa wakisafiri umbali mrefu kwenda kusikiliza mashauri yao, yaliyokuwa kwenye ngazi ya rufani.

Baadhi ya wadau wa sheria akiwamo David Shilatu, aliipongeza mahakama kwa hatua hiyo, kwa kuanzisha masijala ndogo ya Mahakama ya Rufani mkoani humo, kwa kuwa itarahisha shughuli za mahakama, wananchi na wanasheria kwa ujumla.

"Tangu kuanzishwa kwa Masijala ya Mahakama Kuu mkoani Kilimanjaro 1993, kulikuwa hakuna masijala ndogo ya Mahakama ya Rufani, hivyo iliwalazimu watu kusafiri umbali mrefu kutoka nje ya mkoa kwenda kufuatilia mashauri yanayohusiana na mahakama hii," alisema.

Alisema kuna watu walikuwa wanasafiri umbali wa kilomita zaidi ya 200 kutoka Same kwenda Arusha au Dar es Salaam kufuatilia mashauri yao ya jinai na madai yaliyoko kwenye ya Mahakama ya Rufani.

"Kufuatia kufunguliwa kwa majisala hii, wananchi watapata fursa ya kufuatilia na kupitia kalenda ya mashauri yao hapa Kilimanjaro, badala ya kwenda Arusha au Dar es Salaam," alisema.

Naye Tamri Mndeme, kutoka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka ya Serikali Mkoa wa Kilimanjaro, alisema kuanzishwa kwa masijala hiyo, itawasaidia wanafunzi wanaosomea sheria mkoani humo.

"Wanafunzi wanaosomea sheria watapata fursa ya kupata elimu kwa vitendo mkoani hapo, badala ya kwenda Arusha au Dar es Salaam,"alisema.

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 22, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## VITA MIMBA ZA UTOTONI NCHINI UNFPA yataja mafanikio ikiwa na angalizo, Norway yakiri imevutiwa




## Ushuhuda wa vita kuikabili saratani kupitia mikakati afya, mkoa Manyara

Ukurasa 15

### DARASA LA NYWELE ZAKO...

# Hivi ndivyo zilivyo, namna ya kuzitunza kwa ufasaha kiafya

- Namna kinamama kuziosha, steaming...



Hali halisi ya nywele zilizohudumiwa na zinazohudumiwa katika namna tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Dk. Mussa Zaganzi**

MTU anaweza kujiuliza, nywele ni nini? Kitaalamu. Inatajwa ni nyuzi za protini zinazokuwa kwenye ngozi na ni moja ya wasifu unaomuelezea mwanadamu ni nani.

Kwa binadamu, nywele nyingi hupatikana kichwani, kwapani na maeneo ya faragha mwilini.

Namna ya kutunza nywele inatajwa kujumuisha kuziosha kwa maji ya vuguvugu na matumizi ya shampoo.

Hatua ya kwanza kuzisafisha nywele, inatajwa zinasafishwa kuondoa mafuta na uchafu unaoshikana na nywele, hasa kwa vile kwa baadhi ya watu huwa zinamaliza wastani wa wiki mbili, pasipo kuosha nywele.

Wenye nywele za asili huogopa kuziosha kila mara wakihofu zitasinyaa kuwa fupi. Njia bora inashauriwa, kwamba nywele zinapaswa kusafishwa walau kila wiki.

Pili, inaelezwa kwamba nywele inaweza kufanyiwa 'steaming' ambayo ni kitendo cha kuipa uhai nywele na hapo ipo katika namna nyingi.

Njia mojwapo inayoshauriwa kitaalamu na hufanyika kwa namna nyingi, zifuatazo zinatajwa kufaa: Kuchukua mayai matatu na yakatolewa viini vyake na inashauriwa vyema, ikatumika viini pekee; pia kuna kuongezewa vijiko sita vya asali.

Lingine, analitaja kuwa ni kuongeza mafuta ya parachichi kwenye nywele; hali kadhalika nywele kuwekewa mafuta ya kulainisha nywele, mfano habat sauda.

Baada ya hapo, la tatu analieleza ni kwa kuvuruga nywele, yenye mchanganyiko tajwa, kama mhusika hana muda wa kuandaa hiyo 'steaming' asilia, nunua kwa muuzaji unayemuamini.

Baada ya hatua hiyo, mwanamama anashauriwa kwamba, baada ya yote mtu apakae na mchanganyiko huo na kuvaa kofia ya kufunika.

***Mwandishi ni mtaalamu bingwa wa nywele na ngozi, anapatikana katika taasisi ya Natural Skin Solution na kazi hizo zinapatikana bure kupitia njia ya mtandao 'Online Skin Solution'. Simu yake ni + 255 713 039876.***

AFYA

## VITA MIMBA ZA UTOTONI NCHINI

# UNFPA yataja mafanikio ikiwa na angalizo, Norway yakiri imevutiwa

**Na Yasmine Protace**

DHANA rafiki wa afya ya uzazi, msingi wake unaangukia kuwapo miundombinu rafiki katika kuhudumia uzazi katika vituo vya afya, inayojumuisha upatikanaji huduma zote za msingi kiafya kwa mama na mtoto.

Hapo mwanamke anawekwa katika afya bora, wakati wa ujauzito, hata akajifungua salama kwa kujumuisha matunzo na lishe bora kwa mama na mtoto wake.

Kiafya, ukuaji ujauzito salama unategemea uzazi wa mpango kupata huduma muhimu, hadi anapofika hatua ya kujifungua salama.

Ndani ya utekelezaji Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), huwa kunashuhudiwa jinsi serikali inavyozindua vituo vya afya na zahanati, kuhakikisha kinamama, watoto wao na jamii kwa ujumla, zinapata huduma sahihi mahali waliko.

Dhamira ya serikali kupitia mipango yake, inatajwa ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na miongoni mwa yanayofanyika, ni kuboresha miundombinu katika vituo vya afya.

Ndani ya hatua hizo, serikali hadi sasa bado inajikita katika kutoa elimu ya uzazi wa mpango, jambo linalojidhihirisha kupitia matangazo yake ya uzazi wa mpango.




Wasichana wilayani Bunda katika hafla inayohusu ustawi wao, iliyoandaliwa na UNFPA.

### SAUTI YA UNFPA

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Mkazi (UNFPA), Mack Schreiner, anasema hadi sasa uwekezaji mkubwa unahitajika kuboresha huduma za afya ya uzazi wa mpango, ikiwamo kuzuia mimba za utotoni nchini.

Mark anawaambia wadau wa masuala ya uzazi jijini Dar es Salaam aliyokutana nao kwamba:"Tanzania ina idadi ya watu wenye nguvu. Uwepo wa afya ya ngono na uzazi ni lazima, ili kuwezesha kila mtu kustawi na kusaidia kufikia lengo la maendeleo ya taifa kama ilivyoainishwa katika mpango wa maendeleo."

Hapo anataja, idadi ya vijana nchini inaongezeka na hadi mwaka jana, zaidi ya asilimia 40 ya watu wote wako chini ya umri wa miaka 15, akieleza uwekezaji mkubwa unahitajika kuboresha huduma za afya ya uzazi wa mpango na kuzuia mimba za utotoni katika jamii.

"Tunatambua umuhimu wa kupanua huduma za afya na uzazi kwa kila mwanamke, mwanaume na kijana, ili kufikia uwezo wao kamili," anasisitiza na kufafanua UNFPA nchini inatumia mbinu nyingi kufanikisha namna sahihi ya upatikanaji haki za afya uzazi, ikishirikiana na wadau wa eneo hilo, kuwafikia vijana, kinamama na watoto wachanga.

Mwakilishi huyo anataja mafanikio katika mpango wa miaka nane wa UNFPA nchini ulioanza mwaka 2016 na kumalizika Juni iliyopita kwamba, yanajumuisha kuanzishwa vituo 103 vya ziada vya afya na kuongeza upatikanaji huduma za dharura za uzazi na huduma rafiki kwa vijana.

Anasema, hadi sasa kumeshawekwa sera na malengo ya kuboresha huduma za afya ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya na kuongeza uwekezaji katika sekta ya afya, huku serikali nchini imefanikiwa kuongeza huduma za afya ya uzazi kwa mama, mtoto na vijana katika umri balehe.

Ahadi yake nchini ni kwamba, UNFPA itahakikisha kuwa dawa za uzazi wa mpango zinatolewa kupitia serikali na wadau wengine wa maendeleo zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa kwenye mahitaji ya kijinsia na uzazi wa mpango.

### WAZIRI WA NORWAY

Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Norway, Anne Tvinnereim's, anasema wao wanaiamini Tanzania itafika mbali zaidi katika kuhakikisha upatikanaji huduma ya afya ya uzazi, ili kupunguza vifo vya mama na mtoto ,mimba zisizotarajiwa ikiwamo magonjwa ya zinaa.

Anasema, serikali ya Norway inaiona Tanzania kuwa ni miongoni mwa nchi zinazoaminika kufikia maamuzi ya kimataifa na kuhakikisha haki ya upatikanaji huduma za afya ya uzazi kabla ya mwaka 2030.

"Hatua hiyo imetokana na juhudi za serikali hususani utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, la kusimamia haki ya usawa kwa kuwarudisha shuleni wasichana waliokatisha masomo sababu ya mimba," anasema.

Anasema, binafsi alikutana na Rais Samia na kati ya waliyoteta, ni upatikanaji huduma za afya ya uzazi na haki kwa wote, jambo linaloipa Norway imani zaidi kwa Tanzania, kwamba iko katika njia sahihi.

Waziri Anne, anasema Norway kupitia UNFPA ambako ni mchangiaji wake mkubwa, itaendelea kuisaidia Tanzania katika utekelezaji masuala yanayohusiana na afya ya uzazi.

### WIZARA AFYA

Dk. Ahmed Makuwani, Mkurugenzi wa Huduma ya Afya ya Uzazi na Watoto, kutoka Wizara ya Afya, anasema msimamo wa serikali itaendelea kusaidia haki ya afya ya kijinsia na uzazi kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), mkakati unahusu kuanzisha au kuboresha afya kukiwapo zahanati, vituo vya afya, hospitali za kawaida na za rufani, katika maeneo yote watu waliko.

Dk. Makuwani anafafanua hiyo kwa kueleza haja ya kutolewa elimu ya kutosha hasa kwa wanawake, ikiwamo kuboresha miundombinu penye vituo vya afya na anakiri, serikali inatambua mchango wa wadau kutokomeza vifo vya mama na mtoto.

Anaahidi, wataendelea kuunga mkono mfumo wa uzazi uliopo, kwa kuongeza vituo vya afya, utoaji elimu na kuboreshwa miundombinu itakayowasaidia wanawake katika masuala ya uzazi salama.

Mkurugenzi huyo anakumbusha kwamba, maendeleo ya nchi yanaegemea ahadi zilizotolewa katika Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo wa mwaka 2019, ikijumuisha kuzuia vifo vya uzazi kupitia mpango wa kuhudumia afya ya uzazi na uzazi, mafanikio makubwa yakishuhudiwa.



Muuguzi akimpongeza mzazi baada ya kujifungua salama. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

# Ushuhuda wa vita kuikabili saratani kupitia mikakati afya, mkoa Manyara

## • Ajenda maalum kwa mama na mabinti zao

**Na Jumbe Ismailly, Hanang**

SARATANI ya shingo ya kizazi inahusiana na mabadiliko ya chembe hai za shingo ya kizazi, ambayo ni sehemu ya chini ya mji wa mimba (uteri) inayoungana na uke. Ni ugonjwa wenye kawaida ya kuchukua zaidi ya miaka 15 hadi 20 kugundulika mwilini, tangu mtu apate maambukizi ya virusi wanaosababisha ugonjwa huu.

Kabla ya kujitokeza bayana, mwili una kawaida ya kupata mabadiliko kadhaa yanayoweza kugundulika mapema na kuzuilika katika hatua za mwanzoni.

Maji hayo ambayo kwa jina la kitaalamu yanajulikana 'cervix' yanagusa sehemu ya kati ya faragha ya uzazi na mji wa mimba, sehemu yenye kazi nyingi kiafya, ikiwemo kupitisha mbegu za kiume kuelekea mirija ya uzazi, ili kupevusha yai.

Pia, ndiko kunakopitisha damu ya hedhi na eneo anakopita mtoto wakati wa kuzaliwa. Saratani ya shingo hadi sasa inaongoza kusababisha vifo vya wanawake wengi duniani, kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2010, ikikadiriwa asilimia 85 ya vifo hivyo vinatokea katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwemo katika wagonjwa na vifo.

Hata hivyo takwimu za ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi zinaonyesha kwamba,saratani ya shingo ya kizazi ni saratani inayoongoza kwa kusababisha vifo vya wanawake wengi duniani.

Tanzania inatajwa nayo ina saratani inayowaumiza sana kinamama hasa wenye umri wa miaka 15 hadi 44.

Mratibu wa Magonjwa ya Saratani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Restituta Kavishe, anayataja baadhi ya madhara yanayotokana na saratani, ni pamoja na mgonjwa kutokwa damu wakati wa kufanya tendo la ndoa, ikiendana na maumivu.

**ANENAVYO DMO HANANG'**

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', mkoani Manyara, Dk.Mohamed Kodd, anaieleza Nipashe namna wanavyokabiliana na janga hilo kwa kinamama.

Anasema, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, imekuwa na wagonjwa sita waliokuwapo mwaka 2014 na hadi mwaka jana wamekuwapo watano.

Daktari huyo anazitaja aina za saratani kuwa ni pamoja na saratani ya ngozi, shingo ya kizazi, koo, ziwa na chembe hai nyeupe za damu, akisema kinamama wa Hanang wanasumbuliwa zaidi na saratani ya mlango wa kizazi.

Hapo anazitaja tarafa zinazoongoza kwa wagonjwa wengi wa saratani, ni Bassoutu, Endasaki, Sumbay na Katesh, akisema ni takwimu za kipindi kati ya Januari hadi Oktoba mwaka jana, kati yao wawili sasa wanatibiwa katika Hospitali ya Ocean Road jijini Dar-es-Salaam na wagonjwa watatu wanatibiwa kutumia mashine iliyopo katika Hospitali wilayani Hanang.

Dk. Kodd anasema, matibabu ya ugonjwa huo katika hatua za awali yalipatikana wilayani hapo na kufikia hatua nyinginezo, kupatikana nje ya wilaya hiyo (Ocean Road), baada ya kuwapitishia katika Hospitali ya Misheni ya Haydom.




Wauguzi wa wilayani Hanang', mkoani, Manyara, wakiandamana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wauguzi. Hao, ni wakala muhimu katika vita vya kuikabili kansa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**



Wasichana wanafunzi wa Hanang'. Sehemu ya kundi maalum linalolengwa katika kuzuia kansa ya shingo ya kizazi na matiti.

**MRATIBU MAGONJWA**

Mratibu wa Magonjwa ya Saratani wa Halmashauri ya wilaya ya Hanang, Restituta Kavishe, anaweka bayana kuwa watoto wanaostahili kupatiwa chanjo ya ugonjwa huo ni watoto wenye umri wa miaka 14 kutokana na kundi hilo kuwa halijaanza kuwa na kasi ya kufanya mapenzi, hivyo inakuwa vyema kuanza kuwakinga.

"Kwa wilaya ya Hanang' hatuna wagonjwa wengi kwa hiyo siyo kila mwaka tunaweza kupata mgonjwa, kwa mfano mpaka sasa hatuna mgonjwa tangu tulipouanza mwaka 2022. Mfano kwa mwaka jana, tulikuwa na wagonjwa watano tu," anasisitiza Kavishe.

Kuhusu wataalamu wa magonjwa hayo waliopo katika halmashauri hiyo, Mratibu Restituta anafafanua kwamba licha ya halmashauri hiyo kuwa na vituo 38 vya kuhudumia, ni vitano pekee ndivyo vinavyodumia, kukiwapo uhaba wa wataalamu wa kuwafikia.

Restituta anatumia wasaa huo kuwaalika mabinti wenye umri miaka 14 kupatiwa chanjo dhidi ya maradhi hayo, pia wajiepushe na wapenzi wengi na endapo wakishindwa, wajizuie kwa kondomu.

Anasistiza njia nyingine ni ya kila mwanamke kujitokeza kupimwa afya na anapobainika, aanze kupatiwa matibabu haraka, huku akiwataka kinamama wa vijijini wasiruhusu mabinti zao kwenda machungani peke yao, kwani huendana na matukio ya kubakwa.

**WITO WA KISERIKALI**

Hivi karibuni kwenye hafla ya kuzindua Bodi mpya ya Wadhamini ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar es-Salaam, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliitaka bodi hiyo kusimamia ubora wa huduma za taasisi hiyo na kuweka mfumo bora wa kushughulikia malalamiko ya umma.

Mnamo Julai, 31 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, naye akatoa wito kwa taasisi za umma na binafsi, zishirikiane na serikali kupambana dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi, ili kuokoa maisha ya wanawake na kuepuka madhara yanayoambatana.

"Saratani ya shingo ya kizazi inatibika na inaweza kuepukika, endapo itatolewa elimu ya kutosha yenye lengo la kuwasisitiza wanawake kupima afya zao mara kwa mara, ili kupata tiba stahiki,"anasema Waziri Mkuu.

Majaliwa anasisitiza kuwa ni maradhi yayogharimu maisha ya wanawake nchini, kwani kwa mwaka uliopita wanawake wasiopungua 9,219 walifanyiwa uchunguzi na kati yao, 364 walikutwa na saratani ya matiti na ya shingo ya kizazi.

Vilevile, kati ya hao 364 walionekana kuwa na dalili za awali na wengine 26 waligundulika kuwa nayo. Hapo anaendeleza msisitizo wa kwamba serikali inaendeleza maboresho katika utoaji huduma za matibabu na uchunguzi wa kibingwa wa ugonjwa saratani.

AFYA

# Daktari Kinywa: Mtoto kuota meno sio chanzo cha homa na kuharisha



Mtoto katika umri wa kuota meno.

**Na Mary Geofrey**

HATUA ya kuota meno kwa watoto wakati mwingine huwa ni ngumu kwao wenyewe na wazazi wao. Ukuaji wa watoto hupitia hatua nyingi tangu kuzaliwa kwao na mabadiliko hayo huhusisha tabia na namna ambavyo mifumo ya mwili hufanya kazi.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Kinywa na Meno, Dk. Baraka Nzobo, akizungumza na Nipashe kuhusu hatua za watoto kuota meno na matatizo yanayowakabili, anasema watoto wadogo ni lazima kupitia hatua hiyo.

Anasimulia kuwa ukuaji watoto huwa haufanani, lakini wengi huanza na kuota meno wakiwa na umri kati ya miezi minne hadi saba au zaidi ya hapo kufika miaka miwili, ndio wanakamilisha meno yote ya utotoni yanaota.

**DALILI ZA KUOTA**

Dk. Nzobo anasema tofauti na jinsi ambavyo wazazi wengi huamini, tendo hilo la kiasili na kimaumbile, huwa sio chanzo cha kuhara au homa kwa mtoto.

Anasema dalili za kawaida za kuota meno kwa watoto ni kuvimba na kulainika kwa fizi, hasira na kulia, kuongezeka kidogo joto la mwili, lakini si zaidi ya nyuzi joto 38.

Daktari huyo anasema, pia mtu hulazimisha kula kila kitu kikohozi, kusugua fizi, kutoka mate mengi mdomoni, kung'ata na kuvuta chuchu wakati wa kunyonya na kupuliza mate mdomoni mara kwa mara.

Anasema, kuota kwa meno kunaweza pia kusababisha maumivu makali kwa mtoto kwenye fizi zake, lakini hakupaswi kuwa chanzo cha kuhara au kupata homa.

**KWANINI WANAHARA?**

Dk. Nzobo anasema, chanzo cha mtoto kuhara na kupata homa kipindi ambacho meno ya utotoni yanapoanza kuota husababishwa na mambo mengi.

Anasema, mara zote wazazi wengi wamekuwa wakiripoti kwamba watoto wao hupata homa na kuharisha wanapoanza kuota meno na anafafanua: "Hata hivyo dhana hiyo sio kweli.

'Ukweli ni kwamba kuota meno kunaweza kusababisha joto la mwili la mtoto kuongezeka lakini haisababishi homa. Homa ni joto la mwili kuwa zaidi ya nyuzi joto 38."

Pia, anafafanua kwamba katika kipindi hicho, mtoto anapokuwa na umri wa miezi minne hadi saba, meno yake huanza kuota mdomoni na ndiyo wakati ambao watoto wengi hujifunza na kuanza kutambaa.

Hivyo anasema, anapotambaa katika sehemu yenye uchafu, mikono yake inabeba wadudu wanaosababisha magonjwa ya kuharisha na ndio mwanzo wa mtoto kuhara, endapo ataingiza mikono mdomoni na mara tu vidole vyake vinaposugua fizi zinazo muwasha au kumkereketa.

"Kwa kuwa fizi zake zinakuwa zinawasha au zinakereketa kwa sababu ya meno kutaka kuchomoza mdomoni, mtoto huamua kujipa msaada wa kuondoa kero hizo kwa mbinu mbalimbali kama vile kuokota kitu chochote kilicho mbele yake na kukiweka mdomoni na kuking'atia kwenye fizi, ili kuondoa muwasho wa fizi hizo," anasema Dk. Nzobo.

Anasema, kwakuwa mtoto kila mara anaokota vitu visivyo visafi kwenye hali ya usafi, uwezekano wa mtoto kupata maambukizi ya vimelea vya magonjwa vitakavyomletea kuharisha na kupata homa mbalimbali mwilini mwake ni mkubwa.

"Ifahamike kuwa, wakati huu watoto huwa na hamu ya kula kila kitu pamoja na kusugua fizi zao maana huwasha, hivyo wanaweza kula uchafu wa aina mbalimbali ambao kwa mantiki nyepesi ndiyo huwafanya waanze kuhara," anasimulia mtaalamu Dk. Nzobo.

Anasema, katika umri huo mtoto wa meno kuanza kuota, watoto wengi huanza kupewa vyakula vingine tofauti na maziwa ya mama, hivyo kama chakula kisipoandaliwa katika mazingira safi, kinaweza kusababisha maambukizi ya vimelea vya magonjwa ya kuharisha hata kupata homa.

**MADHARA YA IMANI**

Dk. Nzobo anasema imani hiyo potofu ya homa ya meno imesababisha magonjwa mengi ya mfumo wa chakula kupuuzwa na kushindwa kutibiwa kwa wakati kwa sababu wazazi wengi wanaamini kwamba kuota kwa meno ndiyo kunasababisha mtoto kuhara.

Anasema, kwa mtoto mwenye dalili ya kuota meno endapo fizi zake zitaanza kuwasha na kumkereketa anatakiwa kusaidiwa badala ya kuachwa na kusababisha kupata homa na kuhara.

Kwa mujibu wa daktari huyo, pale mzazi anapotakiwa kuhakikisha mwanawe anacheza au kutambaa kwenye mazingira safi kipindi chote cha ukuaji wake, basi mzazi ana wajibu wa kuhakikisha ananawa mikono yake kwa sabuni na maji safi, kisha amsaidie kumsugua fizi zake kwa vidole visafi, ili kumpunguzia mtoto muwasho wa fizi.

Pia, anatoa mbinu mbadala ya kumpa mtoto kijiko kisafi akawa anaking'ata ng'ata, ili kumpunguzia muwasho au kukereketa kwa fizi zake.

**HATUA ZA KUCHUKUA**

Dk. Nzobo anashauri kwamba, mtoto anapokuwa na homa au kuharisha kipindi anachootа meno mdomoni, ni muhimu ampeleke kwenye kituo cha afya kilicho karibu, afanyiwe uchunguzi kubaini chanzo cha homa au kuharisha.

Anasema, ni muhimu kuzingatia ushauri huo kwa sababu ni wakati mwingine mtoto anaweza kuwa na ugonjwa unaoweza kuhatarisha maisha yake.



Mtoto anayetambaa, moja ya vyanzo vya kuharisha.



Ni umri wa mtoto fizi zinawasha.
**PICHA ZOTE: MAKTABA.**

MAZINGIRA

# NEMC yafanya tathmini bandari bubu na kubaini hali mbaya, uchafu umezidi

## •Yapendekeza orodha ya hatua kuchukuliwa

Na Joseph Mwendapole

KATIKA miundombinu ya kuchumi iliyoko kitaifa, mojawapo ni bandari ikipewa heshima kwa jina 'lango la biashara.'

Hata hivyo, mbali na kuwepo huduma hiyo rasmi, pia katika sura ya pili, zipo zisizoendana na uhalisia wa mahitaji hayo kwa maana ya kwamba, haziko rasmi.

Katika mazingira ya bandari hizo rasmi, bandari hujikita katika kuzingatia mazingira rasmi. Ofisa Mazingira Mwandamizi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Romanus Wilhad anasema hii ni kwa kuzingatia masuala yaliyoainishwa Taarifa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Brutland (1987).

Nukuu ya tume hiyo inatamka "maendeleo endelevu ni hali ya kutimiza mahitaji ya vizazi vya sasa bila kuathiri mahitaji ya vizazi vijavyo".

Ronmaus anasema, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), inatekeleza azma hiyo kwenye nyanja zake za maendeleo kwa kushirikiana na wadau husika.

Anasema, sekta ya uchukuzi nayo ina umuhimu kwa maendeleo ya nchi, ikijumuisha shughuli za bandari, chachu muhimu katika kukuza uchumi wa taifa na nchi za jirani.

Anasema shughuli zinazohusiana na bandari, husababisha changamoto mbalimbali za mazingira, ikiwemo kumwagika vimiminika hatarishi na taka ngumu kwenda baharini na maeneo ya pwani.

"Changamoto nyingine ni pamoja na hewa ukaa, moshi na vihatarishi vingine husababisha uchafuzi wa hewa ambayo ni hitaji la msingi kwa viumbe hai.

" Pia, bandari zinaweza kuwa vyanzo vya sauti zilizozidi viwango (kelele), hivyo kusababisha madhara kwa binadamu na viumbe wengine," anafafanua Romanus.

Anasema, masuala ya mazingira katika bandari yameendelea kusimamiwa na baraza kwa kushirikiana na idara husika, ili kuhakikisha mifumo ikolojia iliyopo inalindwa. Hata hivyo, anasema yapo maeneo yanayofanya shughuli za kibandari pasipo kuwa rasmi.

Kwa mujibu wa Romanus, NEMC imeshachukua hatua ya kutathimini, ili kubaini changamoto za kimazingira zinazotokana na uwepo wa bandari zisizokuwa rasmi maarufu Bandari Bubu.

Tathmini hiyo anataja ni kuwa na malengo mahsusi ya kubaini maeneo zilipo bandari bubu kwa kutumia mifumo ya kijiografia, kutathmini mifumo ikolojia inayozizunguka na kugundua shughuli mahsusi zinazofanyika katika kila bandari.

Pia, anataja athari za kimazingira kwa bandari hizo na NEMC inapendekeza hatua za kuchukuliwa, pamoja na kutoa elimu kwa wadau husika kuhusu kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.



Maji taka yakitiririshwa baharini katika bandari isiyokuwa rasmi ya Kunduchi jijini Dar es Salaam.

**KILICHOKUTWA**

Anasema tathmini hiyo ya NEMC, hufanywa na Baraza ilibaini kuwepo zaidi ya bandari zisizokuwa rasmi 693 nchi nzima na kwamba kutokana na bandari hizo kutokuwa rasmi, Baraza limekamilisha tathmini kwenye mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Mwanza.

Anasema bandari zilizokaguliwa zilibainika kuwa na changamoto za kimazingira kulingana na eneo bandari ilipo na shughuli zinazoendeshwa katika bandari hiyo.

Romanus anatoa mfano, baadhi ya bandari zilizofanyiwa tathmini zilibainika kuwa na uchafuzi mkubwa unaosababishwa na kutupa taka ngumu bila ya utaratibu kama vile chupa za plastiki, mifuko ya plastiki, masalia ya mbao na misumari ya kutengenezea vyombo vya majini na kinyesi cha binadamu.

Hapo kuna taka kama vile taulo za kike na nepi za watoto zilizobainika kutupwa kwenye fukwe na ukaguzi huo ulibainisha bandari kutokuwa na mifumo na miundombinu yenye kusaidia uhifadhi wa mazingira ikiwemo kutokuwepo na vyoo na vifaa vinavyokidhi mahitaji ya kuhifadhia taka.

Pia, anasema ilibainika kuwepo masalia ya vyakula na taka ngumu kutokana na shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo, mathalan migahawa isiyokuwa rasmi maarufu 'Mama Ntilie.' Migahawa hiyo inatajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa mazingira maeneo ya bandari.

Anasema, katika baadhi ya bandari, wadau wengi hutumia fukwe za bahari kujisaidia haja kubwa na ndogo, licha ya kuwepo vyoo vya kulipia katika bandari hizo.

Bandari nyingine zilizo karibu na mikoko, inatajwa kuwa chachu muhimu katika afya na uhai wa viumbe hai kwenye fukwe na bahari, ilibainika kuwa sehemu kubwa ya mikoko hiyo imeshakatwa kupisha miundombinu mbalimbali na ujenzi wa majengo.

"Kwa misingi hiyo, uendelezaji na urasimishaji wa baadhi ya bandari hizi utahitaji tathimini ya athari za mazingira ili kunusuru mikoko iliyopo kwenye maeneo hayo.

"Vilevile, kutokana na baadhi ya bandari kuwa na kina kifupi, taratibu za kiuhandisi zitalazimika kufanyika ili kuwezesha vyombo vya majini kutia nanga endapo bandari husika zitarasimishwa. Jambo hilo lisipo fanywa kwa umakini linaweza kusababisha uharibifu wa mazingira kwenye maeneo husika," anasema.

Katika bandari zisizo rasmi, mifumo ya majitaka pia sio ya kuridhisha kwani maji machafu kutoka sehemu kama sokoni na maeneo mengineyo hutiririshwa moja kwa moja kuelekea baharini.

Ukaguzi huo ulibainisha kuwa vyombo vya majini (uvuvi) vinavyohusika kwenye bandari hizi, mfano vya ukanda wa Bahari ya Hindi, ni vya kawaida ambavyo havihusishi meli kubwa zinazofikia maeneo haya. Hata hivyo, baadhi ya bandari zimeunganishwa kwenye mfumo wa jiji wa maji taka na kuwa na vifaa vya kuhifadhia taka ngumu, lakini taka hatarishi na chuma chakavu bado zinahitaji usimamizi imara zaidi kwani zinatupwa ovyo bila kuzingatia kanuni za mazingira na afya ya binadamu.

NEMC ilitumia fursa hiyo kuelimisha jamii ya waendeshaji wa bandari kuhusu matakwa ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na hatua zinazohitajika kuchukuliwa.

Pia, anasema kupitia vikao na mamlaka mbalimbali zinazohusika kama vile Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza lilipendekeza na kuelekeza kuwa endapo bandari husika zitarasimishwa, upembuzi yakinifu ufanyike ukiambatana na tathmini ya athari kwa mazingira.

Aidha, anasema mamlaka husika ziweke bayana maeneo mahususi ya kila bandari kwa kuweka mipaka au alama kwani kwa sasa maeneo hayo hayaoneshi mipaka ya maeneo ya bandari kwamba itasaidia uendeshaji wa bandari husika kutoingiliana na mifumo ikolojia kwenye mazingira katika kufanikisha azma ya serikali ya kuwa na maendeleo endelevu.



Shughuli za kibinadamu katika bandari isiyokuwa rasmi ya Kipumbwi, mkoani Tanga. **PICHA ZOTE: JOSEPH MWENDAPOLE.**

AFYA

# RC KATAVI: NGO ZIKO NYINGI, SIONI KUKABILI MIMBA...UCHAFU HUU JE?

- Awapasha 'madudu' waliyoyaficha ofisini
- Ofisa Ustawi Jamii aanika mazito yao
- Wenyewe wajitetea, wakiri udhaifu wao
- Awanyooshea kidole cha ukali 'ole wenu!'

**Na Neema Hussein, Katavi**

KATAVI ni mkoa uliojaliwa kuwa na rasilimali lukuki, kuanzia mvua za kutosha, ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo, ufugaji, hali kadhalika utajiri wa madini.

Ni eneo lenye mvuto hasa kiuchumi, hata kuwafanya baadhi ya wenyeji kutoka mikoa mingineyo kama vile wafugaji kutoka kanda ya Ziwa, kuhamishia huko shughuli zao za kiuchumi.

Lakini neema hiyo ambayo ni kichocheo cha maendeleo, inakwazwa na baadhi ya mambo ambayo ni hasi kwa maendeleo, ikiwemo kuwapo maradhi ya kifua kikuu katika namna ambayo haipendezi, hasa panapokuwapo kundi kubwa la wananchi wanaoamini katika waganga wa kienyeji.

Vilevile, kuna lingine la pili ambalo ni kilio katika sehemu nyingi nchini, suala la mimba kwa watoto na hasa waliopo shuleni, ikirudisha nyuma juhudi za serikali kupiga hatua kimaendeleo, vijana kufikia malengo yao

Hayo yote ni maeneo ambayo mwandishi wa makala hii alishawahi kuwasilisha kwa kina katika gazeti hili, ikiwa na ufafanuzi wa kimamlaka kutoka kwa wahusika na taarifa ya hali halisi iliyoko.

Mustakabali huo mpana na uhalisia wake, umeufanya mkoa huo ambao umeundwa baada ya kumegwa kutoka jirani Rukwa, kupata mashirika mengi yasiyo ya kiserikali kuhudumia kwa namna mbalimbali, mahitaji ya kijamii kila moja ikigusa eneo maalum.

Ni aina ya hatua inayoendana na sera, pia sheria iliyoko kushirikisha sekta binafsi na umma, katika kufanikisha maendeleo ya kisera kwa jamii, kiuchumi na hata kimaendeleo.



Mkuu wa Mkoa Katavi, Mwanamvua Mrindoko,akizungumza na wahusika wa asasi zisizo za kiserikali, mjini Mpanda.

### JICHO LA RC

Hata hivyo, kadri ninavyotathmini na kuweka uwiano kati ya idadi ya asasi zisizo za kiserikali kuhudumia mapungufu na mahitaji ya kijamii mkoani Katavi na matokeo chanya, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, anasema haridhiki.

Anafafanua kwamba pamoja na kuwepo kwa mashirika mengi yasiyo ya kiserikali ndani ya mkoa huo, anang'aka kwamba bado hajaona mchango unaojitosheleza wa mashirika hayo kupambana na suala la ukatili wa kijinsia, akiwa na tamko mahsusi katika maeneo kama mimba za utotoni, ubakaji na ulawiti.

Ni kauli ya Mkuu wa Mkoa Mrindoko, wakati alipofungua kikao cha mashirika hayo kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, huku akiyataka mashirika hayo kutimiza wajibu wao ili kupunguza tatizo hilo ndani ya mkoa wa Katavi.

Mkuu wa Mkoa, pia anayataka mashirika hayo kutotumika vibaya, hata wakaangukia mikononi mwa wanasiasa, akinyoosha kidole cha angalizo kwamba asasi hizo kutogeuka wakala kushiriki kuchochea mapenzi ya jinsia moja.

"Nimetaka kusikia mnafanya nini katika kila asasi? Sasa niendelee kuwasisitiza kwamba isitokee waziwazi wala na, isitokee chini ya kapeti kwamba umeandikisha NGO yako, kwamba inakwenda kujishughulisha na mazingira na kusaidia watoto kuondokana na ukatili, lakini kumbe chini ya kapeti unafanya mambo yako ya kisiasa yanayofanya amani kuvurugika.

"Hatutavumilia asasi yoyote au NGO yeyote ndani ya mkoa wa Katavi, ambavyo tutabaini kwamba inachochea uvunjifu wa maadili ya Kitanzania. Kuna kipindi tulipata taarifa kuwa zipo asasi ambazo zinachochea mapenzi ya jinsia moja.

"Lakini niseme tu kwamba, ukisikia mahali pengine kuna dalili hizo, basi usibweteke ukajua kwamba na kwako pataendelea kuwa shwari.

"Lazima, tuendelee kusema na nyie na kuwaonya, endapo tukibaini kama kuna NGO ya hivyo cha kwanza tutaifukuza katika mkoa wa Katavi iondoke iende ikafanye 'madudu' hayo maeneo mengine, lakini cha pili tutachukua hatua za kisheria na ndio maana nimetafuta sheria gani inawasimamia, Sheria namba 24 ya Mwaka 2002.

"Malengo ya NGO zenu ni kweli yanalenga kuigusa jamii ya rika mbalimbali, lakini kama mnavyofahamu bado matatizo yapo na kuna baadhi ya maeneo bado hatujaona mikono ya NGO ikiweza kuyatatua huko kwenye jamii.

"Kwa mfano, kuna swala la mimba za utotoni, bado mkoa wetu unakabiliwa na mimba za utotoni. Suala la kuacha masomo, kulawiti na kubaka, watoto kufanyishwa kazi za ndani biashara ya ngono," anasema Mrindoko.

### SAUTI ZA WAHUSIKA

Katika nasaha zake, mwakilishi wa asasi zisizokua za kiserikari mkoa wa Katavi, Eden Ezekiel, anasema malengo makubwa ya kikao hicho, ni kuongeza ushirikiano baina ya mashirika hayo na serikali.

Pia, akakiri kwamba asasi nyingi kujisajili kwa lengo la kutetea na kutatua changamoto zinazowakabili watoto, ila zimeshindwa kufanya kazi yao kutokana na changamoto ya ufinyu wa bajeti, pamoja na kukosa ushirikiano baina yao na serikali, ikiwemo halmashauri na uongozi wa vijiji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Katavi Willison Kennedy, anaainisha changamoto wanazokutana nazo kutoka katika asasi hizo zisizo za kiserikali ni kwamba baadhi zinakuwepo mkoani, ilhali hazitambuliki, wala shughuli zinazofanya.

Kennedy anakiri wamekutana na asasi ambazo zinahamasisha mapenzi ya jinsia moja na mambo yanayovunja haki za binadamu.



Washiriki wa kikao wakiwamo kutoka asasi zisizo za kiserikali wakiwa kikaoni na mkuu wa mkoa. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

AFYA

KUTOKA HOSPITALINI TEMEKE

# Dk. Kimaro: Wenye maradhi haya matatu ndio wanaotuelemea wodini




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipotembelea wodi za Hospitali ya Rufani Temeke.

**Na Pilly Kigome.**

JIJI la Dar es Salaam kwa sasa na hata kabla, linajulikana kwamba 'limeshiba' wakazi, tangu likiwa mji mkuu, lakini hata sasa katika hadhi ya jiji la biashara.

Katika sensa ya mwisho muongo mmoja uliopita, ilikuwa katika makadirio ya wastani wa wakazi milioni tano, sasa jibu jipya linasubiriwa kwa idadi ya wakazi wake, kupitia Sensa ya Watu na Makazi ya hivi karibuni.

Ni muda mrefu kabla ya kuchipua zahanati za sasa, vituo vya afya na hospitali jijini kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ulioanza mwaka 2008, wakazi wa Dar es Salaam, zaidi kwa hospitali ya kiserikali walitegemea Muhimbili kuhudumia wilaya zake pekee zama hizo; Temeke, Kinondoni na Ilala.

Kwa zahanati kuu zilikuwepo; Temeke, Mnazi Mmoja, Amana na Mwananyamala. Lakini, kwa marejeo hayo ya MMAM, mkongwe Mnazi Mmoja yenye umri wastani wa miaka 50, sasa inaungana na nyinginezo mpya kama Sinza na Kitunda.

Vivyo hivyo, Amana, Mwananyamala na Temeke, sasa ni hospitali za rufani, zikibeba hadhi ya kimkoa kila moja, kwa Dar es Salaam, ambayo sasa ina wilaya mpya za ziada Ubungo na Kigamboni. Je, hali ikoje katika hospitali hizo?

HALI YA TEMEKE

Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Joseph Kimaro, anataja kuwapo magonjwa matatu yanayosumbua zaidi kuwa na wagonjwa wengi; tatizo la upungufu wa damu, shinikizo la damu na maradhi ya kinamama.

Dk. Kimaro anaiambia Nipashe kwamba, tathimini ya robo mwaka inayoanzia Aprili hadi Juni mwaka huu, inaonyesha wagonjwa wanaopokelewa hospitalini hapo wengi zaidi ni wenye tatizo la upungufu wa damu (anaemia).

Hapo analiainisha tatizo hilo linajumuisha mchanganyiko wa jinsia wanawake na wanaume, pia umri wenye kupokewa na kulazwa, hali kadhalika kutibiwa na kurudi nyumbani wakiwemo watoto wadogo wenye umri chini ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa mganga huyo mfawidhi, takwimu zilizpo zinaonyesha kwa kipindi hicho, wagonjwa watu wazima waliopatikana na tatizo hilo la damu kuishia mwezi Juni iliyopita walikuwa 238 na watoto chini ya umri wa miaka mitano walikuwa 381.

Dk. Kimaro anasema, ugonjwa huo umeshika nafasi ya kwanza hospitalini hapo kwa wagonjwa wa ndani wanaolazwa, pia wagonjwa wa nje (OPD).

Pia, anataja mengine, ni magonjwa kama Selimundu (Sikosel) ambayo inahusu ukosefu wa damu, hali kadhalika maradhi ya kinamama(Menorrhagia) .

Anafafanua sababu kuu zinazochangia kasi ya kukua ugonjwa huo wa upungufu wa damu, inajumuisha lishe duni hasa kwa watu kutopata mlo wenye virutubisho kama vile madini ya chuma, ambayo mlo kama mboga za majani zina utajiri wake.

Pia, anaeleza kwamba watu wengi huugua minyoo aina ya 'hokworm' kwa muda mrefu, ni sababu ya ongezeko la ugonjwa huo wa upungufu wa damu, kwa kuwa minyoo hiyo ina tabia ya kutoboa utumbo na baadaye kupoteza damu.

Dk. Kimaro anataja sababu ya kumea wagonjwa wenye upungufu wa damu, inatokana na kukosekana virutubisho sahihi vya lishe unaotokana na namna ya ulaji vyakula ndani ya jamii.

Hapo ana maoni kwa serikali ichukue hatua za ziada kuelimisha jamii, kuanzia ngazi ya chini mahali jamii kwenye kata, kisha kupanda ngazi kufikia kitaifa, ili elimu hiyo iwe mtambuka kumfikia kila mtu.

Mtaalamu huyo anafafanua, mtazamo wa awali unaojitokeza kutoka kwenye jamii ni kwamba, kuna shida ya mwamko katika suala zima la mlo na makundi yake,wengi wanakariri baadhi ya makundi ya vyakula na kusahau ulaji wa makundi mengine, yanayoleta virutubisho sahihi mwilini.

Hatma ya kuondokana na upungufu wa yanayojiri, ni pale jamii itakapojitambua kikamilifu kuhusu umuhimu wa lishe, hali anayoamini itafuta wimbi la wagonjwa wenye upungufu wa damu mwilini, ambayo kwa kiasi kikubwa inatokana na lishe duni.

Darasa analotoa Dk. Kimaro, ni kwamba anawataka watu wabadilike wakiacha kula vyakula vya aina moja kila siku na wahamie kwenye virutubisho kwa vingi, ikiwemo ulaji mboga, matunda, dagaa na maharage, milo anayoipa sifa ni makundi muhimu katika mwili wa binadamu.

Anaendelea kufafanua umuhimu wa lishe muhimu mwilini, ikiwemo suala kuzuia magonjwa yatokanayo na upungufu wa virutubisho mwilini na hilo la upungufu wa damu.

Hapo ana maelezo kwamba, ipo haja ya kujikita kutoa elimu ya afya ihusuyo lishe kuanzia ngazi ya kata, ili kuweza kukabiliana na tatizo hasa hilo la upungufu wa damu.

Anasema, watu wengi wamekosa uelewa wa ulaji sahihi na akitolea mfano wa kula ugali aina ya sembe uliokobolewa na kusahau ukoboaji mahindi unakuwa unatoa vitamini muhimu.




Sehemu ya huduma za dharura hospitalini Temeke.

**INANDELEA UK. 20**

# Dk. Kimaro: Wenye maradhi haya matatu ndio wanaotuelemea wodini

INATOKA UK. 19

Pia, anataja suala la ulaji wa viazi mbatata vya kukaanga maarufu kama chips' imekuwa ni staili ya maisha ya watu wengi na wanaodhani wako katika ulaji sahihi, wakijikita zaidi kwenye mlo wa kundi hilo la chakula, kumbe ukweli wanakuwa wamekosea.

Dk. Kimaro anasema, kuugua minyoo kwa muda mrefu nalo kumeonekana kuwa sehemu ya yanayochangia kwenye tatizo la upungufu wa damu, kwa kuwa minyoo hiyo inatoboa utumbo na kuchangia mgonjwa kuvuja damu nyingi.

Hivyo, Dk. Kimaro ambaye pia ni mtaalamu wa afya, ana mapendekezo kwamba jamii inatakiwa kutumia dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu, ili kukabiliana na tatizo hilo, kwani linapokuwa kwa muda mrefu, linaangukia katika shida ya kupoteza damu mwilini.

**JUHUDI ZA KUJIHAMI**

Mnamo Julai mwaka huu, ilishuhudiwa Hospitali ya Rufani Temeke kwa kushirikiana na taasisi ya kijamii, ikiandaa kampeni maalum ya uchangiaji damu.

Ni kampeni ya taasisi ya kidini, ambayo imehusisha zaidi ya misikiti 100 ya wilayani Temeke na watu zaidi ya 350 wanatarajiwa kuchangia.

Mganga Mfawidhi Mkuu wa Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Joseph Kimaro, akisema ni kampeni ya kuendana na kuokoa maisha ya watu wengi,wakiwamo wanaojifungua na wanaopata ajali za barabarani na kuhitajika kuongezewa damu.

"Kila unit moja ya damu itakayochangiwa, itaweza kuokoa watu watatu, kwa hiyo tukiangalia kupitia kampeni hii zaidi ya watu 1000 wataokolewa," akanukuliwa mganga huyo alipokutana na waandishi wa habari kufafanua jambo hilo.

"Kwa hiyo, watu wote watakaopata nafasi waweze kuja kuunga mkono, zoezi hili kuhakikisha damu inapatikana kwa wingi, ili tuweze kuokoa 'wamama' wanaojifungua pamoja wanaopata ajali na wagonjwa wa upungufu wa damu," anasema Dk. Kimaro.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo ya kidini, Juma Said anasema, wameamua hata makusudi kuisaidia hospitali kuokoa makundi mbalimbali ya wahitaji wa damu.

"Damu haichagui dini, rangi, kabila wala Jinsia. Tunawakaribisha wote waweze kujitokeza ili kuokoa wenzetu. Pia, hata sisi ni wagonjwa watarajiwa," anasema Said.



Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Temeke, Dk. Joseph Kimaro.




Sehemu ya Majengo ya Hospitali ya Rufani Temeke.


## CHEMSHABONGO NA -00 3 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Mji mkuu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
5. Bandari kubwa Kenya
7. shauku
8. Bilionea aliyekuwa rais USA
10.husemwa mwisho wa sala na Wakristo
11.huitwa Kigogo wa Afrika
17.kubali wito 18.wajenzi wa nyumba kwa mawe

Chini:
1. shikwa
2. njiwa
3. kifaa cha kuonyesha muda
4. mkulima mkubwa wa mahindi duniani
6. mnyama wa damu baridi mdogo kuliko kenge
9. mwambao
12.alikwa 13.gea 14.ekari
15.peninsula
16.bara kubwa duniani





Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| KINAI | ANI |
| AMANA | ISHI |
| MAKOSA | AINIKA |
| MAKA | BIA |
| AMINI | GHANA |
| KANISA | UPANGA |
| ONA | MBUGA |
| SAIDIA | ABIRIA |
| DUMAZA | ASI |
| KAMBA | NYAKA |
| MAZAO | MBAO |
| KOMA | MAUA |
| AGANO | AU |

M A K O S A

Majibu toleo lililopita





S ■ U N G U A ■
H ■ MI A M B A
I ■ B A N I A ■
R ■ A ■ D A D A
I ■ ■ L ■ L ■ H ■ I ■
K U F I K I R I A ■ U
I M A N I ■ G
S A D I K I A
H ■ H ■ O ■ N
O ■ A ■ T ■ D
■ W A T A N Z A N I A

S A S A ■ R ■ K ■ B
A M A ■ M A S I K A
M A D I N I ■ N ■ O
A N A S A ■ N A I ■
D A K A R ■ A I L I
I ■ A K A R I ■ A ■
■ M ■ A ■ U R E N O
■ B ■ ■ O D A ■ I ■
F A T A K I ■ ■ ■ ■
■ O ■ ■ A A L I M U

maoni: 0755429240





## TEA yazitaka halmashauri kuanzisha mifuko

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Elimu nchini (TEA), imezitaka halmashauri zote nchini kuanzisha mifuko itakayosaidia kuondoa vikwazo vilivyoko maeneo yao kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara na wadau wengine.

Hatua hiyo imetajwa kusaidia kuboresha sekta ya elimu ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na maabara sambamba na vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

Alisema ushirikiano baina ya taasisi na wadau mbalimbali utasaidia kuboresha miundombinu ya elimu na kukuza sekta hiyo ambayo itachochea ufaulu kwa wanafunzi kwa kuwa watasoma kwenye mazingira mazuri yenye utulivu.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuze, alisema fedha nyingi zinatolewa na serikali kwa ajili ya kuboresha miundombinu kama vile ujenzi wa nyumba za walimu, mabweni na manunuzi ya vifaa vya kujifunzia na vya michezo.

"Katika mwaka wa fedha 2022/2023 TEA itatumia kiasi cha Sh. bilioni 8.9 kwa ajili ya ufadhili wa miundombinu na kwamba taasisi mbalimbali za kielimu zimenufaika na mamlaka hiyo katika kuboresha sekta ya elimu," alisema Geuze.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema TEA imesaidia uboreshaji wa miundombinu kwenye maeneo yao ambao umechangia kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Alisema mafanikio hayo ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa vyoo bora na vya kisasa pamoja na nyumba za walimu.

Baadhi ya shule zetu za msingi zilikuwa na mazingira mabaya ya kusomea, lakini baada ya mamlaka hiyo kutupatia fedha tuliweza kujenga vyumba vya madarasa na vyoo.

Alisema kwa sasa zaidi ya shule 10 za msingi wilayani Kyela zimefanyiwa marekebisho ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na vitabu vya kujisomea na kwamba na mategemeo yao ni kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

# Mbeya yakabiliwa unyanyasaji wa watoto wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unakabiliwa na tatizo la unyanyasaji wa watoto wenye ulemavu kufungiwa ndani licha ya baadhi yao kufikia umri wa kwenda shule.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu, Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, utafiti unaonesha baadhi ya watoto wanafungiwa ndani badala ya kuandikishwa shule kupata haki ya elimu.

Alisema tatizo hilo linashughulikiwa na mkoa umeandaa utaratibu kupitia kwa viongozi wa mitaa, vijiji kufanya msako wa nyumba kwa nyumba kuwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto shule.

Hatua hiyo alisema itasaidia watoto wenye ulemavu kwenda shule na kujifunza stadi mbalimbali za maisha na kutimiza ndoto zao kupitia elimu.

Katika kuhakikisha mkoa huo unatoa nafasi kwa watoto wenye ulemavu kupata nafasi ya kusoma kupitia programu ya elimu jumuishi shule za sekondari nne zimeteuliwa kuwa kwenye mradi huo.

Alisema shule za msingi 334 kati ya 811 za mkoa huo zimeingizwa kwenye programu ya elimu jumuishi zikiwamo za Mwenge, Kyela, Katumba ambazo zinawahusisha watoto wa kawaida na wenye ulemavu kusoma pamoja.

Baadhi ya wabunge wa Mkoa wa Mbeya wamesema miongoni mwa ajenda walizonazo kwa sasa ni kutoa elimu kwa wazazi kuhusu athari za kuwafungia watoto majumbani. Alisema elimu hiyo ina lengo la wazazi au walezi kutambua madhara ya kufanya vitendo hivyo kuwa ni sehemu ya unyanyasaji wa kijinsia na haikubali kwa mujibu wa sheria za haki za mtoto.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema ameanza kuwafikia wachimbaji wa madini kuachana na imani potofu kuwa wenye ualbino wanasaidia kupata madini mengi ya dhahabu kwa kutumia viungo vyao.

Mkurugenzi wa Shirika la Child Support Tanzania, linalojihusisha na kuwahadumia watoto wenye ulemavu kupitia programu yake ya Peleka Marafiki Zangu Shule, Noela Msuya, alisema mradi huo unalenga kuboresha mazingira rafiki na salama kwa watoto wa kitanzania kupitia mfumo wa elimu jumuishi.

Child Support Tanzania kupitia mradi wetu wa elimu jumuishi kwa sasa tumewahudumia watoto zaidi ya 600 kwa Mkoa wa Mbeya na kwamba malengo yetu kwa sasa ni kufikia maeneo yote nchini licha ya kuanza jitihada za kufika mikoa ya Rukwa, Mtwara na Kigoma.

Alisema shirika linaendelea kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu na zaidi ya watoto 100 wanahudumiwa kwa kuzingatia viwango na weledi unaotakiwa.

Mradi wa Peleka Rafiki Zangu wote shule, wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 226 unalenga kuwafikia watoto wengi zaidi kwenye mikoa ya Mbeya, Rukwa, Mwanza, Kigoma na Mtwara katika kipindi cha miezi mitano ijayo.




Mratibu wa Mradi wa EFLOWS, Dk. Winfred Mbungu (kushoto), akifafanua jambo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune (kulia), wakati wa mafunzo ya kimataifa ya kuwajengea uwezo wanasayansi, mameneja na wadau wengine namna ya kuendesha na kufanya tathmini ya maji kwa mazingira katika ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi, wilayani humo mkoani Mbeya juzi. Katikati ni Meneja Programu wa WIOMSA, Dk. Mathias Igulu. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# SUA yawajengea uwezo wanasayansi Bahari ya Hindi

**Na Ashton Balaigwa,** MBARALI

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Taasisi inayojishughulisha na Utafiti wa Utunzaji wa Bahari (WIOMSA), wameendesha mafunzo ya kimataifa ya kuwajengea uwezo wanasayansi, mameneja na wadau wengine jinsi ya kuendesha na kufanya tathmini ya maji kwa mazingira katika ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi.

Mafunzo hayo ya siku tano yamehusisha washiriki kutoka taasisi mbalimbali za utafiti katika sekta za maji, mazingira, misitu na washiriki wengine kutoka nchi za ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi, ikiwamo Afrika Kusini, Kenya, Mauritius, Msumbiji, Visiwa vya Shelisheli, Somalia, Visiwa vya Comoro, Madagascar na Visiwa vya Reunion ambao wameshiriki kwa njia ya mtandao. Akifungua mafunzo hayo wilayani Mbarali, Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliwataka wadau waliopata mafunzo hayo wanakwenda kuyafanyia kazi ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa ikiwamo utiririkaji wa majisafi na salama kwenye mito kuelekea baharini mwaka mzima.

"Wanaoishi ukanda wa juu wa mto unakoanzia wanatakiwa kujua fika shughuli za uharibifu wanazozifanya kule ndizo zinazoleta athari kwenye mabwawa ambayo yanajaa tope linalokwenda mpaka baharini na kuathiri viumbe vilivyomo katika mito, maziwa na bahari," alisema Mfune. Mfune aliipongeza SUA na WIOMSA kwa kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa yanaendana na kazi inayoendelea ya kurejesha afya ya mito na kupunguza madhara yanayotokana na uchafuzi wa mazingira.

Alisema zipo shughuli nyingi za kibinadamu zinazofanywa kwenye vyanzo vya maji na kandokando ya mito ikiwamo ukataji miti ovyo, ufugaji usiozingatia ukubwa wa eneo na kuwataka wananchi kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na serikali katika kusimamia sheria na kanuni zilizowekwa ili kuhifadhi mito na mazingira kwa faida ya kizazi hiki na kijacho.

"Sote tunajua umuhimu wa maji kwa taifa zima kama Bwawa la Nyerere ambalo linajengwa kwa gharama kubwa iwapo litashindwa kufanya kazi kutokana na ukosefu wa maji maana yake serikali itakuwa imepoteza fedha hizo bure," alisema Mfaune.

Akizungumzia mafunzo hayo Mtafiti Mkuu wa mradi huo kutoka SUA, Profesa Japhet Kashaigili, alisema lengo ni kujenga wataalamu na utaalamu wa kuweza kufanya tathmini ya maji kwa mazingira ili kusaidia wanapofanya uamuzi katika kugawana maji iwe kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Profesa Kashaigili alifafanua kuwa tathmini hiyo ya maji kwa mazingira itawezesha kuhusanisha madhara yanayotokana na shughuli mbalimbali zinazofanywa na kwa kiasi gani zinasababisha kuathiri ukanda wote wa bahari ili kujua chanzo cha tatizo lilipofikia, madhara na namna ya kutatua.

"Hii itasaidia nchi kutekeleza sera ya maji pamoja na Sheria ya Maji ya Mwaka 2009 ambayo imeainisha katika kugawana maji kwa vipaumbele ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mazingira na kwa shughuli nyingine, hivyo maji kwa ajili ya mazingira ilikuwa ni sehemu ambayo haina utaalamu na hakukuwa na jinsi ya kufanya hivyo bila kujenga utaalamu," alisema Profesa Kashaigili.

Meneja wa Programu WIOMSA ambao ndiyo wafadhili wa mafunzo hayo, Dk. Mathias Igulu, alisema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya bahari na mito, lakini jambo hilo halijaongelewa sana ndiyo wameona ni vyema kuanzisha mjadala na kuwaleta pamoja wanasayansi na wadau wengine kwa maslahi mapana ya uhifadhi wa bahari, mito na mazingira.

"Tunashirikiana SUA kwa kuwa tunajua wana wataalamu wabobevu kwenye masuala ya sayansi za kilimo, maji na mazingira, ufugaji wa samaki na sayansi zingine zinazoendana na hizo kuwaleta pamoja wadau muhimu nchini na nje ya Tanzania kwa kuwa wana uwezo mkubwa wa kusimamia," alisema Dk. Igulu.

Alisema masuala ya bahari na mito ni mambo yanayogusa maisha ya watu kila siku na ni suala la kiusalama pia maana jamii inahitaji kutumia maji katika kuzalisha, ni jambo muhimu na lazima liangaliwe kwa umakini kwa faida ya nchi zote zinazoguswa na mambo hayo.

Mmoja ya washiriki wa mafunzo hayo, Mtafiti Msaidizi kutoka Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi (TAFIRI), Wendo Lukwambe, alisema mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa kwao kwa kuwa yatawasaidia kujua jinsi mtiririko wa maji unavyoenda na namna ya kutunza maji kwa mazingira.



# Wabunge, watumishi 126 wahitimu mafunzo uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE na watumishi wa Bunge wanawake 126 wamehitimu mafunzo ya uongozi yaliyotolewa kupitia programu ya mwanamke kiongozi inayoratibiwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Mahafali hayo yalifanyika jana jijini hapo na wahitimu walitunukiwa vyeti vyao na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Programu hiyo ilitekelezwa kwa ushirikiano na serikali ya Norway na wadau wengine kikiwamo Chuo cha ESAMI.

Akizungumza katika mahafali hayo, Prof. Ndalichako alisema yana umuhimu na yataleta tija kutokana na tayari kuwa viongozi wa wananchi.

"Mwaka 2016 Rais Samia akiwa Makamu wa Rais alitoa rai kwa ATE kutoa mafunzo kwa wanawake viongozi na kuwa tangu alipotoa pendekezo hilo jumla ya wanawake 451 wameshapata mafunzo ya uongozi wakitokea katika sekta binafsi, wabunge wa Bunge la Jamhuri na Baraza la Wawakilishi," alisema.

Alifafanua kuwa Rais alielekeza ATE kuiomba Norway kutoa mafunzo kwa wabunge wanawake na watumishi wa umma na kuwa ndoto hiyo imetimia.

"Ninyi wabunge ni mfano kwa wananchi wenu kwa kutafuta maarifa zaidi kwani elimu haina mwisho, hasa kwa kuwa Rais wetu amekuwa pia na azma ya kuhakikisha usawa wa kijinsia katika uongozi," alisema.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba, alisema wametekeleza maagizo ya Rais kwa kutoa mafunzo hayo ambayo yanahusisha uongozi, utawala bora na uwezo wa kujenga hoja.

Pia alisema wanawake 274 kutoka taasisi mbalimbali wamepata mafunzo hayo na kufikia idadi ya 451.

Kwa upande wake, Balozi wa Denmark, Elisabeth Jacobsen, aliipongeza ATE na Shirikisho la Vyama vya Waajiri Norway (NHO) kwa kufanikisha mafunzo hayo na kuwa ni chachu katika masuala ya uongozi na jinsia.

"Mafunzo haya ya uongozi kwa wanawake ni uwekezaji mkubwa na kuwa ni muhimu katika usawa katika maamuzi mbalimbali na kutoa fursa kwa jinsia zote," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake nchini (TWPG), Shally Raymond, aliishukuru ATE na ubalozi wa Norway kuwezesha mafunzo hayo aliyoyaita kuwa ni mwanzo mzuri wa kuwajengea wanawake viongozi uwezo.



Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zuberi (wa nne kulia), akiongoza kuomba dua kwenye Msikiti wa Mucdam Changombe, jijini Dodoma juzi, unaojengwa ili uweze kukamilika kwa wakati. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Mufti awataka waumini kujenga tabia kujitolea

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE Mkuu wa Tanzania, Mufti Dk. Abubakar Zuberi Mbwana, amewataka waislamu kujenga tabia ya kujitolea fedha na mali zao kwa ajili ya kuendeleza mafanikio ya uislamu.

Mufti alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akiowaongoza viongozi mbalimbali wa dini ya kiislamu wa wilaya na kata wakiwamo mashekhe, maimamu na walimu wa madrasa kwenye dua ya kuombea msikiti wa Mucaddam wa Chang'ombe, jijini hapo.

Aliwataka waumini wa Kiislamu hapa nchini kuwa na tabia ya kupenda mafanikio ndani ya uislamu ikiwamo kujenga majengo mbalimbali kama misikiti na madrasa.

Hata hivyo, amewapongeza waumini wa msikiti huo kujitolea kwa mali na fedha na kufanikisha kujenga msikiti huo wa ghorofa mbili.

Alisema, juhudi zilizofanywa ni mfano mzuri wa kuigwa kwa waumini wengine ili kwenye maeneo yao wanayoishi waweze kujenga majengo ya misikiti kwa ajili ya maendeleo.

Awali, akitoa taarifa fupi ya ujenzi wa msikiti huo wa Muccadam wa Chang'ombe Jiji la Dodoma Mwenyekiti wa Baraza la Bakwata, Wilaya ya Dodoma, Bashir Hussen.

Alisema ujenzi huo ulianza kujengwa mwaka 2021 Septemba kwa juhudi za waumini wa msikiti huo na baadhi ya marafiki waliotoa michango yao ya mali na fedha.

"Msikiti wa hapo mwanzo ulikuwa na hali mbaya sana, lakini kutokana na kauli ya BAKWATA ile inayosema Jitambue, Badilika na acha Mazoea tumeifanyia kazi na sasa tumeweza kujenga msikiti huu wa ghorofa tatu kwa nguvu zetu," alisema.

**Hata hivyo, amewapongeza waumini wa msikiti huo kujitolea kwa mali na fedha na kufanikisha kujenga msikiti huo wa ghorofa mbili.**

# DC awaagiza maofisa elimu kukabiliana na utoro

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, amewataka Maofisa Elimu wa Kata kuweka mikakati ya kukabiliana na utoro shuleni kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili kuinua viwango vya mahudhurio na ufaulu.

Emmanuel aliyasema hayo wakati wa hafla ya kukabidhi vitabu vya mwongozo wa mikakati ya uboreshaji wa elimu, kwa Maofisa Elimu wa Kata, wakuu wa shule na walimu wakuu wilayani Kongwa.

Alisema anachukizwa na vitendo vya utoro kwa wanafunzi na kuielekeza halmashauri hiyo kupitia idara ya elimu msingi na sekondari kwa kushirikiana na viongozi wa kata na vijiji kusimamia vyema utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na utoro wa wanafunzi.

Alisema kumekuwa na tatizo la utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jambo linalohitaji mikakati ya kulikabili.

Alieleza kuwa halmashauri hiyo kupitia idara ya elimu msingi na sekondari kwa kushirikiana na viongozi wa kata na vijiji wanatakiwa kuhakikisha wanasimamia vyema utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na utoro.

Alifafanua zaidi ya kuwa mwongozo huo una mikakati muhimu ya kuboresha elimu katika nyanja zote na wakiutumia vizuri utasaidia kutatua tatizo la utoro na kero nyingine shuleni.

"Mikakati hii sio migeni jambo kubwa ni utekelezaji, nina imani kila jambo linawezekana kama kila mmoja wetu atakuwa na utayari, dhamira ya dhati kufanikisha mikakati hii."

"Kila mmoja akianza kuwa na matamanio na dhamira ya shule yake ifanye vizuri, lazima tutapiga hatua na kupata suluhisho sahihi, nafahamu zipo sababu za kila changamoto, lakini yote yanawezekana ikiwa tutaamua kwa dhamira na matamanio ya kuleta mabadiliko chanya," alisema.

Kadhalika, alisema ni muhimu kujifunza kwa wanaofanikiwa, mtu yeyote asione aibu kufanya hivyo, na kusisitiza kuhusu mahusiano mema na kuheshimiana katika kazi kama nguzo muhimu na kuongeza yeye tayari amefungua milango kwa kila mwana Kongwa na hata watumishi wote kumfikia kwa jambo lolote lenye tija na ustawi wa wilaya hiyo na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari Sudi Abdul, akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi wa halmashauri hiyo, alisema wamejipanga vyema kutekeleza mikakati ya kuboresha elimu wilayani humo na kuahidi kutekeleza maelekezo ya Mkuu wa Wilaya hiyo.





## Kisiwa Mnemba chakabiliwa mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kisiwa cha Mnemba kilichoko Mkoa wa Kaskazini Unguja kinakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya pembezoni mwa fukwe.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya kisiwa cha Mnemba ambacho kimewekezwa na mwekezaji kutoka Afrika Kusini.

Alisema Serikali ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za kufanya makubaliano na kampuni iliyowekeza kisiwa hicho mkataba wake ambao utazingatia masuala ya hifadhi ya mazingira kwa ajili ya kukiokowa kisiwa hicho kimazingira.

Aliitaja mikakati hiyo ni pamoja na kuweka masharti kwa watalii wanaotembelea maeneo hayo kuhakikisha wanatunza mazingira na kuepuka kufanya utalii unaoharibu mazingira.

Aidha, kwa upande wa wavuvi wametakiwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na kuepuka uvuvi unaotishia uhai wa maliasili za baharini ikiwamo matumbawe.

Alisema baadhi ya tozo zinatarajiwa kuongezwa ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuhakikisha kisiwa hicho kinalindwa na hifadhi ya mazingira.

Pia wamiliki wa hoteli hiyo wamekubali kutenga jumla ya Dola za Kimarekani 600,000 kwa ajili ya kujenga kingo za ukuta kuzuia kasi ya maji pamoja na athari za mmomonyoko wa ardhi na fukwe.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu... tayari tumekubaliana na mwekezaji aliyekodi kisiwa hicho kuhusu mikakati ya kulinda mazingira ya baharini kwa watalii wanaotembelea kisiwa hicho ikiwamo kuepuka uvuvi haramu ikiwamo wa kuzamia majini na kuharibu matumbawe," alisema.

Kisiwa cha Mnemba kilikodishwa kwa mwekezaji kutoka Afrika Kusini, mwaka 1992 na kwa sasa serikali inakusudia kuanza kufanya mazungumzo mwezi ujao ikiwamo kupitia mkataba huo na kuangalia masuala ya uhifadhi wa mazingira ikiwa ni njia ya kukihami.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira nchini yapo zaidi ya maeneo 150 yameathirika na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo baadhi ya visiwa vidogo vilivyoko Unguja na Pemba na baadhi ya wakazi wake wameanza kuvihama.

# Serikali kuelimisha wananchi umuhimu wa kutoa ushahidi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutoa ushahidi mahakamani kwa hiari ili kutoa nafasi kesi kusikilizwa na kutolewa hukumu.

Alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake, Mwanajuma Kassim Makame, aliyetaka kujua mahakama inatumia utaratibu gani kuhakikisha wananchi wanatoa ushahidi kwa kesi zinazowakabili ikiwamo za udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema kuna tatizo kubwa la wananchi kukataa kutoa ushahidi mahakamani na matokeo yake kesi hizo kushindwa kusikilizwa kwa kukosa ushahidi.

Alisema utaratibu wa kuwaelimisha wananchi ni mzuri ambao utafanikisha kusikilizwa kesi hizo na kutolewa maamuzi yake kwa mujibu wa sheria.

"Mheshimiwa Naibu Spika Mahakama zetu tutaendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhusu umuhimu wa kutoa ushahidi katika kesi mbalimbali ikiwamo za udhalilishaji wa kijinsia ili haki itendeke," alisema.

Alisema Serikali ya Zanzibar itaendelea na mikakati yake ya kuhakikisha kesi za udhalilishaji wa kijinsia zinasikilizwa kwa haraka na kutolewa hukumu zake kwa mujibu wa sheria.

Alizitaja juhudi hizo ikiwamo za kuongeza idadi ya majaji na mahakimu ambao kwa kiasi kikubwa wataongeza kasi ya kusikiliza kesi hizo kwa wakati.

"Mheshimiwa Spika tumeongeza idadi ya majaji na mahakimu ambao kwa kiasi kikubwa tunaamini kesi za udhalilishaji wa kijinsia zitasikilizwa kwa wakati katika kipindi kifupi," alisema.




Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakifuatilia kikao cha baraza hilo, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bil. 537/- kujenga barabara za njia nne Unguja, Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

KIASI cha Sh. 537,829,626,400.00, kitatumika katika ujenzi wa barabara tatu Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 103.5 unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mradi huo utatekelezwa na kampuni ya PROPAV UK kwa kushirikiana na kampuni ya ujenzi MECCO ya Tanzania ukifadhiliwa na Serikali ya Uingereza kupitia UKEF United Kingdom Export Finance.

Kampuni hizo zimeshatiliana saini mkataba na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Zanzibar.

Katika hafla hiyo iliyofanyika juzi Kisauni Zanzibar, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab, alisaini kwa niaba ya SMZ wakati kampuni ya PROPAV iliwakilishwa na Mkurugenzi wake wa Miundombinu, Leandro Motta, pamoja na Nasser Sheikh, Mkurugenzi wa MECCO.

Barabara zitakazohusika na ujenzi huo ni Mkoani-Chake Chake, Pemba yenye urefu wa kilomita 43.5 na Unguja ni Tunguu-Makunduchi (Km. 48) na Kisauni-Fumba (Km. 12).

Barabara hizo zitakuwa mbili kwa nne (four lane), kila moja itakuwa na uwezo wa kupita gari mbili zinazokwenda mwelekeo mmoja, taa na njia za waendao kwa miguu na taasisi nyingine zitahusishwa kulingana na miundombinu itakayohitajika.

Akitoa mchanganuo wa mradi huo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema hatua hiyo imekuja baada ya safari ndefu ya mashauriano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na makandarasi kuhusu upatikanaji fedha.

"Tumeanza mbali na tumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwani hapa tulipofika ni matokeo ya jitihada zao kubwa kutaka kufanikisha jambo hili la maendeleo, wametupa miongozo mizuri na msaada mkubwa kuhakikisha fedha zinapatikana," alibainisha.

Aliwashukuru wanasheria wa serikali hizo kwa ushirikiano wao na maoni mazuri yaliyochangia kukamilika kwa mchakato wote na hatimaye kusaini makubaliano ya ujenzi wa barabara hizo zitakazojengwa kwa kiwango cha kisasa.

Alisema Serikali ya Zanzibar na PROPAV zilianza kusaini mkataba wa maelewano Julai 19, 2021, na mkandarasi huyo alikuwa na jukumu la kutafuta fedha, huku SMZ ikiwajibika kuwapa taarifa muhimu zinazohusiana na kazi hiyo kubwa.

"Baada ya hapo, PROPAV walilazimika kuzungumza na Serikali ya Uingereza kwa kushirikiana na Wizara za Fedha Zanzibar na Tanzania ili kutafuta fedha hizo hadi tukafanikiwa," alieleza.

Alizishukuru wizara hizo pamoja na anayoiongoza kwa jitihada na ushirikiano wao uliolenga kufanikisha jambo hilo na hatimaye kusaini mkataba wa ujenzi.

Aliwataka wananchi watakaopitiwa na ujenzi huo kutoa ushirikiano na kuvumilia harakati zinazoweza kupangua shughuli na maeneo yao, huku akiwahakikishia serikali inafanya tathmini na kusema haitamuacha mtu anayestahili bila kulipwa fidia kwa usahihi kwa nyumba na vipando vitakavyoondolewa kupisha mradi huo.

Mkurugenzi wa Miundombinu katika Kampuni ya PROPAV Leandro Motta, ameishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi na Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwaamini.

"Hii ni heshima kubwa kwetu, na tunaahidi kufanya kazi hii kwa viwango bora kama tulivyokubaliana, tukielewa ujenzi huu ni muhimu kwa kuifungua Zanzibar na kuwaunganisha wananchi wake katika harakati za kiuchumi na kijamii," alisema.

Aliwatoa wasiwasi wananchi wa Zanzibar kuwa kampuni yake ina uzoefu wa miradi mikubwa na kuikamilisha kwa wakati, huku akimtaja mshirika wao MECCO kwa uwezo wake ambaye tayari imejenga barabara kadhaa Unguja na Pemba kwa kiwango kizuri.

Wakuu wa mikoa ya Kusini na Mjini Magharibi, Rashid Hadidi Rashid na Idrissa Kitwana Mustafa, ambao mikoa yao itapitiwa na ujenzi huo, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Mawasiliano na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Yahya Rashid Abdalla, wameishukuru serikali kuwa mradi huo utapendezesha miji na kuvutia uwekezaji.

Waliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa wajenzi na kuwasihi wafanyakazi watakaofanya kazi hiyo kujiepusha na vitendo vya wizi wa vifaa ikiwamo mafuta vinavyoweza kuzorotesha ujenzi huo.



HABARI KANDA YA ZIWA

## Halmashauri yatenga mil.147/- kwa wenye ulemavu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Sh. milioni 147.8 kwa ajili ya utoaji wa mikopo isiyokuwa na riba kwa watu wenye ulemavu ili kukuza mitaji yao.

Lengo la mikopo hiyo ni kuliwezesha kundi hilo kujikwamua kiuchumi na kuondokana na utegemezi ndani ya familia na jamii wanazotoka.

Fedha hizo zimetengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ambazo zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri ambayo ni asilimia 10 kwa mwaka.

Aidha, halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha uliopita ilifanikiwa kutoa mikopo isiyokuwa na riba ya Sh. milioni 64.2 kwa vikundi 20 vya watu wenye ulemavu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa hiyo, Robert Kwela aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake namna wanavyotoa mikopo kwa wajasiriamali hususani wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kuwasimamia na kuhakikisha wanaongeza mitaji yao.

Alisema mwaka wa fedha 2020/2021 walivipatia vikundi vinane mkopo wa Sh. milioni 44.215 na vilifanikiwa kurejesha Sh. milioni 13.470.

Vikundi hivyo bado vinadaiwa Sh. milioni 30.745 na kwamba mwaka huu wa fedha 2022/2023 wanaendelea kupokea maombi mbalimbali ya mikopo kwa makundi hayo.

"Tumekuwa tukitenga fedha kupitia mapato yetu ya ndani kila mwaka kwa ajili ya wajasiriamali wetu, tumetoa mikopo ya Sh. milioni 64.215 kwa vikundi 20 vya watu wenye ulemavu kuanzia mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021, vimerejesha Sh. milioni 24.361 na vimebakiza Sh. milioni 36.854," alisema Kwela.

Kwa upande wake, Katibu wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu wilayani Kahama (SHIVYWATA), Zawadi Masoud, alisema mikopo inayotolewa na halmashauri imesaidia kuwakwamua kiuchumi kwa kuongeza mitaji kwenye biashara zao.

Alisema mwaka jana wenye ulemavu wa kusikia walipata mkopo wa Sh.milioni 25 ambazo waliziwekeza kwenye biashara zao na sasa wanaendelea na marejesho.

# Wauzaji samaki sokoni wawatoa hofu walaji

**Na Virus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wachuuzi wa samaki katika Soko la Mirongo jijini Mwanza, wamesema kitoweo wanachouza kwa wateja wao hakigandishwi kwenye barafu kwa kutumia dawa ambazo zinadaiwa kusababisha saratani.

Wamesema samaki wanaouza wanatoka ziwani moja kwa moja na kwamba wanahakikisha hawajakaa katika majokofu ya kuhifadhia bidhaa hiyo.

Kauli hiyo imetolewa jana jijini Mwanza na wachuuzi hao siku chache baada ya Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango kubainisha kuwa chanzo cha wakazi wa mikoa ya kanda ya ziwa kuugua saratani ni matokeo ya kula samaki wanaohifadhiwa kwa kutumia maji ya kuoshea maiti.

Nipashe ilitembelea wachuuzi hao katika mwalo wa Mswahili na Soko Kuu la Mwanza la Mirongo na kuzungumza nao ili kujua njia wanazotumia kuhifadhi samaki wanaobaki.

Wachuuzi hao walisema samaki wanaoliwa katika maeneo mbalimbali mkoani Mwanza ni wazima kwa kuwa wanavuliwa siku hiyo hiyo kutoka ziwani na siyo wale wanaohifadhiwa katika majokofu.

Mwanaisha Juma (40) ni mchuuzi wa samaki kutoka katika mwalo wa Mswahili alieleza kuwa idadi kubwa ya samaki hupatikana mida ya asubuhi na jioni na huuzwa mpaka wanaisha.

"Mimi nachukua samaki hapa Mswahili mwaloni majira ya asubuhi na jioni kama unavyoona nina samaki wangu nauza katika Soko la Mkuyuni na uhakikisha samaki hawa wanaisha na hatuna friji za kutunzia, " alisema.

Hellen Moses ambaye ni mchuuzi kutoka katika Soko Kuu Mirongo alieleza Nipashe kuwa idadi kubwa ya wakazi wa Mwanza hununua samaki wa siku hiyo hiyo kutoka soko hilo.

Hellen alieleza kuwa wanauza samaki kwa wamiliki wa hoteli kubwa mkoani humo kulingana na mahitaji yao, hivyo kuwafanya wauze kitoweo hicho asubuhi na jioni ili kukidhi mahitaji ya wateja wao.

"Samaki wetu tunawachukua katika mialo mbalimbali ikiwamo Bwiru, Kigoto na Mswahili na wananunua kulingana na mahitaji ya wateja wetu na hatuhifadhi samaki wetu katika friji," alieleza.

Hellen alipoulizwa kuhusu jinsi wanavyohifadhi samaki hao endapo wakikosa wateja, alieleza kuwa idadi ya samaki wanaobaki ni kidogo na wanawakaanga kwenye mafuta ili waweze kuwauza kesho yake.

Mwenyekiti wa Wavuvi katika mwalo wa Mswahili, Robert Mussa, alipoulizwa juu ya uvuvi kuhusishwa na matumizi ya maji ya maiti alieleza kuwa kazi yao ni kutoa samaki ziwani mengine wao hawajui.

Alisema: "Sisi kazi yetu ni kutega samaki na dagaa tukiishawafikisha nchi kavu hatuhusiki nao tena hivyo matumizi ya hayo maji yanayohusishwa sisi hatujui chochote," alisema Robert.



Wachuuzi wa samaki aina ya sato na sangara, wakisubiri wateja katika soko kuu la Mirongo, jijini Mwanza jana. Samaki mmoja anauzwa kwa bei ya 5,000/- hadi 8,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Polisi yabaini ukatili wanaofanyiwa watoto usiku

**Elizabert Seleman,** SENGEREMA

JESHI la Polisi katika Kata ya Nyampulukano wilayani Sengerema mkoani Mwanza limebaini idadi kubwa ya watoto wasiokuwa na makazi wanaokula vyakula vya majalalani na kulala katika nyumba ambazo hazijaisha 'mapagara' kwa kila siku.

Kutokana na mtindo huo wa maisha ya watoto hao, wanadaiwa kulawitiwa nyakati za usiku na watu wasiojulikana kutokana na kulala nje ama kwenye nyumba ambazo hazijaisha.

Polisi jamii katika Kata ya Nyampulukano wilayani Sengerema mkoani Mwanza, limesema walibaini watoto hao baada ya kufanya msako wa wahalifu katika eneo hilo.

Polisi Jamii katika kata hiyo, Joyce Pastory alisema katika msako huo wa usiku walibaini watoto hao wakiwa wamelala kwenye mazingira magumu.

Alisema katika msako huo walibaini baadhi ya watoto hao kulawitiwa na watu wasiojulikana nyakati za usiku, huku akiwaomba wazazi na walezi kuchukua majukumu ya malezi ili kunusuru kundi hilo.

Watoto hao wanadaiwa kuwa na umri wa kati ya miaka nane hadi 12 na wengi wamekimbia kutoka katika mikono ya wazazi pamoja na walezi wao.

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Kituo cha Afya cha Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Ester Masolwa aliwaonya wazazi na walezi wanaowafanyia watoto wao vitendo vya ukatili na kusababisha kukimbia familia zao.

Alisema kama wazazi na walezi watakaa na kuzungumza na watoto hao pamoja na kutimiza wajibu wao hakutakuwa na tatizo hilo kama ilivyo kwa sasa.

HABARI KIMATAIFA

# Ethiopia yaipinga ripoti Umoja wa Mataifa

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

SERIKALI ya Ethiopia imepinga vikali ripoti ya Tume ya Umoja wa Mataifa, na kuielezea kuwa taarifa hiyo siyo kamili, haina misingi, uthibitisho na inalenga kuihujumu nchi hiyo.

Tume inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa Jumanne iliangazia kile ilichokiita taarifa za kuaminika za mauaji makubwa yaliyofanywa na jeshi la ulinzi la taifa la Ethiopia.

"Serikali inajutia njia ya haraka, isiyo na viwango, na inayoendeshwa na ajenda iliyochagua kutekeleza wajibu wake," ilisema ripoti hiyo.

Serikali ilijitetea ikisema imewafikisha wahusika wa ukiukaji wa haki za binadamu mbele ya sheria.

Serikali ya shirikisho na vikosi vya waasi vya Tigray vimeshutumu kila mmoja kwa ukiukaji wa haki za binadamu huku vita katika eneo la kaskazini la Tigray vikiendelea. **BBC**

# Tshisekedi aituhumu Rwanda kuivamia Congo DRC

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, amehutubia hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa, na kuituhumu Rwanda kuishambulia moja kwa moja nchi yake.

Kiongozi huyo, alisema licha ya nia njema ya serikali yake na mkono wa amani ulionyooshwa na raia wa Kongo, shukrani ya baadhi ya majirani imekuwa kuunga mkono makundi ya waasi mashariki mwa DRC.

Tshisekedi ameitaja kwa jina Rwanda, akidai iliwaingiza wanajeshi wake ndani ya eneo la Kongo mwezi Machi, kwa kukiuka sheria za kimataifa na mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Aidha, rais huyo wa DRC aliituhumu Rwanda kuwasaidia waasi wa M23 katika kuiangusha helikopta ya walinzi wa amani wa Umoja wa Mataifa, tukio lililosababisha vifo vya watu wanane.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa ambayo shirika la habari la AFP liliona nakala yake, ilisema jeshi la Rwanda liliingilia kati dhidi ya ngome za jeshi la DRC kuanzia Novemba mwaka jana hadi Juni mwaka huu. **DW**

# Russia yawaita wanajeshi akiba, yajiandaa na mapigano makali

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladmir Putin amesaini amri ya kuwahamasisha raia kujiunga na jeshi wakati nchi hiyo ikiendelea kupambana katika uwanja wa vita nchini Ukraine.

Putin alisema atatumia kila njia kulinda ardhi na watu wake.

Kiongozi huyo ameamuru uhamasishaji huo wa kwanza wa kijeshi nchini humo tangu Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Katika hotuba yake katika televisheni jana asubuhi, alisema wanajeshi wa ziada wanahitajika ili kushinda vita siyo tu dhidi ya Ukraine, lakini waungaji mkono wake wa mataifa ya magharibi.

Hatua hiyo inaonekana kama kukiri kwa Putin kwamba vita vyake vya uvamizi haviendi kama ilivyopangwa, baada ya karibu miezi saba ya mapigano.

"Ili kulinda nchi yetu, mamlaka yake na uhuru wa mipaka yake, ili kuhakikisha usalama wa taifa letu na watu katika maeneo yaliyokombolewa, nimeona ni muhimu kuunga mkono mapendekezo ya wizara ya ulinzi na mkuu wa majeshi kufanya uhamasishaji wa sehemu nchini Russia," alisema Putin.

Amri ya rais iliyochapishwa kwenye tovuti ya Ikulu ya Kremlin, ilisema wito huo utawahusu watu wenye uzoefu wa kijeshi.

Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergei Shoigu alisema wanajeshi wa akiba 300,000 watakusanywa ili kulipiga tafu jeshi katika kampeni yake nchini Ukraine.

**RUSSIA YAREKEBISHA IDADI YA VIFO VITANI**

Russia pia imefanya marekebisho ya kwanza ya idadi ya vifo katika kipindi cha karibu miezi sita.

Shoigu alisema wanajeshi 5,397 wa Russia wameuawa tangu kuanza kwa mzozo huo, huku akikanusha madai ya Ukraine na mataifa ya magharibi kwamba imepata hasara kubwa katika kampeni yake hiyo ya uvamizi iliodumu kwa miezi saba sasa.

Waziri Shoigu alisema asilimia 90 wanajeshi waliojeruhiwa wamerudi kwenye uwanja wa mapambano.

Hii ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Russia kutoa idadi rasmi ya vifo tangu Machi 25, ilipoosema wanajeshi 1,351 walikuwa wamekufa.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani Pentagon ilisema mnano Agosti kwamba inaamini wanajeshi wa Russia kati ya 70,000 na 80,000 wameuawa au kujeruhiwa vitani, na Julai ilikadiria idadi ya vifo vya Warusi kuwa 15,000.

Shoigu alisema Russia ina watu milioni 25 wanaoweza kupigana.

Tangazo la Putin limekuja katikati mwa mkutano wa Baraza kuu la Umoja wa Mataifa mjini New York, ambako uvamizi dhidi ya Ukraine unajadiliwa.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy amehutubia baraza hilo katika ujumbe uliorekodiwa.

Hata hivyo, Rais Putin hakwenda New York.

Waziri wa Ulinzi wa Uingereza Ben Wallace alielezea uhamasishaji huo kama kukiri kwa Putin kwamba uvamizi wake unashindwa.

**PAPA FRANCIS AIOMBEA UKRAINE**

Kiongozi wa Kanisa la Katoliki Duniani, Papa Francis amezungumzia mzozo wa Russia na Ukraine akisema raia wa nchi hiyo wanakabiliwa na ukatili, unyama na mateso.

Bila kuitaja Russia, Papa aliwaambia wasikilizaji wake kwa ujumla katika uwanja wa Mt. Peter kwamba Waukraine ni watu wa maadili wasio na kosa wanaouawa.

Pia alizungumza kuhusu mazungumzo aliyofanya na Kadinali Konrad Krajewski, mkuu wake wa shirika la kutoa misaada nchini Ukraine.

Vyombo vya habari vya Vatikani vilisema Krajewski, ambaye ni raia wa Poland, alipigwa risasi na watu wengine wiki iliyopita alipokuwa akitoa msaada.

**DW**



Mwonekano wa daraja la Gaoliao lilivyovunjika baada ya kutokea tetemeko la ardhi lenye ukubwa wa 6.8 katika mji wa Yuli kisiwa cha Taiwan juzi. **PICHA: EPA-EFE**

# Sall ataka kuondolewa vikwazo Zimbabwe

**NEWYORK,** Marekani

MWENYEKITI wa Umoja wa Afrika (AU) ambaye Rais wa Senegal, Macky Sall ametoa wito wa kuondolewa vikwazo dhidi ya Zimbabwe.

Wito huo aliutoa jana wakati akihutubia mkutano mkuu wa 77 wa Umoja wa Mataifa mjini New York.

Kiongozi huyo wa Senegal, alisema hatua kali dhidi ya Zimbabwe zinazidisha mateso ya watu.

Sall alikuwa kiongozi wa kwanza wa Afrika kuhutubia Baraza Kuu.

Alilitaka Baraza la Usalama kushughulikia mizozo barani Afrika kwa njia sawa na kushughulikia mizozo mingine.

Pia alitoa wito wa mageuzi katika baraza hilo ambayo yatalifanya kuwa shirikisho zaidi na pengine kuipa Afrika kiti cha kudumu.

Sall pia alitoa wito kwa Afrika kupewa kiti katika kundi la G20, linalojumuisha viongozi wa mataifa 20 makubwa kiuchumi duniani.

Viongozi zaidi wa Afrika wanatarajiwa kuhutubia mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa jana katika siku ya pili ya mjadala huo wa ngazi ya juu.

**BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CALVIN HUMPHREY MASSAWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **Ns. 1792/0017/2016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TRUST. ST. PATRICK SCHOOL** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CHU/RB/356353/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALFATERESIA PETER MWASANGAMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0248-0537** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MARIAN GIRLS' HIGH SCHOOL** mwaka **2017.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/374829/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MARIAM MKAMBA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma ; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0526-0034** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MRINGA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2002**, cheti cha kurisiti cha kidato cha nne chenye index namba **P.0377-0241** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LUGALO JWTZ** mwaka **2004** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0738-0518** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **RIDHWAA SEMINARY SECONDARY SCHOOL** mwaka **2007.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:MBI/RB/2003/2015**

## KUPOTEA KWA VYETI



**UPENDO DUNFORD KACHENGA** anatangaza kupotelewa na vyeti, cha kidato cha nne chenye index namba **S0234-0035** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya **ST.LUISE MBINGA GIRLS SECONDARY** mwaka **2012,** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1187-0699** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya **ST.MARY GORETI SECONDARY** mwaka **2015.**

Taarifa ya polisi **IRI/IRI/RB/331110/2022.**

## KAMPUNI YA ESSENCE BAKERY COMPANY LTD

Uongozi wa Kampuni ya **ESSENCE BAKERY COMPANY LTD** yenye TIN number **152-449-844** iliyopo Plot namba, Block namba, Street Tegeta – Madale iliyosajiliwa mwaka 2021 umeamua kuifunga Kampuni hiyo ambayo kwa sasa haifanyi shughuli zozote.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI Na 69/....2022**
**JINA LA MDAI: MENGI LUSEGA LUBUWA**
**JINA LA MDAIWA: FESTO LITEREKO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:FESTO LITEREKOI...............MDAIWA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya pesa kiasi cha sh.4,066,000/=.Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 30/09/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20/09/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI Na278/....2022**
**JINA LA MDAI: MENGI LUSEGA LUBUWA**
**JINA LA MDAIWA: RICHARD MSHANDETE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:RICHARD MSHANDETE................MDAIWA**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya pesa**

Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 30/09/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO**:Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20/09/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......48/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SAFIA MOHAMED MSASA WA K/NDEGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA HUSNA AMIR MPONDA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 09 mwaka 2022**

HAKIMU
MOROGORO

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF TEMEKE**
**FORM No. 58**
**DISTRICT AT TEMEKE AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 795 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**FESTO EDWARD SANGA**
**BY 1. REMIA ELI WAINGA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above -named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of SEPTEMBER.........2022

Dated at DAR ES SALAAM this 29 day of AUGUST...2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

**RESIDENT MAGISTRATE**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI

# KHLOÉ KARDASHIAN ATARAJIA MTOTO WA PILI NA X WAKE



**LOS ANGELES, Marekani**

TANGAZO jipya la msimu wa pili wa The Kardashians litamtazama kwa mara ya kwanza, Khloé Kardashian akithibitisha kutarajia mtoto wa pili na mpenzi wake wa zamani, Tristan Thompson.

"Kuna kitu ambacho niko tayari kuzungumzia," alisema Khloe mwenye umri wa miaka 38, akiliambia Gazeti la Us Weekly wakati 'trela' la msimu wa pili wa kipindi cha maisha halisi ya familia ya The Kardashians, iliyotolewa Jumanne.

"Tristan na mimi tutapata mtoto mwingine na inapaswa kuwa wakati wa kusisimua sana na ni uzoefu tofauti."

Trela hiyo inaangazia Khloé anapojiandaa kushiriki na ulimwengu kwamba anatarajia mtoto wake wa pili na nyota huyo wa mpira wa kikapu mwenye umri wa miaka 31, licha ya hivi karibuni kuhusishwa kutoka kimapenzi na Maralee Nichols.

Wanandoa hao wa zamani waliingia kwenye mzozo Novemba 2021, kabla tu ya Khloe kugundua kuwa mpenzi wake huyo mzaliwa wa Canada alikuwa na mahusiano na mwanamitindo Nichols, ambaye alimshtaki kwa matunzo ya ujauzito.

Dada yake Kim ambaye yupo kwenye familia ya kipindi cha Keeping Up With the Kardashians, ndiye aliyegundua kuwa Thompson amempa ujauzito mwanamke mwingine kupitia kesi hiyo mwezi mmoja baadaye.

Nichols alizaa mtoto wa kiume, Theo, Desemba 2021 na Thompson alithibitishwa kuwa baba wa mtoto huyo kupitia vipimo vya DNA mwezi mmoja baadaye.

Licha ya kutokuwa kimahusiano kwa sasa, wawili hao watamtarajia mtoto huyo wa pili.

"Khloé na Tristan hawajarudiana. Hawajazungumza tangu Desemba," kilisema chanzo kimoja kikinukuliwa na TMZ.com

Msimu wa pili wa The Kardashians utaonyeshwa kwa mara ya kwanza leo Alhamisi, Septemba 22.

## PAULA: ALIYEPEWA KAPEWA TU

**Na Mwandishi Wetu**



MREMBO, mwanamitindo na mjasiriamali maarufu kupitia mitandao ya kijamii, Paula Kajala, amesema kwa sasa yeye anamshukuru Mungu kwani ana uwezo wa kufanya lolote, huku akifurahia maisha.

Kupitia ukurasa wake wa instagram, mrembo huyo ambaye ni mtoto wa Kajala Masanja na produza mkongwe wa muziki wa Bongo Fleva nchini, Paul Khalfan Majani, amesema mtu yeyote hatakiwi kuwa na makasiriko naye.

Hivi karibuni alikuwa Dubai ambako alikuwa akila maisha, ambapo amesema hakuna haja ya mtu kuwa na makasiriko anapomuona mwenzake amefanikiwa kwani kila mtu anapata riziki yake kutoka kwa Mungu.

"Aliyepewa kapewa tu, wewe huna haja ya kuwa na makasiriko kwani anayetoa ni mmoja tu; ni Mungu hivyo inategemea namna ulivyomuomba," aliandika.

## COUNTRY WIZZY ALIOGOPA SANA KUPATA MTOTO



RAPA Country Wizzy ameweka wazi kuwa kwa mara ya kwanza alivyosikia kuwa mpenzi wake ni mjamzito hakuwa tayari kabisa kupata mtoto na alichanganyikiwa.

Kupitia kwenye kipindi cha FreshWeekend, Country aliulizwa vitu ambavyo vimetokea kwenye mahusiano yake ambavyo hawezi kuvisahau.

"'Nilidata' kwa sababu sikuwa tayari mimi kupata mtoto. Nilimwambia mama yake atoe lakini akakataa.

"Siku zilivyokuwa zinakwenda mimi kila mwezi nilikuwa 'nadata'. Nilikuwa naogopa sana mtoto.

"Lakini, nilikuja kufurahi sana alipojifungua na mimi nikawa baba, nilifurahi sana," alisema.

# KIDUKU, MANDONGA WATAMBA KUTOA VICHAPO VIKALI MTWARA

**Saada Akida na Baraka Jamali,** MTWARA

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kassim 'Twaha Kiduku', amesema yupo fiti kumkabili mpinzani wake, Abdo Khaled kutoka Misri.

Pambano hilo ambalo litafanyika Jumamosi katika Uwanja wa Nagwanda Sijaona, litatanguliwa na mapambano 12 ya utangulizi likiwamo la Karim Mandonga na Salim Abeid.

**Mabondia hao wamewasili Mtwara tangu jana na wapo tayari kwa pambano hilo, ambalo kwa Kiduku litakuwa la raundi 10 kuwania Mkanda wa Ubingwa wa UBO uzito wa kilogramu 76.**

Akizungumza na gazeti hili jana, bondia huyo alisema amejiandaa vema kuelekea katika pambano hilo ambalo linasubiriwa kwa hamu na wadau wa masumbwi.

"Nimejiandaa vizuri, naendelea na mazoezi mepesi, namuomba Mungu niwe fiti hadi siku ya pambano ili kufanya kitu kizuri," alisema Kiduku.

Alisema amepata baraka zote kutoka kwa viongozi wa mkoa wake, akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, na kuwahakikisha hatawaangusha na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania.

"Shoo shoo bendera chuma mlingoti chuma sijaja bure Mtwara Abdo Khaled lazima akae, simfikishi raundi ya nne atakwenda kusimulia kwao Misri Kiduku ni nani.

"Hii ni baraka kubwa kwangu, kwani nimepata baraka zote naamini pambano litakuwa nzuri, muhimu ni uzima na afya bora, nimejiandaa vizuri kwa ajili ya kumchapa mpinzani wangu," alisema Kiduku baada ya kupata mapokezi mazuri wilayani Mtwara.

Katika mapokezi hayo, yaliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya, ambaye ni mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mkoa, yalianzia Uwanja wa Ndege wa Mtwara kwa kuzunguka mitaa mbalimbali ya mkoani hapo kabla ya kwenda kwa Mkuu wa Mkoa, Kanali Ahmed Abasi Ahmed, ambaye aliwakaribisha mabondia hao mkoani hapa.

Kwa upande wa Mandonga ambae alikuwa kivutio kikubwa kwa wana Mtwara wengi, waliojitokeza kumpokea, alitamba kumpasua Salim Abeid ili akasimulie kwa watoto wenziwe ambao wanatamani kukutana naye huku akidai yeye si saizi yake.

"Nitaisimamisha Mtwara na dunia itajua Mandongo ni mtu gani. 'Mandonga Mtu Kazi' nitampasua Salim ili akawasimulie watoto wenziwe ambao wanatamani kukutana na mimi," alisema Mandonga.

Kwa upande wa Promota wa Pambano hilo, Selemani Semunyu, alisema maandalizi yamekamilika kwa asilimia kubwa na kwamba mabondia wanaendelea kujifua katika kambi zao ili kuonyesha burudani nzuri.

"Tunamshukuru Mungu maandalizi yamekamilika kwa asilimia kubwa, inasubiriwa siku ya upimaji uzito ambapo ndiyo itadhihirisha kama pambano lipo," alisema Semunyu.

Twaha Kiduku anashuka ulingoni akiwa na kumbukumbu ya kushinda pambano lake dhidi ya Alex Kabangu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) lililofanyika Machi 26, mwaka huu mjini Morogoro.

Mbali na pambano la utangulizi kati ya Mandonga na Salim mapambano mengine ya utangulizi yalikuwa kati ya Nasra Msami dhidi ya Halima Bandora, Francis Miyeyusho atazichapa na Adam Lazoro na Selema Galileo dhidi ya Shaban Ndaro.

Wengine ni Alto Kyenga dhidi ya Ibrahim Tamba, Bosco Bakari atazichapa na Maliki Deo, huku Joseph Mchapeni akipanda ulingoni dhidi ya Pascal Manyota.

## MAVETERAN...



Mchezaji wa All Stars Veteran, Faje Mayanga (kushoto) na Ally Hamza wa timu ya Kinyerezi Veteran, wakiwania mpira kwenye mechi iliyopigwa viwanja vya JK Parks, Kidongo Chekundu jijini Dar es Salaam juzi. All Stars Veteran ilishinda kwa bao 1-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Semwogerere kocha mkuu mpya Pamba

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa zamani wa timu ya Taifa ya Uganda Cranes, George Semwogerere, ameteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa Pamba kwa ajili ya kukinoa kikosi hicho kwenye Ligi ya Championship.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo, imesema wamefikia makubaliano na kocha huyo kwa ajili ya kuhakikisha timu inafanya vizuri msimu huu na kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunayo furaha kuwajulisha kuwa tumeingia makubaliano ya kimkataba na kocha George Semwogerere kutoka nchini Uganda kuwa kocha mkuu wa kikosi chetu.

"Tunaamini tutayafikia malengo kutokana na uwezo wa kocha huyo pamoja kulifahamu soka la Tanzania kwa muda mrefu. Semwogerere aliwahi kuwa nahodha wa timu ya Taifa ya Uganda 'The Cranes' na alifanya makubwa sana," ilihitimisha taarifa hiyo.

Alikuwa mchezaji mahiri wa timu ya Express na timu ya Taifa ya Uganda miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka 1990, akicheza pamoja na aliyewahi kuwa Kocha wa Simba, Jackson Mayanja, Majid Musisi, Idd Batambuze, Paul Hasule, Issa Ssekatawa na wengineo.

Pamba imemchukua kocha huyo baada ya Mkenya Yusuph Chipo kutimkia Coastal Union na hii ikitokana na kumpoteza aliyekuwa kocha wake mkuu, Juma Mgunda ambaye kwa sasa anakaimu nafasi ya Kocha Mkuu kwenye Klabu ya Simba.

# NMB CDF Trophy 2022 kurindima Lugalo

**Na Saada Akida**

KLABU ya Gofu Lugalo inatarajia kuandaa mashindano ya 'NMB CDF Trophy 2022' yanayotarajiwa kufanyika Oktoba Mosi hadi 2, mwaka huu.

Mashindano hayo yatakayofanyika katika viwanja vya Gofu Kawe, Dar es Salaam kwa kushirikisha klabu zote nchini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Brigedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo, alisema mashindano hayo yatashirikisha makundi yote kuanzia wakubwa na watoto (Junior).

"Licha ya kuwapo kwa klabu zote, pia timu kutoka Malawi na viongozi waandamizi wa jeshi hilo wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi wa nchi hiyo, watashiriki mashindano haya makubwa kwa nchi hii, " alisema Luwongo.

Alisema mashindano ya mwaka huu yatakuwa na mvuto kutokana na idadi kubwa ha washiriki ambao wamejisajili.

"Tunaamini mashindano haya ya mwaka huu yatakuwa na mvuto kutokana na idadi ya washiriki na maboresho yaliyofanywa na mdhamini NMB.

Nahodha wa klabu hiyo, Meja Japhet Masai, alisema wachezaji wote walioalikwa wataanza kucheza Ijumaa kwa 'mapro' wote kucheza kuanzia asubuhi na kwa wale wachezaji wa ridhaa watacheza Jumamosi na kwa ujumla mashindano yatakuwa ya siku mbili tu.

Alisema mashindano hayo yatakuwa ya wazi kwa wachezaji kucheza kwa mfumo wa 'close na neti'.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalum NMB, ambao ndiyo wadhamini, Getrude Mallya, alisema wameamua kudhamini mashindano hayo ili kuhakikisha mchezo huo unafika mbali.

"Tunafahamu kuwa mashindano haya yatafanyika chini ya uongozi mpya wa Mkuu wa Majeshi Tanzania na tukaona tuendelee kuwa wadhamini na kutoa kiasi cha Sh. milioni 25," alisema.

Katika mashindano hayo mgeni rasmi anatarajia kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda ambaye ni mlezi wa klabu ya Lugalo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POCHETTINO ATAJWA NICE**
KLABU ya Nice inamatumaini inaweza kumshawishi kocha wa zamani wa Paris St-Germain na Tottenham, Mauricio Pochettino kuchukua nafasi ya Lucien Favre kama kocha mpya wa klabu hiyo ya Ligue 1. (ESPN)

**TIELEMANS HAJUTII ARSENAL**
KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, amesema hajutii kubaki Leicester City msimu huu wa majira ya joto licha ya kuhusishwa na uhamisho wa kujiunga na Arsenal. (*Sky Sports*)

**PULISIC ALIA NA TUCHEL**
WINGA wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 24, amesema "nilifadhaishwa" na uamuzi wa kocha wa zamani, Thomas Tuchel kutomuanzisha katika mchezo wa mkondo wa pili wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid mwaka 2021. (*ESPN*)

**ALLAN KUTIMKIA ARABUNI**
KIUNGO wa kati wa Everton na Brazil, Allan mwenye umri wa miaka 31, ameanzisha mazungumzo ya kujiunga na klabu ya Falme za Kiarabu ya Al-Wahda katika wiki mbili zijazo. (*Football Insider*)

**MMILIKI AISHANGAA CHELSEA**
MMILIKI wa Chelsea na Mkurugenzi wa muda wa Michezo, Todd Boehly, ameshindwa kuelewa ni kwa nini utawala uliopita haukumsajili Aurelien Tchouameni kabla ya kiungo huyo kujiunga na Real Madrid. (*Sport*)

**LEAO KUSAINI**
MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, anataka kusaini mkataba mpya na timu hiyo ya Serie A licha ya kuwavutia Chelsea. (*La Gazzetta Dello Sport, via Teamtalk*)

**MARTINEZ AACHWA ARGENTINA**
MLINZI wa Manchester United, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24 na beki wa kati wa Tottenham Hotspur, Cristian Romero (24), wote wameachwa kwenye kikosi cha Argentina kabla ya mechi mbili za kirafiki kutokana na masuala ya visa. (*Mirror*)

**TOURE NA UKOCHA**
KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester City na Ivory Coast, Yaya Toure, anawasaidia vijana wa chini ya miaka 21 wa Uingereza kujiandaa kwa mechi dhidi ya Italia na Ujerumani anapojaribu kukamilisha kuhitimu ukocha. (*Mail*)

**SHACKLETON KUBAKI MILLWALL**
JAMIE Shackleton wa Leeds United anatarajiwa kuondoka pale kwenye dimba la Elland Road msimu ujao, huku Millwall ikiwa na chaguo la kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, wakati mkopo wake na klabu hiyo utakapomalizika. (*Athletic*)

**JUVE KUMJADILI ALLEGRI**
BODI ya Wakurugenzi ya Juventus itafanya mkutano Ijumaa kujadili mustakabali wa kocha, Massimiliano Allegri, huku miamba hao wa Serie A wakijikuta katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikishinda mara mbili pekee kati ya mechi saba. (*Calciomercato*)

**MINTZLAFF ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA wanamlenga Mtendaji Mkuu wa RB Leipzig, Oliver Mintzlaff kuchukua nafasi ya ukurugenzi wa ufundi pale Stamford Bridge. (*Athletic*)

**VETERE KUSAJILI SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo na kina na mtaalam wa kuajiri, Jeff Vetere ili kuongoza usajili wao wa wachezaji wasizodi umri wa miaka 21. (*Football Insider*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO AWAACHA MBALI MESSI, NEYMAR, MBAPPE

## ●●● Ni katika ushawishi mkubwa Instagram kuelekea Kombe la Dunia Qatar...

**LONDON,** England

CRISTIANO Ronaldo anaongoza dhidi ya Lionel Messi, Neymar Jr na Kylian Mbappe kama mwanasoka mwenye ushawishi mkubwa zaidi kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram kuelekea Kombe la Dunia la 2022 baadaye mwaka huu.

**Mshambuliaji huyo wa Ureno amekuwa na ongezeko la asilimia 48 la wafuasi wake kwenye mtandao huo kwa mwaka uliopita.**

Ana wastani wa zaidi ya thamani ya dola milioni 3.5 katika kila chapisho, kwa mujibu wa watafiti wa Nielsen Gracenote.

Nyota mwenzake wa Manchester United, Jadon Sancho ndiye mchezaji wa Uingereza mwenye ushawishi mkubwa zaidi, huku Gavi akiwa ndiye nyota mpya aliyeibuka na ongezeko kubwa la wafuasi kwa asilimia 51.65.

Orodha hiyo ni kwa mujibu wa vipimo vya ushawishi wa Nielsen, ambavyo hutathmini jumla ya wafuasi, ukuaji wa wafuasi, kiwango cha ushiriki na wastani wa thamani ya kila chapisho kwenye Instagram ili kutoa jumla ya thamani.

Iliorodhesha wachezaji ambao wanatarajiwa kushiriki katika Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar.

Ronaldo ana wafuasi milioni 480 kwenye Instagram, huku Messi wa Argentina akifuatia na watu milioni 360 - ukiwa sawa na ukuaji wa asilimia 38 katika miezi 12 iliyopita - na kila chapisho lake katika mtandao lina thamani ya dola milioni 2.6.

Washambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar na Mbappe wanashikilia nafasi ya tatu na nne, kila mmoja akiwa na wastani wa zaidi ya thamani ya dola milioni moja kwa kila chapisho.

Vinicius Junior wa Brazil yupo nafasi ya tano alikuwa na ukuaji mkubwa zaidi wa wafuasi ikilinganishwa na mchezaji yeyote aliyeongeza kwa asilimia 90, baada ya kufunga bao la ushindi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiichezea Real Madrid dhidi ya Liverpool, huku Karim Benzema akishika nafasi ya sita.

Paulo Dybala wa Argentina na AS Roma, yupo nafasi ya saba na Mfaransa N'Golo Kante anashika nafasi ya nane, huku Paul Pogba akishika nafasi ya tisa na 10-bora imefungwa na Sergio Ramos.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,033,2

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 23 SEPTEMBA 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/22 | 20:30 | Bastia Borgo vs Le Mans | 2.78 | 3.13 | 2.46 |
| 02. 23/09/22 | 20:30 | Saint Brieuc vs Orleans | 2.48 | 3.15 | 2.75 |
| 03. 23/09/22 | 20:30 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 2.35 | 3.14 | 2.94 |
| 04. 23/09/22 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Avranches | 2.63 | 3.08 | 2.63 |
| 05. 23/09/22 | 20:30 | FC Versailles 78 vs Nancy | 2.32 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/09/22 | 20:30 | Sedan vs Le Puy | 2.34 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 23/09/22 | 21:00 | Ireland U21 vs Israel U21 | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 23/09/22 | 21:45 | Italy vs England | 2.62 | 3.17 | 2.68 |
| 09. 23/09/22 | 21:45 | Finland vs Romania | 2.29 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 23/09/22 | 21:45 | Alloa Athletic vs Airdrieonians | 2.43 | 3.63 | 2.43 |
| 11. 23/09/22 | 22:00 | Dordrecht vs Maastricht | 2.33 | 3.53 | 2.68 |
| 12. 23/09/22 | 22:00 | Morocco vs Chile | 2.70 | 3.27 | 2.60 |
| 13. 23/09/22 | 22:00 | The New Saints vs Dundee FC | 2.64 | 3.57 | 2.27 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, airtel money, ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# PEDRI AIPA HISPANIA KOMBE LA DUNIA

**MADRID, Hispania**

PEDRI amefichua kwamba, Hispania iliyopo chini ya kocha, Luis Enrique, ni miongoni mwa timu inayopewa nafasi kubwa ya kushinda Kombe la Dunia lijalo nchini Qatar baadaye mwaka huu.

'La Roja' hao wamevumilia kampeni za kusikitisha za Kombe la Dunia tangu ilipotwaa taji hilo mwaka 2010, na kutupwa nje katika hatua ya makundi mwaka 2014 kabla ya kushindwa kwa mikwaju ya penalti hatua ya 16 bora na wenyeji Urusi miaka minne iliyopita.

Hata hivyo, kuibuka kwa vipaji kadhaa vya vijana - ikiwa ni pamoja na Pedri na kiungo mwenza wa Barcelona, Gavi - kumemwezesha Enrique kuanzisha upya mtindo wa kucheza unaotegemea umiliki wa mpira ambao ulikuwa maarufu chini ya kocha, Vicente del Bosque.

Huku Hispania ikitarajiwa kuanza kampeni ya Kombe la Dunia dhidi ya Costa Rica katika kipindi cha zaidi ya miezi miwili tu, Pedri haoni sababu wao washindwe kubeba taji hlo.

"Pengine watu hawatarajii mengi kutoka kwetu, hawatuoni kama wenye nafasi, lakini ndani tunajiona kama tuna nafasi kubwa," alisema akiiambia Sport.

"Hatutavaa medali bila kufanya lolote, tukifanya kazi inavyostahili nafasi itakuja.

"Siku zote kuna shinikizo kwa Barca na timu ya taifa. Lazima ujaribu kuwa bora, kuwa mtulivu na kufurahia.

"Hapa na Barca tuna timu kwa kila kitu. Tunafanya kazi ili mwisho wa msimu tuweze kushinda kila kitu tunachocheza."

Pedri, ambaye atafikisha umri wa miaka 20 Novemba, tayari ameshacheza mechi 12 za kimataifa na kujidhihirisha kuwa mchezaji muhimu wa Barcelona.

# UEFA yaitoa Urusi kwenye Euro 2024

**PARIS, Ufaransa**

SHIRIKISHO la Soka la Ulaya (UEFA), limethibitisha kuwa Urusi haitajumuishwa katika droo ya mwezi ujao ya kufuzu kwa michuano ya Ulaya (Euro 2024).

Urusi pia imetengwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), na UEFA imefuata baaada ya uvamizi wa kijesh nchini Ukraine Februari, mwaka huu huku timu za taifa na klabu za nchi hiyo zikipigwa marufuku kushiriki mashindano yoyote ya bara la Ulaya au kimataifa.

UEFA ilithibitisha kabla ya msimu wa 2022-23 kwamba klabu za Urusi zitatengwa kushiriki mashindano yao msimu huu, ingawa Euro 2024 haikutajwa hapo awali.

Hata hivyo, huku wakithibitisha utaratibu wa droo ya mchujo itakayofanyika Oktoba 9, mwaka huu, UEFA sasa wamethibitisha Urusi haitakuwa miongoni mwa timu 53 zitakazoshiriki.

Taarifa ilisema: "Timu zote za Urusi kwa sasa zimesimamishwa baada ya uamuzi wa Kamati ya Utendaji ya UEFA ya Februari 28, 2022, ambayo imethibitishwa zaidi na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo mnamo Julai 15, 2022.

"Kwa hiyo Urusi haijajumuishwa katika droo ya kufuzu kwa ubingwa wa Soka la Ulaya wa UEFA 2022-24."

Ujerumani, wenyeji wa michuano ya Euro 2024 inafuzu moja kwa moja, pia hawatakuwa kwenye droo ya mwezi ujao, ambayo itatoa makundi saba ya timu tano na makundi matatu ya timu sita.

## HABARI MICHEZO


283,276/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 24/09/22 | 17:00 | Morecambe vs Cambridge Utd | 2.85 | 3.30 | 2.44 |
| 02. 24/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Charlton | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 24/09/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Accrington | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 04. 24/09/22 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 05. 24/09/22 | 17:00 | Hartlepool vs Gillingham | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 06. 24/09/22 | 17:00 | Sutton United vs Salford City | 2.42 | 3.28 | 2.88 |
| 07. 24/09/22 | 17:15 | Mirandes vs Zaragoza | 2.98 | 3.18 | 2.41 |
| 08. 24/09/22 | 19:00 | Sarmiento vs Arsenal Sarandi | 2.36 | 3.14 | 3.24 |
| 09. 24/09/22 | 19:30 | Malaga vs Villarreal B | 2.31 | 3.24 | 3.09 |
| 10. 24/09/22 | 19:30 | Ponferradina vs Tenerife | 2.73 | 3.13 | 2.63 |
| 11. 24/09/22 | 21:30 | Lanus vs San Lorenzo | 2.49 | 3.14 | 3.04 |
| 12. 24/09/22 | 21:45 | Israel vs Albania | 2.41 | 3.18 | 3.08 |
| 13. 24/09/22 | 22:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.36 | 3.12 | 3.07 |
| 14. 25/09/22 | 04:00 | Mexico vs Peru | 2.29 | 3.21 | 3.21 |
| 15. 25/09/226 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.77 | 3.88 | 2.30 |
| 16. 25/09/22 | 15:00 | Burgos vs Levante | 3.39 | 3.04 | 2.26 |
| 17. 25/09/22 | 17:15 | Lugo vs Real Oviedo | 3.24 | 2.99 | 2.37 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 22/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3146 | Australia vs New Zealand | 1.54 | 4.17 | 5.90 |
| 13:30 | 2391 | Trinidad and Tobago vs Tajikistan | 2.02 | 3.35 | 3.26 |
| 13:30 | 5845 | Kasetsart University FC vs Ranong United | 2.20 | 3.35 | 3.05 |
| 15:00 | 4069 | Viking FK 2 vs FK Haugesund 2 | 1.58 | 4.72 | 3.89 |
| 16:00 | 3890 | Bujumbura City vs Olympic Star | 2.85 | 2.70 | 2.85 |
| 16:00 | 5048 | CA Platense vs Rosario Central Reserve | 2.99 | 3.09 | 2.26 |
| 17:00 | 1001 | Patronato Reserve vs Defensa Y Justicia Reserve | 3.20 | 3.10 | 2.15 |
| 17:00 | 1380 | Newells Old Boys vs Independiente Reserve | 2.04 | 3.18 | 3.37 |
| 17:00 | 2559 | Kazakhstan vs Belarus | 2.21 | 3.03 | 3.48 |
| 17:00 | 2606 | Deportivo Toluca U20 vs Santos Laguna U20 | 2.75 | 3.43 | 2.25 |
| 17:00 | 2812 | Monterrey U20 vs Puebla U20 | 2.19 | 3.43 | 2.84 |
| 17:00 | 4061 | Kustosija vs NK Vukovar 91 | 2.61 | 3.06 | 2.56 |
| 18:30 | 3175 | Sola vs Vidar | 2.08 | 4.24 | 2.61 |
| 18:30 | 3237 | Italy U21 vs England U21 | 3.10 | 3.65 | 2.06 |
| 19:00 | 1425 | ASEC Mimosas vs Societe Omnisport | 1.40 | 3.82 | 8.03 |
| 19:00 | 3584 | Iceland vs Venezuela | 2.37 | 3.47 | 2.85 |
| 19:00 | 4516 | Latvia vs Moldova | 1.66 | 3.63 | 5.25 |
| 19:30 | 2255 | Ironi Tiberias vs Hapoel Ramat Gan | 2.67 | 2.98 | 2.78 |
| 19:30 | 3188 | Nazareth Ilit vs Hapoel Rishon Lezion | 2.71 | 3.07 | 2.66 |
| 19:30 | 4004 | Hapoel Acre vs Maccabi Jaffa | 3.02 | 2.92 | 2.52 |
| 19:30 | 4145 | Hapoel Kfar Saba vs SC Kfar Qasem | 2.68 | 3.09 | 2.68 |
| 19:30 | 4312 | Ahi Nazareth vs Ironi Hasharon | 2.20 | 2.97 | 3.57 |
| 20:00 | 1568 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Katamon | 3.09 | 3.05 | 2.23 |
| 21:00 | 2049 | Switzerland U21 vs Japan U21 | 1.94 | 3.58 | 3.28 |
| 21:00 | 3078 | Flamengo SP U20 vs Ituano FC U20 | 2.90 | 2.99 | 2.38 |
| 21:00 | 3247 | Floya vs Skjervoy | 1.17 | 6.89 | 9.85 |
| 21:00 | 4410 | Corinthians SP U20 vs Desportivo Brasil U20 | 1.64 | 3.69 | 4.53 |
| 21:00 | 4851 | Ponte Preta SP U20 vs FC SKA Brasil SP U20 | 1.68 | 3.60 | 4.44 |
| 21:00 | 5112 | Palmeiras SP U20 vs Portuguesa Desportos SP U20 | 1.40 | 4.41 | 6.27 |
| 21:00 | 5188 | Capivariano SP U20 vs Mirassol FC U20 | 2.16 | 3.19 | 3.09 |
| 21:00 | 5218 | Santos SP U20 vs Guarani SP U20 | 1.36 | 4.52 | 6.87 |
| 21:00 | 5450 | Ferroviaria SP U20 vs Ibrachina FC SP U20 | 1.98 | 3.24 | 3.48 |
| 21:00 | 5577 | SAO Paulo SP U20 vs Penapolense SP U20 | 1.32 | 4.91 | 7.07 |
| 21:45 | 1429 | Lithuania vs Faroe Islands | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 21:45 | 1510 | Croatia vs Denmark | 2.47 | 3.19 | 2.84 |
| 21:45 | 2273 | France vs Austria | 1.38 | 4.76 | 7.49 |
| 21:45 | 2469 | Liechtenstein vs Andorra | 3.68 | 3.13 | 2.09 |
| 21:45 | 3451 | Morton vs Ayr United | 3.35 | 3.26 | 2.02 |
| 21:45 | 3636 | Belgium vs Wales | 1.36 | 4.74 | 8.06 |
| 21:45 | 4427 | Poland vs Netherlands | 3.39 | 3.54 | 2.03 |
| 21:45 | 4544 | Slovakia vs Azerbaijan | 1.37 | 4.54 | 8.27 |
| 21:45 | 4749 | Shelbourne vs Shamrock Rovers | 4.41 | 3.38 | 1.73 |
| 21:45 | 4967 | Turkey vs Luxembourg | 1.24 | 5.67 | 11.13 |
| 21:45 | 5463 | Queen of South vs Edinburgh City | 1.51 | 4.50 | 4.69 |
| 22:00 | 4753 | Patriotas FC vs Alianza Petrolera | 1.99 | 3.06 | 3.70 |

IJUMAA - 23/09/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 5167 | Zacatepec vs Cancun FC | 1.55 | 3.83 | 5.11 |
| 02:10 | 1867 | Independiente Medellin vs Deportivo Pereira | 1.90 | 3.20 | 3.84 |
| 03:05 | 1003 | CF Atlante vs Venados FC | 1.50 | 3.89 | 5.71 |
| 03:30 | 2817 | Vila Nova GO vs CRB AL | 2.20 | 2.80 | 3.48 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# JANG'OMBE, POLISI MAMBO MAGUMU LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Polisi Zanzibar na Taifa Jang'ombe zimeendelea kupata matokeo mabaya katika Ligi Kuu ya Zanzibar inayoendelea visiwani hapa.

Katika mchezo wa juzi uliozikutanisha timu hizo, zimetoka sare ya bila kufungana kwenye muendelezo wa ligi hiyo, mechi ikipigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri.

Kwa matokeo hayo, timu zote zimepata sare mbili hadi sasa huku kila moja ikipoteza mchezo mmoja kati ya mitatu ilizocheza, hivyo kuambulia pointi mbili, na kuifanya Polisi kushika nafasi ya 12 na Taifa Jang'ombe ya 13.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu ya Polisi, Ali Mtuli alisema kadri wanavyoshuka dimbani timu wataendelea kuimarika, hivyo ana matumaini mchezo ujao watapata matokeo mazuri.

Alisema kikosi chake katika mchezo huo wa tatu kimecheza vizuri ikilinganishwa na michezo miwili ya awali, hivyo kutokupata matokeo kwenye mechi hiyo kumetokana na ushindani uliokuwapo kutoka kwa wapinzani wao kwa dakika zote 90.

Alisema wachezaji wote walicheza vizuri katika dakika zote na licha ya kushambuliwa mara kadhaa, safu ya ulinzi iliweza kufanya kazi yake vizuri.

"Timu ilicheza vizuri kwa mipango ya kupata alama tatu, lakini tulipata alama moja, hivyo tunajipanga katika mchezo ujao ambao naamini tutapata matokeo mazuri kwa kuwa kikosi chetu hivi sasa kimeshaungana vizuri kupitia michezo hii mitatu.

Timu ya Polisi inatarajia kushuka dimbani Septemba Jumatatu ijayo dhidi ya Uhamiji SC, mchezo utakaochezwa katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 10 alasiri.

Katika Mchezo mwingine uliopigwa juzi, Uhamiaji ilifanikiwa kuwazima majirani zao, timu ya Zimamoto kwa kuwafunga mabao 2-0 mechi hiyo ikipigwa Uwanja wa Amaan saa moja usiku.



Wachezaji wa timu ya Kitunda FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nabi ataka siku 10 za kuimaliza Al Hilal

INATOKA UK. 32

"Nimeandaa programu maalum kwa wachezaji wangu, matarajio yangu siku 10 kuanzia leo hadi siku ya mechi, wachezaji watakuwa imara, hasa safu ya ushambuliaji kuwa makini kwa nafasi wanazozipata katika mechi," alisema Nabi.

Alisema wachezaji wake hawajapata muunganiko mzuri hivyo anahakikisha anaendelea kutengeneza taratibu kikosi chake na kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao ikiwamo dhidi ya Ihefu na Ruvu Shooting na kisha dhidi ya Al Hilal Oktoba 8, mwaka huu.

## Mgunda sasa amulika mambo mawili Simba

INATOKA UK. 32

na makocha wengine, baada ya hapo maamuzi sahihi yatafanyika, sifa anazo na uwezo anao ni miongoni mwa watu ambao bodi itamjadli," alisema.

Katika hatua nyingine alisema vikosi vya timu ya wanaume na wanawake vimeingia kambini tayari kwa majukumu yanayowakabili.

"Kikosi cha timu ya wanaume baada ya mechi dhidi ya Nyasa Big Bullets kilipata mapumziko, kinaingia kambini leo (jana) saa tisa kinatakiwa kuwa kambini kabla ya kuelekea mazoezini Mo Arena Bunju, tayari kuanza maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu Septemba 28 dhidi ya Mbeya City pamoja na raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto.

"Pia kikosi cha timu ya soka ya wanawake, Simba Queens nacho kiliingia kambini Jumatatu kujiandaa na fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu," alisema Ahmed.

Wakati timu ya wanaume ikitarajia kucheza mechi yake kati ya Oktoba 7 hadi 9 nchini Angola, Simba Queens inatarajia kucheza fainali hizo zitakazofanyika nchini Morocco kuanzia Oktoba 30, mwaka huu ikiwa imepangwa Kundi A, pamoja na timu za AS FAR ya Morocco, Green Buffaloes ya Zambia, na Determine Girls ya Liberia.

# Michezo

Alhamisi Septemba 22, 2022


Nipashe


UKURASA 30



**Pedri aipa Hispania Kombe la Dunia**

**TUTAWACHAPA...**




Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas (katikati), akiwa pamoja na mabondia, Twaha Kiduku (kushoto) na Karim Mandonga, ofisini kwake baada ya kuwasili mkoani hapo jana tayari kwa kupanda ulingoni Jumamosi dhidi ya Mmisri Abdo Khaled na Salim Abeid. **HABARI UK. 28. PICHA: Baraka Jamali**

# Mgunda sasa amulika mambo mawili Simba

●●●Naye kujadiliwa sambamba na makocha walioomba kuinoa, Bodi ya Wakurugenzi kujifungia...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

LICHA ya uongozi wa Klabu ya Simba kusema Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda ni miongoni mwa watakaojadiliwa pale Bodi ya Wakurugenzi itakapokaa kujadili makocha waliotuma wasifu wao kuomba kazi ya kukinoa kikosi hicho, mwalimu huyo amesema akili yake ipo kwenye kuzitafuta pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya City na baadaye kwenda kuwawinda Primeiro de Agosto ya Angola.

Simba wanaendelea kutumia mchezo wa Mbeya City kwa kutafuta pointi muhimu kufikia malengo yao ya ligi na kujiimarisha zaidi kwa mchezo wa kwanza wa raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto.

Kikosi cha Simba kitakuwa na kibarua kigumu ugenini kuwakabili Mbeya City, mchezo utakaochezwa Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya na baada ya hapo wataikaribisha Dodoma Jiji Oktoba 2 kabla ya kuifuata Primeiro de Agosto kwa mchezo utakaopigwa kati ya Oktoba 7 hadi 9, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema baada ya mapumziko mafupi wamerudi uwanjani kufanyia kazi mapungufu yao pamoja na maandalizi kuelekea michezo ijayo ikiwamo dhidi ya Mbeya City.

Alisema kabla ya kuanza kujiandaa na mechi ya kimataifa, anafikiria zaidi pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya City, ambao ana anaamini utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya ugumu wa ligi.

"Mechi zote ni muhimu kwetu, tunafanya maandalizi ya mechi iliyopo karibu yetu, kabla ya kucheza mchezo wetu wa hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto, tunahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo yote," alisema Mgunda.

Wakati huo huo, uongozi wa klabu hiyo umesema Mgunda ni miongoni mwa makocha watakaojadiliwa pale Bodi ya Wakurugenzi ya Simba itakapokaa kujadili makocha walioomba kukinoa kikosi hicho.

Akizungumza jana, Dar es Salaam, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema hata hivyo mchakato huo kwa sasa hauna presha sana kama ilivyokuwa awali kutokana na timu kuwa kwenye mikono salama ya Mgunda.

"Mchakato wa kusaka kocha mpya unaendelea na unakwenda vizuri, bado tunaendelea kupitia maombi ili tupate kocha sahihi, kwa sasa presha siyo kubwa ya kutafuta kocha kwa sababu timu iko kwenye mikono salama chini ya Mgunda, kuna utulivu, na hiyo inatupa fursa sisi kutafuta kocha sahihi kwa makini zaidi bila presha, hatuhitaji kufanya makosa tena, tunafanya upembuzi yakinifu ili kupata kocha anayetufaa," alisema Ahmed.

"Katika makocha ambao wametuma maombi yakianza kujadiliwa na yeye Mgunda atakuwa kwenye mjadala, pamoja

INAENDELEA UK. 31

## Nabi ataka siku 10 za kuimaliza Al Hilal

**Na Saada Akida**

HUKU kwa sasa akielekeza akili yake katika mchezo ujao wa Ligi Kuu Bara ugenini dhidi ya Ihefu FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema siku 10 zinamtosha kukiandaa kikosi chake kuhakikisha kinafanya vizuri kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Yanga baada ya kuitoa Zalan FC ya Sudan Kusini katika hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa jumla ya mabao 9-0, raundi ya kwanza sasa itaanzia nyumbani dhidi ya Al Hilal iliyoitoa St. George ya Ethiopia kwa faida ya bao la ugenini baada ya matokeo ya jumla kuwa 2-2.

Al Hilala ilikubali kipigo cha mabao 2-1 ugenini kabla ya kushinda nyumbani kwa bao 1-0, hivyo kunufaika na bao la ugenini, wakati Yanga yenyewe ilishinda mchezo wa kwanza mabao 4-0 na kisha wa marudiano kuibuka na ushindi wa 5-0, shukran kwa straika wao hatari, Fiston Mayele aliyetupia mabao sita kwa kufunga hat-trick katika kila michezo yote miwili.

Tayari Yanga wameanza mazoezi ya utimamu wa mwili 'gym' pale Gymkhana jijini Dar es Salaam kabla ya leo kuanza mazoezi ya uwanjani kwa ajili ya michezo hiyo wakitaka kwanza kumalizana na Ihefu FC Septemba 29 na kisha Ruvu Shooting Oktoba 3, mwaka huu kabla ya kuialika Al Hilal tano baadaye.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Nabi alisema kabla ya kuvaana na Ruvu Shooting, watakuwa wamefanya mazoezi magumu ambayo yatawapa majibu kuelekea katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Alisema mazoezi ya gym yatawasaidia wachezaji wake kuongeza stamina na kuwapa uwezo wa kupambana kwa dakika zote 90, kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye mechi zilizopo.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >